Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Sita – Tarehe 16 Juni, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo nina wauliza maswali tisa na ninawashukuru sana kwani ninasikia walijipanga vizuri, angalau kila chama kina watu watatu na wanasema leo tumuone Mheshimiwa Spika kama atatuchakachua.

Mimi sina lengo la kuchakachua isipokuwa naomba muulize maswali kwa kifupi ili Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kujibu na ili ninyi wote muweze kuuliza na kama Mheshimiwa Mbunge mmoja atakuwa anarefusha maswali basi itakuwa tatizo. Leo hatuna Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa hiyo tunaendelea na wale waliojipanga.

Sasa nitamuita Mheshimiwa Eng. Mohamed Habib Juma Mnyaa.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya dhahabu kuuliza swali fupi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kwanza kabla ya kukuuliza swali fupi uniruhusu ninukuu vifungu viwili vya Katiba, katika Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 73 inayoeleza masharti ya kazi ya Wabunge. Sheria ya mwaka 1984 Namba 15 Ibara ya 13.

Ibara ya 73 inasema: “Wabunge wote wa aina zote watashika madaraka yao kwa mujibu wa Katiba hii na watalipwa mshahara, posho na malipo mengine kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge.”

Pia, Ibara ya 26 inasema kwamba: “Kila mtu ana wajibu wa kufuata na kutii Katiba hii na Sheria za Jamhuri ya Muungano”.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika kadhia hii iliyoingia hivi karibuni ambayo ilianzia kwa Wabunge mpaka kwa wanaharakati na vyombo vya habari, ambayo imesababisha kuleta fitna baina ya Wabunge na wananchi wao. Serikali inatoa tamko gani kuhusu kadhia hii?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Eng. Mohamed Habib Juma Mnyaa, kwa kawaida huwa anauliza maswali mengine magumu lakini leo kidogo afadhali. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema kwamba stahili za Wabunge kwa bahati nzuri zipo kwa mujibu wa Katiba na Sheria ambazo zinatungwa baada ya pale au taratibu nyingine zitakazokuwa zimewekwa na Serikali.

Lakini pengine kabla sijasema hili labda kwa manufaa ya Watanzania, niseme kwamba posho hizi hasahasa ni makundi mawili. Zipo posho ambazo tunasema Katibu Mkuu ambaye ndiye mtendaji mkuu wa shughuli ndani ya Wizara hawezi kuzirekebisha kwa namna yoyote ile kwa sababu ni stahili ambazo zipo kwa mujibu wa sheria au taratibu ambazo zimewekwa, na zipo posho ambazo Katibu Mkuu anaweza akazirekebisha kwa kadri atavyoona inafaa. Hizi ambazo Katibu Mkuu anaweza tunaziita ni *discretionary*, hili kundi la kwanza tunasema ni *non discretionary* posho ambazo hazina namna.

Kwenye kundi hili tunaloliita ni *non discretionary* ni zile ambazo kama ulivyosema, kwa mfano zile ambazo zimetokana na matakwa ya Katiba ya Sheria hakuna namna itabidi mpaka kama mkitaka kurekebisha mrudi huko mkafanye marekebisho ndiyo muweze kurejea tena na utaratibu wa kawaida na hizi ziko nyingi. Lakini zipo nyingine hata kama si kwa mujibu wa sheria lakini zimewekwa taratibu ambazo ni lazima tuzizingatie. Nitatoa mfano tu. *(Makofi)*

Kwa mfano, Diwani halipwi mshahara bali analipwa posho. Kwa hiyo, utakapokuwa unazungumza posho ujue ni pamoja na posho ya Diwani ambayo ndiyo tumemtengenezea utaratibu kwamba na yeye ndiyo stahili katika kumuwezesha kutimiza majukumu yake.

Kuna mifano mingine mingi tu, lakini kwa mfano Askari wana kitu wanaita *ration allowance* ni utaratibu ambao uko ndani ya utaratibu huo wa Majeshi ya Polisi na Jeshi la Wananchi. Hata ungefanya nini huwezi ukaenda kumpokonya *ration allowance* Askari ambaye tumemuwekea kwa ajili ya kuwezesha kutekeleza majukumu yake inavyotakiwa. Kwa hiyo, posho zile ambazo ni *discretionary* ndiyo hizo ambazo mnasema kwa mfano *honorarium*, mmewekewa kakifungu watu wanachapa kazi mpaka saa nane za usiku, unaweza kabisa ukatoa *honorarium* kwa watendaji wako.

Kwa mfano pia katika maandalizi ya bajeti Makatibu Wakuu na Wataalamu wengi wanafanya kazi *over time* lakini kwa taratibu zilivyo hata ningekesha mimi mpaka asubuhi ziwezi kulipwa *over time.* Sheria kwa nia njema tu na taratibu ziliona watu wa namna hii ni vizuri kuwatunuku kitu kidogo kwa kazi waliyoionyesha kwa kujitolea

muda wote. Si dhambi ni kitu ambacho kiko pale ni namna ya kuwa-*motivate* na kuwafanya waweze wafanye kazi vizuri zaidi.

Kwa hiyo, tunazo posho za namna hiyo na tunaweza tukaziangalia kwa makundi mbalimbali *specifically* hili la Wabunge. Wabunge kwenye Katiba ndivyo ilivyo na sheria zilizotungwa ndivyo zinavyosema na mara nyingi tunachofanya ni nini? Inapokuwa ni kanuni mara nyingi Spika atamuomba Mheshimiwa Rais kibali cha posho aina fulani ili iweze kuwa ni sehemu ya utaratibu wa kuwasaidia Wabunge, hicho kikishafanyika Mbunge atalipwa.

Sasa najua kumekuwa na maneno mengi sana kana kwamba ni jambo kubwa la ajabu sana, mimi nasema si kubwa sana hili na kwa mimi nikilitazama na ninalisema hili kwa nia njema tu, huyu Mbunge hata hicho mnachokiita posho ambacho tunakipigia kelele sehemu kubwa wala hatumii yeye binafsi, ndiyo! Sehemu kubwa ya posho anazopata Mbunge ndiyo hizohizo hajatoka hata hatua 10 unaambiwa kuna mtu mlangoni anakungojea, unaingiza mkono mfukoni unamkabidhi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni jambo lililofanyika kwa nia njema kuwasaidia Wabunge angalau waweze kupunguza matatizo mengine yanayowakabili kwa sababu wanakabiliwa na mambo mengi *personal.*

Lakini kubwa ni watu ambao wanawawakilisha na wengine wala siyo wa Majimbo yao, siyo wa Majimbo yao hata kidogo. Unatoka tu nje unapambana na mtu anakwambia Mzee sina nauli ya kwenda kijijini nimeishiwa. Mara ngapi hapa tumebanwa mashati? Ni mara nyingi sana.

Kwa hiyo, ingawa kweli ni jambo ambalo limekuzwa na kufanywa la ajabu, lakini mimi nasema Serikali ilichosema tuziangalie posho hizi kwa kuzingatia mpango tuliouweka ili tuone namna tunavyoweza kuziwianisha au kuzi-*rationalize* kwa sababu bado kwa vyovyote vile mimi ninavyoona itakuwa ni busara zaidi hicho kidogo ambacho kitakuwa kimewekwa kwa lengo hilo angalau kikaingizwa hata kwenye mshahara wake kiendelee kumsaidia huyu mtumishi au Mbunge kutekeleza majukumu yake inavyotakiwa. Hii kwamba ukifanya hivyo pengine utaonekena Mzalendo sana, mimi nasema tuwe wakweli kwa upande wetu.

Nalisema hili kwa sababu najua nimekuwa Naibu Waziri, Waziri na Waziri Mkuu najua kinachowapata Wabunge wengi na Bungeni hapa nani asiyejua? Watu wanaishia kukopa benki usiku na mchana hapa. Nimesema kwa kirefu sana lakini kwa kifupi nasema tu kwamba Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa ni jambo ambalo Serikali tumesema kwa sababu limesemwa mno na limetoa *wrong impressions* kwa Watanzania, wajibu wangu mimi kama Waziri Mkuu ni kusema *fine*, yamesemwa lakini wajibu wetu vilevile ni kuwaeleza Watanzania wasije wakaliona jambo hili kama vile ni jambo la ajabu, hapana! Sisi tutaliangalia *in that context* na ninaamini kabisa Watanzania watatuelewa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyaa bado utauliza swali la nyongeza? Mbona limejibiwa vizuri waachie wenzako nafasi tafadhali.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Wabunge sote tumeapa hapa na kwa kuwa bado tunaitumikia Katiba hii, ni nini hatua za Serikali kwa wale wanaojaribu kuvunja Katiba hii? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Ni kwamba anataka kuzua vita juu ya vita lakini hakuna sababu. Mimi ninachosema tu ni kwamba ndiyo, maana alianza mwenzangu Kabwe na baadaye likaonekana limepamba moto, sawa! Mimi nasema ni jambo jema na kamwe si wa kwanza wapo waliowahi kujitosa huko siku za nyuma wakatoa mishahara yao kwa watu. Katika hii ambapo hatujafikia uamuzi wa mwisho kwamba ni nini kifanyike mtu unaweza ukasema mimi posho yangu sitaki nataka ibaki Hazina ikafanye shughuli za Maendeleo. Lakini mimi ninachoogopa ni kufanya jambo hili lionekane kama vile ni kubwa na kwa maana ya Wabunge hawa kwa hiyo lote sasa ni uamuzi wa Wabunge wa CHADEMA, mimi najua wapo CHADEMA wengi tu hapa wanamezea mate tu lakini wafanye nini? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na ninapenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumekuwa tukisikia kwamba wakimbizi kutoka Rwanda na Burundi ambao wamepewa uraia Tanzania watahamishiwa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Kama ni kweli, ni kwa nini Serikali iwahamishie wakimbizi hawa Mikoa ya Lindi na Mtwara wakati wakimbizi hawa wamepata uraia na wako huru kuishi mahali popote na wanaweza kuchangua kuishi mahali popote kama Watanzania wengine wanavyofanya?

La pili, tumekuwa tukisikia madhara yanayoletwa na wakimbizi hawa katika Mikoa ya Kagera na Kigoma. Mheshimiwa Waziri Mkuu, huoni sasa kwa kuwapeleka wakimbizi Mikoa ya Mtwara na Lindi ni kuhamisha madhara yale ambayo yamekuwa yakionekana Mkoa wa Kigoma na Kagera kama vile ujambazi, watu kuuawa, uharibifu wa mazingira na kadhalika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Na Njombe pia wanaambiwa watakwenda. *(Kicheko)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba tu niseme kwamba namshukuru sana Mheshimiwa Faith Mitambo.

Jambo hili nimeanza kulisikia kitambo kidogo hivi, si jepesi sana kulizungumzia kwa sababu lina unyeti wake lakini naomba niseme tu kwa nia njema kwamba jambo hili lilitokana na uamuzi wa Serikali baada ya kuombwa na wenzetu ambao ndiyo

wanakabiliwa na tatizo hilo kutokana na sababu fulanifulani na Umoja wa Mataifa chini ya *UNHCR* ndiyo waliojaribu pia ku- *spear head* hilo wazo. Sasa Tanzania si mara ya kwanza kufanya hivi, Mwalimu aliwahi kufanya hivyo siku za nyuma akatoa uraia kwa waliokuwa wanaitwa wakimbizi wakati ule na tunao mpaka leo wanaishi hapa Tanzania.

Kwa hiyo, kutokana na zile fikra tu za kibinadamu za kuona kwamba hawa wananchi ni wale ambao kwa namna moja ama nyingine wamekuwa wakikumbwa na matatizo mbalimbali na wamekuwepo hapa muda mrefu na wengine wamezaliwa hapahapa kundi kubwa ni wale waliozaliwa hapa na wengine ni wazee sana tangu wametoka huko kwao miaka ya 1972. Kwa hiyo, Serikali ikaona pengine si vibaya kama sehemu ya Jumuiya ya Umoja wa Mataifa, basi jambo hili tulitazame tuone namna gani tunaweza tukasaidiana.

Kwa hiyo, katika maamuzi yaliyofanyika ikawa ni kwamba kwa wale ambao wanataka kurudi kwao tuwasaidiei warudi kwao, wale ambao wanafikiria kule kwao hata kusema unakwenda wapi, hawana na wamekaa hapa muda mrefu wana umri mdogo uliobaki basi ni hiari yao wao wenyewe kubaki hapa tuwakubali wabaki hapa. Kwa hiyo, katika zoezi hilo ndiyo tukapata watu kama 160,000 ambao tuliona kwamba wangeweza kubaki baada ya mchujo.

Pili, ikawa ni kwamba kwa sababu wameishi katika makambi kama wakimbizi, si vizuri wakaendelea kuishi katika hisia za ukimbizi ni bora waondokane na hizo hisia maadamu tuko katika mchakato wa kuwapa uraia. Ndiyo maana uamuzi ukasema hao wakimbizi 166 tuwatawanye katika familia ndogondogo nchi nzima karibu katika mikoa yote. Kwanza, ni kwa sababu hatukutaka waendelee kuonekana kama wako kundi moja lakini pili tulitaka vilevile waweze kuingia katika maisha ya kijamii kwa haraka zaidi wanapokuwa ni familia au kaya moja ama mbili. Ndiyo maana ule uamuzi umeuona si Lindi na Mtwara ni mikoa karibu yote ukiondoa mikoa ile ambayo imebeba mzigo huu kwa maisha yao yote kama vile Kigoma, Rukwa na Tabora, mikoa mingine yote tuliwaomba kidogokidogo. Kwa hiyo, dhana ilikuwa ni kuwatawanya nchi nzima.

Sasa zoezi halijaanza kumekuwa na vikwazo vya hapa na pale lakini matumaini yetu ilikuwa ni kwamba jambo hili lingepokelewa vizuri na wenzetu huko mikoani kwa sababu si wengi wanaokwenda katika kila eneo. Lakini nimepata kidogo fikra kutoka kwa baadhi ya Wabunge kwamba pengine jambo hili lingetazamwa tena upya basi na mimi nilimnong’oneza Rais kwamba kuna mawazo haya pengine tuliangalie ingawa kwa kweli kwa hatua niliyofikia sina hakika kama tunaweza tukarudi nyuma tunaweza tukatazama namna ya kulifanya lakini jamii ya Kimataifa nadhani wanatusubiri kwa hamu kuona kwamba tutalifanyaje. Kwa hiyo, kwa ufupi naweza kusema hivyo tu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Michael Lekule Laizer.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kuuliza swali kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ulipokuwa Naibu Waziri TAMISEMI na Frederick Sumaye alikuwa Waziri Mkuu Serikali ilileta hoja Bungeni kwamba kila Halmashauri itateua Madiwani watatu kwa kila Halmashauri. Jambo ambalo limeleta mvutano mkubwa sana Bungeni mpaka Bunge likakubali, lakini ikaja hoja ni namna gani wateuliwe. Wabunge wakapendekeza ni kila Halmashauri iteue majina, lakini Waziri mwenye dhamana apendekeze majina katika hayo majina yaliyotoka kila Halmashauri.

Lakini baada ya Bunge kukubali hilo jambo halijafanyiwa kazi mpaka sasa. Je, ni nini kilichositisha utaratibu huo mpaka leo na nilidhani kama Serikali ingeshindwa ingeleta utaratibu kwamba imeshindikana kwa ajili ya jambo hili. Kwa hiyo, sasa ni nini kilichositisha jambo hilo lisifanyike?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, anachosema Mzee Lekule ni kweli kabisa na kama ni kutumia utaratibu huo ingekuwa tuanze kutumia katika uchaguzi si huu tuliomaliza juzi ila uchaguzi ule wa mara ya mwisho. Lakini wakati ule ilishindikana kwa sababu taratibu zilikuwa bado hazijakamilika kwa maana ya kanuni. Lakini baada ya pale kanuni zile zimekamilika kwa hiyo kama ni kujaribu kutumia ile sheria itakuwa ni safari hii ndiyo tunatarajia tujaribu kui-*apply* maadam sasa zoezi la kupata madiwani kwa maana ya Viti Maalum pamoja na maeneo mengine imeshakamilika. Hivi sasa ndiyo tunalitazama ili tuweze kutoa maelekezo kwa halmashauri tuone zoezi litakavyokwenda. Kwa hiyo, litakuwa linafanyiwa majaribio kwa mara ya kwanza safari hii.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi nimuulize Waziri Mkuu maswali. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa muda mrefu sasa wafanyakazi hapa nchini hasa wanaotoka kwenye sekta binafsi hasa maeneo ya viwandani na migodini wamekuwa wakilalamika juu ya ukiukwaji ya sheria za kazi zinazofanywa na waajiri. Je, ni lini sasa Serikali ita-*act seriously* ili kutatua matatizo hayo ya wafanyakazi? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, siwezi kulijibu vizuri sana swali hili la Mheshimiwa Regia Mtema kwa sababu limekuwa *specific* kwamba ni lini sasa tutatua tatizo hili. Kwa hiyo naomba niseme tu kwamba matatizo yanayohusiana na mahusiano ndani ya maeneo mbalimbali ya kazi yako mengi, sasa maeneo ya kazi yanaweza kuwa ni katika ofisi zetu, kwenye viwanda vyetu, inaweza ikawa vilevile migodini.

Kwa hiyo ninachoweza kuahidi tu mama ni kwamba tutaendelea kujitahidi kwa kadri tutakavyoweza kama ambavyo tumekuwa tukijaribu kuchukua hatua mbalimbali kujaribu kutatua migogoro ya maeneo ya kazi, ndiyo maana tunajaribu sana kuwatia moyo waajiri kuona kwamba suala la kuwa na vyama vya wafanyakazi katika maeneo ya kazi isiwe hisani, ni kwa ajili ya kuwasaidia na wao wenyewe kuleta mahusiano mazuri. Inakuwa ni chombo ambacho kinawawezesha kukutana, kubadilishana mawazo na kuweza kupanga mipango kwa urahisi zaidi. Kwa hiyo ni jambo ambalo tutaendelea nalo kwa kadri tutakavyoweza chini ya Wizara zinazohusika, Wizara ya Kazi ni mojawapo, lakini Nishati na Madini nao wanahusika kwa kiasi kikubwa.

Lakini nadhani tatizo la upande wa madini linakwenda mbali zaidi ya mahusiano tu ya kikazi kwa sababu pale kuna masuala mengine ambayo si lazima yawe ya kikazi yanahusisha vilevile jamii zinazozunguka migodi hiyo kwa hiyo nalo hilo ni tatizo lingine lakini linahusiana moja kwa moja na migodini. Kwa hiyo yote haya ni matatizo, ni changamoto ambazo tunazo na tutaendelea kuziangalia muda unavyokwenda.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Regia huachii wenzio nafasi, haya uulize swali fupi.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza. Wanapaswa na wao kuwahi maana niliamka saa kumi na moja.

**SPIKA:** Usinimalize muda bwana, endelea msianze kunijibu mimi haya.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** *Okay*, Mheshimiwa Waziri Mkuu nashukuru kwa majibu yako nina swali la nyongeza. Kwa kuwa imeshathibitika waajiri wengi wanakiuka sheria za kazi na ofisi yako ina taarifa, na sijawahi kusikia mwajiri yoyote akichukuliwa hatua za kisheria, tatizo liko wapi?

Je, mnawaogopa waajiri au kuna tatizo gani hapo? Naomba kupewa majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Serikali tumuogope mwajiri kwa lipi, maana Serikali ni Serikali tu eeh, hakuna suala la kumuogopa mwajiri hapa ninachosema tu ni kwamba kama Serikali tunajitahidi kutafuta namna nzuri ya kuwafanya wafanyakazi na waajiri waweze kutengeneza mfumo wa mawasiliano ambao tunadhani ni *approach* nzuri zaidi kuliko hata hilo unalolifikiria. Hawa mmoja mmoja ndiyo wale ambao tuna-*deal* nao unapewa onyo chini ya Wizara ya Kazi, wengine wanachukuliwa hatua ila tu sema tu kwa sababu halitangazwi sana. Lakini kikubwa pale ni ule mfumo wa utatu ambao tunajaribu kuufanya, mwajiri upande mmoja, Serikali upande wa pili na wafanyakazi hiyo ndiyo itatusaidia sana kuleta mahusiano mazuri na maelewano katika sehemu zetu za kazi na kupunguza kabisa tatizo la mifarakano kati ya mwajiri na mwajiriwa.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kumuuliza Waziri Mkuu, nataka nikurejesha katika Katiba, kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ibara ya 133 inaelekeza kuundwa kwa mfuko au mfuko wa Hazina wa pamoja wa Serikali ya Muungano.

Je, mpaka leo ni kitu gani ambacho kinasababisha au kinafanya mfuko huu uwe bado haujaundwa?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nilidhani ungenilinda lakini basi ngoja nijaribu. Kwa sababu jambo hili limejitokeza kwenye mjadala wa bajeti ya Waziri wa Fedha, kwa hiyo mimi napenda niamini kwamba katika maelezo yake atajaribu kulielezea kidogo hivi, lakini ninachoweza kusema ni kwamba ni kweli kabisa kwamba jambo hili

limechukua kidogo muda mrefu kuliko lilivyotarajiwa, lakini imani yangu ni kwamba tutaumaliza mgogoro huu mapema kadri itakavyowezekana.

Wenzetu wa Zanzibar walikutana wakatoa maamuzi yao juu ya jambo hili wakaleta upande wa Serikali upande wa Bara na sisi tukaliingiza katika utaratibu wa kawaida wa kiserikali kujaribu kulifikisha mwisho. Kwa hiyo baada ya hatua hizi mbili kukamilika basi ule mfuko naamini utaanzishwa. Nataka nikuahidi tu kwamba tutajitahidi tulifanyie sasa haraka nisije nikaulizwa tena juu ya jambo hili nadhani tutajitahidi mwaka huu tulimalize.

**MHE. SALUM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi niulize swali kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu Serikali katika kudhibiti matumizi.

**SPIKA:** Sauti haisikiki vizuri labda umesogea mno.

**MHE. SALUM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Waziri Mkuu Serikali katika kudhibiti matumizi imeangalia uwezekano wa kuangalia kodi za wafanyakazi mbalimbali lakini vilevile kusitisha ununuzi wa magari na uagizaji wa *furniture* kutoka nje. Lakini toka Rais Kikwete alipoteua Baraza jipya la Mawaziri, baadhi ya Mawaziri wanaendelea kulala katika mahoteli yenye gharama kubwa wakati Serikali imejenga nyumba kwa ajili yao.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu huoni kwamba jambo hili linakwenda kinyume na azima halisi ya mpango wa maendeleo ya miaka mitano uliozinduliwa na Rais Kikwete tarehe 7 mwezi huu ya matumizi mazuri ya rasilimali chache tulizonazo kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi naomba tu Mheshimiwa Khamis awe mkweli, nitajie Mawaziri walio mahotelini mpaka leo, ili tujue namna ya kulishughulikia.

**SPIKA**: Mheshimiwa Salum mpira kwako.

**MHE. SALUM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Ninayo taarifa ya Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**SPIKA:** Hayaa!

**WAZIRI MKUU:** Haya basi nimesikia. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, asante, Mheshimiwa Waziri Mkuu Taarifa ya Haki za Binadamu ya Tanzania kwa mwaka 2010 iliyotolewa na kituo cha haki za binadamu na sheria mwezi Mei mwaka huu inaonyesha kwamba katika mwaka 2010 peke yake jeshi la polisi limehusika katika mauaji ya raia 52 na ripoti hiyo inaungwa mkono na ripoti ya haki za binadamu kwa Tanzania ya  Wizara ya Mambo ya

Nchi za Nje ya Marekani, ambayo nayo inasema kwamba jeshi la polisi la Tanzania limekuwa likishiriki katika mauaji ya raia, *judicial execution*.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tangu Januari 2008 mpaka wiki iliyopita jeshi la polisi katika kanda maalum ya polisi ya Tarime limeua wana kijiji 26 wa eneo la Nyamongo ulioko mgodi wa dhahabu wa North Mara.

Je, ni sera ya Serikali ya nchi hii kuruhusu jeshi la polisi kuua wananchi bila kuchukua hatua? *(Makofi)*

**SPIKA**: Mheshimiwa Tundu Lissu swali hili liko mahakamani, kwa hiyo namwita Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi hii kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali, kwamba katika kikao cha nane, mkutano wa 17 Bunge la Tisa, siku ya tarehe 5 Novemba, 2009 Waziri Mkuu wakati akijibu swali la papo kwa papo aliahidi kumuagiza Waziri wa Mambo ya Ndani kuchukua hatua dhidi ya taarifa za kuuliwa wananchi kumi wanaoishi kwenye mgodi wa Tarime uliopo Nyamongo, mgodi ambao unamilikiwa na Barick African Gold na kwa kuwa hadi sasa hatua hazijachukuliwa na kumekuwepo na mauaji yanaendelea na vitendo vya ubakaji vinavyofanywa na jeshi la polisi na walinzi wa mgodi ule.

Je, Waziri Mkuu sasa ataliambia nini taifa kuhusu mauaji yanayoendelea kule na vitendo hivi vya ubakaji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge katika lawama tunayopewa sisi Bunge ni kwamba tunaingilia kazi za mihimili mingine, kwa hiyo naomba nalo hili pia litoke kwamba ni swali ambalo liko mahakamani.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu ubakaji suala liko mahakamani? (Makofi)

**SPIKA:** Naomba ukae nikisimama wewe unakaa, lipo pamoja hapo. Kwa hiyo tunaendelea na Mheshimiwa Mwigulu Mchemba Madelu.

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Spika, asante. Wanafunzi wa kidato cha nne wa shule za sekondari za kata kama ilivyo kwa wanafunzi wengine wanajiandaa na mtihani wa kidato cha nne, huku kukiwa bado kuna upungufu wa walimu uliosababisha matokeo mabovu kwa wanafunzi waliopita. Kwa kuwa, wanafunzi wa sekondari wa shule hizi za kata katika shule za vijijini ni wachache na walimu ni wachache.

Je, Serikali haifikirii kuwa ni vyema kuwakusanya wale wanafunzi wachache katika shule moja ya tarafa na kuwakusanya wale walimu wachache katika *joint facility* hiyo ili hao wanafunzi waweze kupata walimu wa kila somo wanapojiandaa kuelekea kwenye huo mtihani*? (Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ushauri wa Mheshimiwa Mwigulu ni mzuri ungeweza pengine kutusaidia kupunguza tatizo hili la walimu, lakini nao vilevile lazima uangaliwe kwa upande mwingine kwa sababu si mwepesi kiasi hicho. Maana yake ni nini?

Maana yake ni kwamba ni lazima basi tuchukue vilevile hatua ya kuhakikisha tunazo *hostels* za kutosha katika eneo hilo na nyumba za kutosha kuwaweka walimu katika shule hiyo. Sasa kwa sababu ni jambo limejitokeza katika mfumo wa swali kwa kweli litahitaji pengine Wizara ya Elimu na Mafunzo walitazame walifanyie kazi tuone namna inavyoweza kufanyika lakini haiwezi kuwa kwa haraka kujibu tatizo lililopo sasa pengine tunaweza tunaweza tukalitazama kwa maana ya huko tunakwenda. Ni wazo nzuri lakini linabidi vilevile litazamwe kwa namna nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini upande wa pili ni vizuri vile vile Mheshimiwa Mwigulu ukajua vilevile kwamba sina hakika kwamba kweli unaweza ukawakusanya wanafunzi ndani ya tarafa moja katika eneo moja, kwa sababu uhaba unaosema utaukuta katika baadhi ya maeneo, lakini sehemu nyingi wanafunzi ni wengi wa kutosha kuweza kuwa na kituo chao katika shule yao waliko. *(Makofi)*

Kwa hiyo, changamoto kubwa inayobaki kwa serikali ni mpango uliopo wa kutoa mafunzo kwa walimu wengi zaidi ili tuweze pole pole kuweza kujaza nafasi hizi kadri muda unavyokwenda, na mimi nina hakika Waziri wa Elimu ataelekeza jitahada ambazo tumefanya na tunazoendelea kufanya kukabiliana na changamoto ya uhaba wa walimu shuleni, sekondari na hata shule za msingi.

## MASWALI YA KAWAIDA

**SPIKA:** Kwanza kabisa naomba nikushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna ulivyojibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge, leo maswali yote yalikuwa maswali ya msingi. Nimekataa maswali mawili kwa sababu wenzetu hawa wanatuhumiwa na tarehe 17 wengine wanatakiwa kufika kunako husika. Sasa tunayo lawama kabisa tumeletewa na muhimili mwingine kwamba tunaingilia sehemu ya shughuli zao. Kwa hiyo, hii ndiyo sababu nimekataa tunaendelea na ofisi ya Waziri Mkuu

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Kuhusu Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Baada ya maswali. *(Makofi)*

Na. 59

### Michango inayotozwa kwa ajili ya Mifugo

**MHE. TUNDU A. LISSU** aliuliza:-

Kwa muda mrefu kumekuwa na michango mingi ya lazima inayotozwa kwa ajili ya mifugo ya aina mbalimbali kwenye maeneo yote ya Halmashauri za Wilaya, lakini haitoi huduma zozote kwa ajili ya mifugo ikiwemo majosho kwa ajili ya kujikinga na maradhi mbalimbali ya milipuko na ya kuambukiza:-

(a) Je, ni fedha kiasi gani kimekusanywa kama michango ya lazima ya mifugo kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Singida. Jimbo la Singida Mashariki katika kipindi cha 2005/2006 hadi 2010/2011 na fedha hizo zimetumikaje?

(b) Je, Serikali haioni kuwatoza wananchi michango ya mifugo bila kuihudumia mifugo hiyo ni kuwanyonya wananchi?

(c) Ni lini Serikali itaanzisha miradi ya kufufua majosho katika jimbo la Singida Mashariki ili wananchi waweze kunufaika na fedha wanazochangishwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tundu A. Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mpango shirikishi wa maendeleo inawashirikisha wananchi katika kuibua, kupanga na kutekeleza miradi kupitia mpango wa fursa na vikwazo wa maendeleo. Majosho ni miongoni mwa miradi inayoibuliwa na wananchi. Wananchi huchangia asilimia 20 ya gharama za mradi ambapo kiasi cha kuchangia huamuliwa na mkutano mkuu wa kijiji kupitia Kamati za Maendeleo.

Kwa upande wa majosho wananchi huchangia shilingi 100 kwa ng'ombe na shilingi 50 kwa mifugo mingine wakati wa kuogesha. Fedha hizi ni kwa ajili ya upatikanaji wa madawa ya mifugo. Malalamiko mengi ya wananchi juu ya michango yanatokana na ushiriki wao mdogo katika kuamua kiasi, namna na wakati muafaka wa kutoa michango hiyo hii ikiwa ni pamoja na kutopatikana kwa taarifa za mapato na matumizi ya fedha hizo katika ngazi ya vijiji na vitogoji.

Vilevile uko utaratibu wa kuhudumia mifugo kupitia mfuko wa maendeleo wa mifugo ya *LDF*i na mpango wa maendeleo ya kilimo wa wilaya na jumla ya shilingi bilioni 2.6 za *DADPS* na milioni 39.4 za *LDF* zimetumika katika kipindi cha mwaka 2005/2006 hadi 2010/2011.

(b) Mheshimiwa Spika, kimsingi maamuzi kuhusu michango ya kiwango cha kuchangia huamriwa kupitia mkutano mkuu wa kijiji na fedha hizo hutumika katika miradi iliyoibuliwa na wananchi wenyewe.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005/2006 hadi 2010/2011, Halmashauri imekarabati majosho 15 kati ya 37 na kujenga majosho manane.

Katika jimbo la Singida Mashariki, Majosho yaliyojengwa ni Tupendane, Mkiwa, Matongo na Iguka na majosho yaliyofanyiwa ukarabati ni Dung'unyi, Makhotea, Siunyu na Mung'aa. Aidha, majosho yaliyojengwa na kufanyiwa ukarabati huendeshwa na Kamati za mifugo na kupatiwa dawa lita kumi (10) kwa kuanzia kwa ajili ya uendeshaji wa majosho hayo.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kumwuliza Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri mimi niliomba takwimu za fedha ambazo wananchi wamechangishwa kwa ajili ya mifugo waliyonayo na sijapata takwimu hata moja.

Sasa kwa vile hakuna takwimu wananchi wamekuwa wanachangishwa shilingi 2000 kwa kichwa cha ng'ombe, shilingi 1000 kwa mbuzi, kondoo, punda, mbwa na wanachangishwa kwa nguvu wasipokuwa na fedha wanapigwa, wamevunjwa viungo wengine.

Sasa swali ni je, Serikali ina mpango gani kuwachukulia hatua za kiutendaji za kuwaondoa kazini Mkurugenzi wa Halmashauri ya Singida na Mkuu wa Wilaya ya Singida kwa kuchangisha wananchi bila kuwepo utaratibu wowote wa kisheria? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, labda niliweke jambo hili wazi ili tuweze kuelewana hapa. Takwimu anazozizungumza ni kweli anazungumza hizi za shilingi 100/= kwa ajili ya ng'ombe na shilingi 50/= kwa ajili ya mbuzi.

Ni kweli kabisa kwamba ukienda katika vijiji vyetu takwimu hizi hazipatikani, ni kweli anavyosema na sio uongo. Nilipojaribu kuwafuata wote wale wanaohusika katika jambo hili sikuweza kupata takwimu hizi na ndiyo maana tumejibu hapa tukasema kwamba takwimu hizi hazikupatikana.

Nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji, tumezungumza na Afisa Mifugo na Bwana Paschal Mabiti, Mkuu wa Wilaya tumezungumza naye asubuhi ya leo na wote tumekubaliana kwamba ni kweli kuna tatizo hapa. Hatua iliyochukuliwa na Serikali au Serikali imetoa maelekezo kwamba kuanzia sasa taarifa hizi zitoke kutoka kwenye kijiji kutoka kwenye kitongoji ziende moja kwa moja na tarehe 25 zifike kwa Mkuu wa Wilaya na zifike kwa Mkuu wa Mkoa kuonyesha nini kilichotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameona kwamba kuna wasiwasi katika jambo hilo. Sisi hapa tumezungumza na Mheshimiwa Mkuchika tumekubaliana kwamba tutapeleka *delegation* kutoka TAMISEMI itakwenda Singida kwenda kuangalia hayo yote anayozungumza Mheshimiwa Mbunge. Kama ikithibitika kwamba ni kweli sisi tutachukua hatua. Kwa hiyo, hayo ndiyo maamuzi ya Serikali. (*Makofi)*

**MHE. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa michango hii ni sawasawa na michango wanayotozwa wananchi wa jimbo la Biharamulo Magharibi pamoja na hayo hawana huduma wanayoipata. Leo hii wameshaanza kuchangishwa fedha kwa ajili ya Sherehe ya Uhuru na Jamhuri. Je, Serikali inasemaje kuhusu hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hii michango inayozungumzwa hapa ni ya hiari.

Lakini nataka niseme utaratibu ambao unaotumika hakuna mchango wowote unaweza ukatolewa katika Halmashauri au katika Wilaya bila ya kupata kibali cha Mkuu wa Wilaya. Mkuu wa Wilaya ni msimamizi wa shughuli zote za Serikali katika eneo linalohusika. Tunafanya hivyo ili ku-*control* ili kuweko na nidhamu watu wasije wakaibuka tu kila mtu ananyanyuka anataka kufanya mchango.

Mheshimiwa Spika, kama nimemwelewa vizuri na hilo tutalifuatilia anachozungumza hapa anazungumzia mchango kwa ajili ya sherehe jambo ambalo kama nilivyosema hapa ni suala la hiari, mtu anaombwa tunakuomba utupatie msaada anatoa msaada ule. Sasa nataka kujua *modality* yake nitafuatilia ili tujue kwamba ni nini kinaendelea. Lakini *at the bottom line* huwezi ukachangisha mchango wowote bila kupata kibali cha Serikali.

Na. 60

**Mikopo kwa Wajasiriamali Wanawake**

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA** aliuliza:-

Suala la kuwajali wajasiriamali limeelekezwa vizuri kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005/2010. Ni kutokana na ukweli huo Serikali inawajali wajasiriamali wanawake wa mkoa wa Rukwa.

Je, ni vikundi vingapi vya wajasiriamali wanawake wa Mkoa wa Rukwa walipatiwa mikopo katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010 na ni kiasi gani cha fedha kilitolewa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mbunge kwa kuwa leo ni tarehe 16 Juni, 2011 Tanzania inaungana na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika. Kwa ruhusa yako ninaomba kupitia Bunge lako Tukufu kuwatakia kheri, baraka, afya njema na maisha marefu, Watoto wote wa Afrika na watoto wote wa Tanzania. Kauli mbiu ya mwaka huu "Tuungane kwa Pamoja kuchukua hatua za haraka kushughulikia tatizo la watoto wanaoishi mitaani."

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Rosweeter Faustine Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubalilna na Mheshimiwa Rosweeter Faustine Kasikila, kuwa suala la kuwajali wajasiriamali limeainishwa vizuri katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 - 2010. Kutokana na ukweli huo Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikitoa mafunzo na mikopo kwa wanawake wajasiriamali.

Mheshimiwa Spika, kwa mkoa wa Rukwa, Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*Women Development Fund* (WDF), imekuwa ikitoa fedha za kuwakopesha wanawake wajasiriamali katika Halmashauri mbalimbali za mkoa wa Rukwa. Kwa kipindi cha mwaka 2005 - 2010 jumla ya vikundi 341 vimepatiwa mikopo yenye thamani ya shilingi 377,640,000. Sambamba na kupatiwa mikopo, mafunzo ya ujasiriamali yametolewa kwa vikundi vya wanawake 797.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Katika kipindi hicho hicho cha mwaka 2005 – 2010 kuna vikundi 102 katika Halmashauri ya Nkansi havikupata mikopo baada ya kuomba. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa mikopo kwa vikundi hivyo 102?

Je, Serikali ina mkakati gani endelevu wa kutoa mikopo kwa wanawake wajasiriamali wa Mkoa wa Rukwa. Lakini na wengine pia wanapokuwa wameelimishwa, wakahamasishwa, wakahamasika, wakaunda vikundi vya maendeleo kwa ajili yao wenyewe na watoto wao, lakini wanakuwa hawapewi mikopo hiyo wanavunjwa mioyo. Je, Serikali ina mkakati gani endelevu wa kuendelea kuwapa mikopo wanawake hawa wanapokuwa wameomba?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ni mfuko ambao wa marejesho. Wizara inatoa kiasi cha fedha na Halmashauri inatakiwa kuchangia asilimia fulani ya mapato yake ambayo ni asilimia 10 au 5 kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na asilimia 5 kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo katika Halmashauri ya Nkansi ilipatiwa fedha za mfuko kutoka Wizarani kwa mara ya mwisho mwaka 2003/2004 na hawajarejesha. Usiporejesha Wizara haiwezi kukupatia fedha. Naomba nimwombe Mheshimiwa Mbunge atusaidie kuhakikisha kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Nkansi inafanya marejesho na Halmashauri pia inatenga asilimia 10 ya mapato ya ndani ili kuuboresha Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba Serikali ina mkakati gani ya kuwasaidia wajasiriamali wanawake. Kuna mradi wa kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo *SELF*, lakini pia Serikali ina mpango wa uwezeshaji wa wanawake kiuchumi na kuongeza ajira. Namshauri Mheshimiwa Mbunge asikilize Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mama Nagu, Waziri wa Nchi, Uwezeshaji na Uwekezaji halafu atazame ni kwa kiasi gani masuala ya kuwawezesha wanawake yametiliwa mkazo. Lakini sisi kama Wizara tutaendelea kuhamasisha Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, *SACCOS*, *SELF* na Benki ya Maendeleo ya Wanawake.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa leo Tanzania inaadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika na Naibu Waziri amewatakia kheri watoto hao wa Tanzania na kumekuwa na tatizo la watoto wa mitaani hasa katika miji mikuu hapa nchini Tanzania. Serikali inajua ni watoto kiasi gani hapa Tanzania wako mitaani kwa kukosa matunzo maalum na ina mipango gani ya kuwasaidia watoto wa mitaani?

**SPIKA:** Christina kwa kweli swali kabisa halipo. Lakini kwa sababu ni Sikukuu yao basi Waziri ujibu, lakini lilikuwa nje kabisa. Jibu Mheshimiwa Waziri kwa sababu mwenyewe ndiyo ulianza kuwapongeza watoto hao.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, tumefanya tathmini mwaka jana wa kuangalia ni kiasi gani cha tatizo la watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Siwezi kumpa takwimu sasa hivi Mheshimiwa Mbunge, lakini nitoe tu kauli kwamba tatizo hili ni kubwa na linakua kwa kiasi kikubwa. Lakini sisi kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ujumbe wetu ni kwamba suala la watoto wa mitaani ni suala la familia, suala la wazazi, suala la walezi, suala la sisi Serikali za Mitaa na Halmashauri husika za miji.

Kwa hiyo, tumejipanga kushirikiana na Halmashauri za Mitaa na Miji kuhakikisha kwamba tunalitatua tatizo hili haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Na. 61

**Kuanzisha Kitengo Maalum cha Kushughulikia**
**Ajira Kwa Vijana**

**MHE. ESTHER A. BULAYA** aliuliza:-

Moja kati ya changamoto zinazolikabili Taifa letu ni ukosefu mkubwa wa ajira kwa vijana:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba, kuna umuhimu wa kutenga au kuanzisha Kitengo Maalum kitakachoshughulikia matatizo ya ajira kwa vijana pekee ili kumaliza tatizo hilo?

(b) Je, ni nini matarajio ya Serikali katika tatizo la ajira kwa vijana katika kipindi cha miaka mitano ijayo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Amos Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Kwa sasa Serikali haioni sababu za kutenga au kuanzisha Kitengo Maalum kitakachoshughulikia matatizo ya ajira kwa vijana pekee, kwani muundo uliopo unakidhi mahitaji ya kushughulikia suala la ukosefu wa ajira kwa vijana.

(b) Wizara yangu inayo Idara kamili ya ajira kwa ajili ya kushughulikia masuala ya ajira kwa ujumla kipaumbele kikiwa ni vijana. Zaidi ya hapo, katika Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuna Idara ya Maendeleo ya Vijana ambayo inayoshughulikia masuala ya kiujumla yahusuyo vijana. Aidha, naomba pia ieleweke kuwa ukosefu wa ajira hasa kwa vijana hausababishwi na kutokuwa na Kitengo Maalum, bali unasababishwa na mambo mengi hasa (i) Kasi ndogo ya ukuaji wa nafasi za ajira katika uchumi (*Demand side)* na (ii) Uwezo mdogo wa kujiajiri au kuajirika miongoni mwa nguvu kazi inayoingia katika soko la ajira (*Supply Side).*

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, Serikali inatarajia kutekeleza MKUKUTA II kwa lengo la kupunguza ukosefu wa ajira kutoka asilimia 11.7 mwaka 2006 hadi kufikia kiwango cha asilimia 5 mwaka 2015 kupitia utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Kukuza Ajira inayobainisha upatikanaji wa ajira zaidi ya milioni tano.

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mepesi ya Mheshimiwa Waziri katika maswali magumu ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, hivi karibuni, ni juzi tu tumepitisha mpango wa miaka 5 na imeoanisha mipango mbalimbali kwa ajili ya kutatua tatizo la ajira kwa vijana na ukizingatia ndio wengi hawana ajira na wanazagaa mitaani.

Lakini katika majibu yake ameelezea mpango wa MKUKUTA II wa kupunguza ajira. Lakini mpango namba moja kwa miaka 5 iliyopita uliweza kupunguza tatizo hili kwa asilimia 100 tu. Je, katika Bajeti ya mwaka huu kupitia miradi mbalimbali Serikali ina mpango wa kupunguza tatizo hili kwa asilimia ngapi?

Swali la pili, kwa mujibu wa taarifa mbalimbali za uchumi sekta binafsi imekuwa ikitoa mchango mdogo sana katika kutatua tatizo la ajira na hasa baada ya kupunguza tatizo la ajira imekuwa ikishindwa kutoa ajira kwa vijana.

Je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa wa kukutana na sekta husika kuingia makubaliano maalum wanapoanza mchakato wa ajira wahakikishe kuna idadi maalum ya vijana watakaoajiriwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri nafahamu utajibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** MheshimiwaSpika, kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kuwatetea vijana hasa ajira zao katika Bunge hili na kwa kweli niseme anawakilisha vizuri jimbo lake la Vijana.

Lakini vile vile nisikubaliane naye kwamba nimetoa majibu mepesi, majibu ninayotoa hapa ni mazito sana ni *commitment* kubwa sana ya Serikali ya kupunguza tatizo la ajira kutoka asilimia 11 kama ilivyokuwa mwaka 2006 kuelekea asilimia 5 ni *commitment* kubwa ambayo kwa kweli tuna jukumu kubwa sana kama sekta ya Umma na sekta binafsi kuifikisha. Kwa hiyo, majibu haya si mepesi hata kidogo.

Lakini nimweleze kwamba tunapoangalia katika mpango wa miaka 5 katika kipindi hiki, hakuna kipindi ambacho sekta au eneo la kuongeza ajira limewekewa kipaumbele kama kipindi hiki. Wote mmeona katika vile vipaumbele 5 kuongeza ajira au kukuza ajira ni moja ya mipango mizito ya Serikali kwa miaka 5.

Kwa hiyo, kama tuliipunguza kwa asilimia moja katika kipindi kilichopita dhamira hii ambayo tumeiweka sasa ya kupunguza kwa kiasi kikubwa naamini itafikiwa kama wote sekta ya Umma na sekta binafsi itaweka nguvu zake.

Mheshimmiwa Spika, la pili kuhusu sekta binafsi nataka niwatetee wenzetu wa sekta binafsi kwamba kwa kweli katika kipindi kirefu wamekuwa ni nguvu kubwa sana

katika kuongeza ajira kwenye uchumi wetu na hasa tunapoangalia kwamba sasa sekta ya kilimo imekua na asilimia ya watu walioko kwenye ajira kwenye sekta ya kilimo inazidi kupungua toka asilimia 85 miaka kama 15 iliyopita sasa hivi ni kwenye asilimia 70. Asilimia 30 kwa kweli iliyobaki kwa kiwango kikubwa ni sekta binafsi hasa kwenye uwekezaji, viwanda, biashara, mawasiliano, ujenzi, sekta binafsi inatoa ajira kubwa sana.

Lakini bado tunalo jukumu kama Serikali kuwasiliana na kukaa na sekta binafsi, kuendelea kuangalia ni namna gani tusaidiane ili sekta hii iendelee kutoa ajira kwa vijana. Kwa hiyo, hii nataka nimwahidi kwamba tutakaa na sekta binafsi, tutaendelea kukaa nao, na tumekuwa tukifanya hivyo ili sekta hii iendelee kukuza ajira za vijana.

Na. 62

**Tiba ya Ugonjwa wa Malaria Nchini**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

Maradhi ya Malaria bado ni tatizo kubwa katika nchi yetu na mpaka sasa wananchi hawajui tiba halisi ya malaria:-

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu dawa inayofaa kutibu malaria hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli ugonjwa wa malaria bado ni tatizo kubwa nchini. Hata hivyo tafiti zinaonyesha uelekeo wa kupungua kwa maradhi na vifo vinavyotokana na maambukizi ya malaria. Utafiti mkubwa wa kisayansi wenye uwakilishi wa kitaifa unaofanyika kila baada ya miaka miwili, utafanyika tena kuanzia Oktoba 2011 hadi Februari 2012 ili kupata matokeo halisi ya hali ya ugonjwa wa malaria hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na usugu wa dawa iliyokuwa inatumika yaani SP Serikali ilitoa mwongozo wa kutumia dawa mseto *(ACTs)* kutibu malaria isiyokuwa kali. Katika mabadiliko ya wakati huo, dawa ya Kwinini iliendelea kutumika kutibu malaria kali.

Kwa kutambua umuhimu wa dawa mseto na mchango wa sekta binafsi katika kuchangia utoaji wa huduma hapa nchini, mwaka huu 2011, Serikali imeanzisha rasmi mpango wa upatikanaji wa dawa mseto kwa bei punguzo kwenye sekta binafsi.

Mpango huu unalenga kuwezesha dawa ya mseto ya kutibu malaria ipatikane kwa bei isiyozidi shilingi za Kitanzania 1,000/=. Mpango huu umeanza kutekelezwa.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na napenda nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri maswali madogo mawili kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa dawa hii imeambiwa huwa inapunguzwa bei, lakini sijui kama Wizara ya Afya inayo habari kuwa watumiaji wa dawa hizi hasa wale watoto wadogo wanaathiriwa sana na dawa hizi na wengine hata kufikia hatua ya kupoteza maisha yaani kufa?

La pili, kwa kuwa nchi nyingi duniani wanaokabiliana na malaria hawaendi kwenye vyandarua na dawa za kuweka kwenye vyandarua wanakwenda kukabiliana na mbu katika mazalio yao na mpango huu ulikuwepo katika nchi hii hii miaka ya nyuma.

Hivi ni jambo gani linalopelekea Serikali kuwa na kigugumizi katika kukabiliana na mbu na badala yake wanaleta vyandarua na dawa za vyandarua? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri. Najua wewe ni Waziri wa Afya na Daktari. Kwa hiyo, naomba ujibu kwa kifupi, usitupe semina saa hizi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, binadamu wanapotumia dawa yoyote kwa ajili ya kutibu maradhi, siyo kila binadamu anaweza akapatana na dawa hizo, hata SP zilikuwa zinatoa *reaction*, *quinine* zinatoa *reaction*. Sasa kwa wale ambao wanapata *reaction* kwa ajili ya hizi dawa, hasa watoto ambao wana malaria kali, tunatumia dawa ya *quinine*.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kuna *reaction* na hakuna dawa yoyote ambayo inatumika isiyo na *reaction* kwa binadamu. Kwa hiyo, hata dawa hii itakuwa na *reaction* na ndiyo sababu tumekuwa na *line* ya pili ya dawa ya *quinine*, kwa ajili ya kutibu wale ambao hawapatani na dawa hii.

Ningependa kumpongeza Mheshimiwa Suleiman, amekuwa na *knowledge* nzuri sana ya kuzia malaria, anajua kwamba kuna malaria, kuna kutumia viatilifu pamoja na kuangamiza mazalia ya mbu. Unapopambana na maradhi yoyote, kunakuwa na Mpango wa Muda Mfupi na Mpango wa Muda Mrefu. Kama Wizara, Mpango wa Muda Mfupi ni kutoa vyandarua na kuhakikisha kwamba, familia zote nchini zinapata vyandarua. Tulianza na hati punguzo, tukawapa watoto na sasa kila kaya itakuwa inapata vyandarua kufuatana na mahitaji yake na tumejipanga kwa hilo.

Hatua ya pili ni kupambana na chanzo cha malaria ambacho ni mbu, tumeshaanza kunyunyizia dawa ambayo inadumu kwa muda mrefu katika mikoa mitatu ambayo imekuwa na vifo vingi vya malaria; Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Mara na Mkoa wa Mwanza. Tukishamaliza kwenye mikoa hii mitatu, tutaendelea kwa awamu mpaka tumalize Mikoa yote ya Tanzania.

Hatua ya tatu, katika Bonde la Jangwani na katika Jiji la Dar es Salaam, kwa kushirikiana na Wacuba, Serikali imewalipa Wacuba wanaanza kuleta viua wadudu ambavyo kwa sasa hivi tumeshajitayarisha na wakati wowote wataanza kuwanyunyuzia.

Jambo lingine zuri ni kwamba, hatufanyi tu kama Mradi Msonge, *Vertical Programme*, tumekubaliana na Wacuba wanajenga kiwanda Kibaha ili hili zoezi liweze kuwa endelevu, tuweze kupambana na malaria katika nchi hii kwa dhati kabisa.

Na. 63

**Uzazi wa Mpango na Kuongeza Bajeti ya Wizara**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (K.n.y. MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA)** aliuliza:-

Uzazi wa Mpango katika nchi umeshuka kwa asilimia 0.6 na mimba milioni 2.5 katika mwaka 2005 zilikuwa ni zile zisizotarajiwa:-

(a) Ili kukabiliana na hali hii Serikali ina mpango gani licha ya kuongeza bajeti toka shilingi 0.5 bilioni hadi shilingi 14.3 bilioni kupitia *Busket Funding* kwa kuongeza bajeti ya Wizara husika na kutilia msisitizo wa uzazi wa mpango kudhibiti hali ya ongezeko kubwa la watu?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani kutoa Elimu ya Uzazi wa Mpango kwenye shule zetu ili kuwapa Elimu juu ya Uzazi wa Mpango?

(c) Je, ni sababu gani zinazosababisha kuwepo na mimba zisizotarajiwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Mary Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Wizara ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 14.8 kwa ajili ya kununulia dawa za uzazi wa mpango; shilingi 0.5 bilioni zilikiwa ni fedha za kutoka ndani na shilingi 14.3 bilioni zikiwa ni fedha za kutoka kwa Wadau wa Maendeleo kupitia *Busket Fund*. Aidha, mahitaji halisi kwa mwaka 2010/2011 ya dawa za uzazi wa mpango, yalikadiriwa kuwa kiasi cha shilingi 23.4 bilioni. Ili kufikia lengo, Serikali ya Uingereza kupitia Shirika la Maendeleo la *DFID*, ilitoa msaada wa shilingi bilioni 15.3 (Dola za Kimarekani milioni 10.2). Kwa kuongeza matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango ili kufikia asilimia 60 ifikapo mwaka 2015 kutoka asilimia 27 ya mwaka 2010; Wizara ina mkakati wa kuongeza upatikanaji wa huduma za uzazi wa mpango wa njia zote katika vituo vya huduma, kuongeza uwezo kwa watoa huduma za uzazi wa mpango, ikiwa ni pamoja na kuboresha sera na kutilia mkazo katika usimamizi na ufuatiliaji.

(b) Mheshimiwa Spika, ingawa Sera ya Wizara ya Elimu bado haijaruhusu huduma za uzazi wa mpango kutolewa katika Shule za Msingi, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Kitengo cha Afya ya Uzazi na Mtoto, ina Program ya Afya ya Uzazi kwa Vijana, ambayo imeandaa mikakati kadhaa ya kuhakikisha kuwa, Elimu ya Uzazi wa Mpango inawafikia vijana wote wakiwemo walioko mashuleni. Pia Mitaala ya Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo nchini imeboreshwa ili kujumuisha masuala ya Elimu ya Afya ya Uzazi ikiwemo Magonjwa ya Ngono. Elimu hii ya Afya ya Uzazi hutolewa kuanzia darasa la tano.

(c) Sababu zinazosababisha kuwepo na mimba zisizotarajiwa ni pamoja na kutotumika kabisa au kwa usahihi njia za uzazi wa mpango, nazo ni:-

- Kubakwa au kufanya tendo la kujamiana bila ya kinga wakati wa kipindi cha rutuba ya uzazi;

- Kukosa elimu sahihi kuhusu uzazi wa mpango, kuzuiwa na mwenza/wenza au imani potofu za kimila;

- Kuwepo kwa dhana na vumi potofu zisizohakikiwa kitaalam kuhusu uzazi wa mpango katika jamii husika;

- Mfumo dume; mwanamke anakua hana uhuru wa kutumia njia za uzazi wa mpango kwa sababu mume wake hataki na akitumia atafukuzwa; na

- Kutopatikana kwa dawa za uzazi wa mpango zinapohitajika.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii, kuwapongeza Machampioni wa Uzazi wa Mpango wakiwemo Mary Mwanjelwa na Jenista Mhagama akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Naibu Waziri amekiri kabisa huduma hii ya uzazi wa mpango katika nchi yetu ya Tanzania mpaka sasa inawafikia wanawake kwa asilimia 27 tu; na kutokana na tatizo hilo la kimsingi, vifo vya wananwake wakati wa kujifungua vimekuwa vikipungua kwa kiasi kidogo sana, kutoka wanawake 570 kati ya wanawake 1,000 mpaka wanawake 440 tu; kwa hiyo unaona kabisa kwamba; *trend* ni ndogo sana; na kwa kuwa bajeti ya Wizara kifungu kidogo 2001 kila mwaka kimekuwa kikiongeza fedha, mwaka jana ilikuwa bilioni 20, mwaka huu ni bilioni 22, lakini fedha hii haishughulikii tatizo la msingi la uzazi salama kwa maana ya uzazi wa mpango:-

(a) Je, Waziri na Wizara hii yuko tayari sasa katika kifungu hicho kwenye bilioni 22 kujikita kuongeza huduma ya mpango wa uzazi kwa wanawake wote kwa nchi yetu ya Tanzania?

(b) Kwa kuwa nchi jirani na rafiki zetu kwa kuwaokoa hawa akina mama wanaokufa kwa wingi kama vile gari likipinduka na wanawake 440 wakafa kwa pamoja hilo ni Janga la Kitaifa, wakaamua kutunga sheria inayojikita katika kulinda haki za hawa wanawake wanaokufa; je, Serikali ipo tayari sasa Bunge hili litunge Sheria ya Kuwasaidia Kuwalinda hawa Akina Mama na Watoto Wadogo Wanaokufa wakati huo wa uzazi?

**SPIKA**: Mheshimiwa Naibu Waziri jibu, kwa kweli sitaki majibu marefu maana tayari tupo nje ya wakati.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwenye suala la ongezeko la kifungu cha fedha kwa ajili ya *family planning*, ninaomba kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba, hizo pesa zipo. Tunapozungumzia *Family Planning* tunafanya mambo mengi, hatununui dawa tu; tunatoa elimu na tunatoa mafunzo kwa wahudumu ili waweze kutoa huduma sahihi na tunanunua sasa vitendea kazi pamoja na dawa kwa ajili ya *Family Planning.*

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa tumejipanga kuhakikisha kwamba, tunaongeza utumiaji wa uzazi wa mpango kutoka asilimia 27 mpaka asilimia 60 katika bajeti yetu ya mwaka huu. Kwa hiyo, kutoa tathmini sasa hivi siyo rahisi ila ninaamini kwamba, kwa sababu tumejipanga wahudumu wapo na maeneo ya kazi, *facilities*, zipo basi ninafikiri kwamba hilo lengo litafikiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ni kweli kwingine wametoa sheria ya kuhakikisha kwamba wanawake wanapata *access* kwa ajili ya huduma za uzazi wa mpango. Ninafikiri kwa sababu bado tuna Sera ya Afya na tunaamini kwamba, kutokutumika kwa dawa za uzazi wa mpango na vifo vya akina mama inachangiwa na mambo mengi; kweli kutokutumia uzazi wa mpango inachangia, lakini kuna mambo mengine kama kuchelewa kwenda hospitali au kutokwenda kujifungulia kwenye vituo vyetu. Kwa hiyo, sambamba na kutangaza na kuhimiza uzazi wa mpango, tutahimiza pia akina mama kwenda kujifungulia kwenye hospitali za kisasa badala ya kwenda kujifungulia nyumbani, kwa sababu ni asilimia arobaini tu wanajifungua.

Kwa hiyo, tuhakikishe akina mama wanajifungulia hospitalini na tuhakikishe kwamba, wakishajifungua wanaweka nafasi kati ya mtoto na mtoto ili waweze kuboresha afya zao.

Na. 64

**Fedha Zilizohusishwa na Wizi, Uzembe na Ubadhirifu**

**MHE. MASOUD ABDALAH SALIM** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa akilihutubia Bunge tarehe 18 Novemba 2010 alisema uzembe, wizi, ubadhirifu havitavumiliwa na

atazipa uzito unaostahili Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuchukua hatua zipasazo:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha zilihusishwa na uzembe, wizi na ubadhirifu kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2009 hadi Oktoba, 2010?

(b) Je, wahusika walichukuliwa hatua gani?

**NAIBU WAZIRI YA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mbunge wa Mtambile, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kutoa taarifa kuwa, Ripoti za Ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hutolewa kufuatana na Mwaka wa Fedha wa Serikali. Kwa kuwa kipengele (a) cha swali kinachohusisha sehemu ya ukaguzi wa kipindi tajwa, kinaonesha kwamba, kiasi cha shilingi 512,477,774,322 kilichohojiwa na *CAG* kilionesha kuwepo kwa viashiria vya uzembe, wizi ama ubadhirifu. Kiasi hiki kinahusisha Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, ni vigumu kutoa tamko la moja kwa moja kwamba, upotevu wote wa fedha za Serikali unahusiana (bila kutia shaka) na ama uzembe, wizi au ubadhirifu; matokeo ya ukaguzi yanaonesha kuwepo viashiria vya uzembe, wizi, ubadhirifu ambao huwasilishwa kwenye taasisi husika za Serikali zenye mamlaka kwa hatua na uchunguzi zaidi wa kitaalamu na uthibitisho kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba, baada ya kupokea Taarifa hii ya Ukaguzi ya Mwaka 2009/2010, ambayo sasa inaweza kufanyiwa kazi baada ya kuwasilishwa Bungeni katika Bunge la Aprili, Serikali imeanza kuchukua hatua stahiki zikiwemo kufikisha taarifa kwenye vyombo vya uchunguzi kama vile TAKUKURU na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashataka *(DCI)*, kwa hatua zao ama kwa ajili ya uchunguzi zaidi wa kitalaam.

Taarifa na hatua zitakazochukuliwa, zinaweza kutolewa baada ya taasisi hizi kukamilisha taratibu zao na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria au maamuzi zikiwemo Kamati za Kudumu za Bunge *(Oversight Committees)* zinazoshughulikia kusimamia fedha za umma na Maafisa Masuuli.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa kuanzia mwaka 2006/09, jumla ya Halmashauri 30 zilibainika na ufisadi na watumishi 921 walifikishwa mahakamani; cha ajabu watumishi 14

walishushwa madaraka, mmoja akapewa onyo na mmoja akashushwa mshahara; je, ni lini tabia hii ya Serikali kuwaachia mafisadi kuendelea kutesa kwa fedha za umma huku Wananchi maskini wakiendelea kulipishwa kodi itakwisha?

(b) Wakati mwingi ambao tunaendelea kuhoji hapa Bungeni kwamba ni kwa nini fedha za umma hazipatikani zile ambazo mafisadi wanazichukua, majibu ya Serikali mara nyingi wanasema wahusika wametoroka au wamefariki dunia; je Serikali haioni ni vyema leo iseme isikike Watanzania wasikie ili ukweli ubainike; je, aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu wa Tanzania, Ndugu Balali ni kweli amefariki dunia; na kama ni kweli; je, Serikali iko tayari kutoa ushahidi wowote wa mkanda wa video ili asiingie katika ile historia ya wale ambao wamezikwa kwenye Bahari Kuu kama Osama Bin Laden? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI YA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU):** Mheshimiwa Spika, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imechukua hatua mbalimbali zikiwemo onyo, adhabu ama kufukuzwa kazi kwa baadhi ya Wakurugenzi katika kipindi cha mwaka 1998 - 2010, kiasi cha Wakurugenzi 75 wamefukuzwa kazi. Vilevile Halmashauri 33 zimechukuliwa hatua mbalimbali kuanzia mwaka 2005/06 mpaka 2009/10, ikiwemo kufikishwa mahakamani baadhi ya Halmashauri. Kama tutakumbuka vizuri, hata Waziri Mkuu ilibidi aingilie kati, alikwenda Bagamoyo baada ya kupata Taarifa ya *CAG* kwamba, mambo kule siyo mazuri, akachukua hatua yeye mwenyewe binafsi na kuweza kuwachukulia hatua wale watu ambao walikuwa wamefanya ubadhirifu pale Bagamoyo na sasa hivi shauri liko Mahakamani. Vilevile kuna Halmashauri zingine nyingi ambazo hatua hizi zimechukuliwa zikiwemo Kilosa, Rombo na hata Kishapu.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la kuhusu kama Balali yupo hai au vipi; taarifa ambazo mimi ninazo mpaka sasa na ambazo kama wengi mnafahamu ni kweli tulipokea taarifa kutoka Ubalozi wetu kule alipokuwa Marehemu Balali kwamba, amefariki na amezikwa huko huko. Sasa Balali kweli hatutamwona amekufa na mambo yake yote amekufa nayo. (*Kicheko*)

**SPIKA**: Mnanishangaza kweli, sasa akija akawatokea usiku mtasemaje?

Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha, ninaomba niwatangaze wageni wetu waliopo hapa. Tunao wanafunzi 20 na walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari ya Gonja, ambayo iko Wilaya ya Same, Mkoa wa Kilimanjaro. Ninaomba walimu na wanafunzi wasimame; ahsante sana, karibuni sana, ninajua mmesafiri safari ndefu. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 80 na walimu wao watatu kutoka Shule ya Sekondari ya Msalato iliyopo Dodoma, ahsanteni sana. Tunaambiwa hii ni Shule ya Vipaji Maalum, kwa hiyo, tunaomba msome sana hii ni shule ya wasichana peke yao; jitahidini mje mchukue Uspika hapa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunayo matangazo ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa January Makamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuwa, leo tarehe 16, saa saba mchana, kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Msekwa B.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, leo saa saba watakuwa na kikao Chumba Namba 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Augustino Lyatonga Mrema, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, saa tano na nusu kutakuwa na kikao kitakachofanyika katika Ukumbi wa Msekwa C. Ninapenda sasa hivi tuanze kufanya vikao saa saba, kwa sababu Wabunge wengi wanakuwa hawapo, lakini kwa leo mfanye saa tano na nusu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Serukamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana, watakuwa na mkutano Chumba Namba 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi Chana, anawatangazia Wajumbe wake kwamba, saa saba mchana, watakuwa na kikao Chumba Namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba, watakuwa na mkutano katika Ukumbi wa Msekwa C; ninaona mtakutana na Kamati ya Hesabu za Serikali, kwa hiyo, mtajua huko huko Makatibu wenu wataangalia wapi anakaa nani. Mtatangaziwa mtakapokaa kwa sababu kuna wengine nimeshawatangazia hapa.

Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mwenyekiti wa Chama cha Maskauti wa Hiari cha Wabunge Maskauti, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kikundi hicho na Waheshimiwa Wabunge wengine wanaotaka kujiunga na kikundi hicho kwamba, leo hii saa saba kutakuwa na kikao katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Hawa ni Chama cha Maskauti, mnaalikwa kule; mtajua wenyewe, Makatibu wenu wataangalia namna gani mtakaa kwa sababu kuna Kamati nyingi zimepangwa kwenye Ukumbi huo.

Waheshimiwa Wabunge, ninafikiri kulikuwa na Mwongozo wa Mheshimiwa Tundu Lissu.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo kuhusu jambo ambalo limetokea wakati wa kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu. Wakati wa kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu, mimi mwenyewe pamoja na Mheshimiwa Esther

Matiko, tumemwuliza Waziri Mkuu kuhusiana na mauaji ambayo yamekuwa yanafanywa na Jeshi la Polisi katika eneo la Nyamongo kwenye maeneo yanayozunguka Mgodi wa *North Mara*.

Mheshimiwa Spika, ulikataza maswali hayo yasijibiwe kwa hoja kwamba, masuala haya yapo mahakamani. Kanuni ya 64(1)(c), inasema kwamba, Mbunge hatazungumzia jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama. Kwa kesi zote 52 za Watanzania waliouawa na Jeshi la Polisi mwaka jana na watu 72 ambao wameuawa na Jeshi la Polisi, tangu mwaka 2008 Januari, hakuna kesi hata moja ya mauaji inayowakabili waliohusika na mauaji hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, mimi na baadhi ya watu wengine, tumeshtakiwa kutokana na matukio ya Tarime, lakini hatujashtakiwa kwa mauaji. Hatujashtakiwa kwa suala lolote linalohusu mauaji ya Watanzania 72 katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Sasa ninaomba ufafanuzi kwa nini maswali yanayohusu mauaji yanayofanywa na Polisi ambayo hayako katika Mahakama yoyote, yamekataliwa kujibiwa. Labda taarifa nilizonazo siyo sahihi sana, pengine kuna taarifa ambazo waliohusika na mauaji haya wamefunguliwa mashtaka mahali fulani; mimi sielewi labda wewe Mheshimiwa Spika unafahamu.

Kwa hiyo, ninaomba mwongozo wako kama kuna kesi yoyote ambayo inahusu Polisi waliohusika na mauaji haya basi tuambiwe ili haya maswali yawe yamekataliwa kwa mujibu wa kanuni hizi. Kama hakuna kesi, basi tutaomba maswali yetu yajibiwe kwa mujibu wa kanuni hizi. Ninaomba mwongozo wako. (*Makofi*)

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, nami ninaomba kutumia Kanuni hiyo hiyo ya 64(2), ambayo inasema; Mbunge yeyote anayeamini kuwa Mbunge mwingine amevunja au amekiuka masharti ya fasihi ya kwanza ya kanuni hii, atasimama mahali pale na kumwambia Spika wa Bunge kuhusu utaratibu. Mimi niliwasikiliza vizuri Waheshimiwa Wabunge hawa wawili walipokuwa wanauliza katika kile kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu, walikuwa *specific* wanazungumzia mambo yanayohusiana na Mgodi wa Nyamongo, Tarime.

Mimi siyo Mwanasheria, Mheshimiwa Tundu Lissu yeye ni Mwanasheria. Ni kweli kabisa Mheshimiwa Tundu Lissu na mwenzake wako nje kwa dhamana kwa kesi inayowakabili na ni kweli kabisa nilivyosikia haina mahusiano na mauaji ya Polisi, lakini ni kesi inayohusiana na Mgodi wa Nyamongo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwa utamaduni na kwa utaratibu na kanuni hizi fasili ya (c) inazungumza wazi kwamba, Bunge au Mbunge yeyote hatazungumzia jambo lolote ambalo linasubiri uamuzi wa Mahakama na jambo hili linazungumzia mgodi na Askari wanaosemekana wameuawa katika eneo la mgodi; je, kwa nini tusiiachie Mahakama ikamilishe kazi hii ambayo ina uhusiano?

Kuendelea kulijadili jambo lenye kesi Mahakamani linalohusiana na Mgodi wa Nyamongo liwe la Polisi au liwe la Raia siyo kuingilia uhuru wa Mahakama? Pamoja na mwongozo wa Mheshimiwa Tundu Lissu, lakini ninaridhika kabisa kwamba, kifungu (c) cha Kanuni ya 64, kinatuzuia sisi Wabunge kupenda kuhoji mambo yaliyoko Mahakamani.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Ninaomba isiwe utaratibu zaidi ya mmoja, ndiyo kanuni zetu zinavyosema. Sasa nitaanza na mwongozo alioomba Mheshimiwa Tundu Lissu.

Waheshimiwa Wabunge, tusijifanye sisi ndiyo Mahakama ya kila kitu na tunajua kila kitu. Waheshimiwa Wabunge wawili hawa, hivi sasa wako kwenye dhamana. Sasa Mheshimiwa Matiko yupo na Mheshimiwa Tundu Lissu yupo na eneo linalozungumziwa ni lile ambalo imetokea hitilafu kwa ajili yao. Wako kwenye tuhuma. Sasa tukisema hawa, afadhali angeuliza mtu mwingine, lakini hawa hawa, ninasema *to be on the safe side*, tutumie kifungu hiki cha 64(1)(c), jambo hili libakie huko liliko. Hatuna hasara yoyote wala hatutapata faida yoyote kwa kusema tuanze kuzungumza hapa suala ambalo ni refu na la siku nyingi. Kwa hiyo, ni huko huko ambako wao wametuhumiwa. Huo ndiyo uamuzi wangu kwamba; haya masuala tuiachie Mahakama. Hivyo ndivyo nilivyoamua.

Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, bila kuathiri, ninataka kutumia Kanuni ya 5(4), ipo katika kifungu cha uendeshaji wa shughuli za Bunge na Uongozi, ambapo kanuni ya 5(1) inaelezea suala zima la utaratibu wa mamlaka ya Spika katika uendeshaji na uongozi bora wa vikao. Kanuni ya ndogo ya (4) inasema; Mbunge yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa Spika, anaweza kuwasilisha sababu za kutokuridhika kwake kwa Katibu wa Bunge, ambaye atawasilisha malalamiko hayo kwa Spika.

Maana yangu ni kwamba, katika uendeshaji bora wa vikao, baada ya wewe kutoa uamuzi hakuna Mbunge yeyote anayeweza kuendelea kubishana na Kiti ili kuleta uendeshaji mzuri wa vikao na kama mtu atakuwa na hoja anaweza kuleta malalamiko yake kwa kupitia utaratibu huu.

Ninalisema hili bila kuingilia maudhui ya hoja ya Mheshimiwa Tundu Lissu, kwa sababu undani wake siujui ila ninataka kulieleza hili ili kuepusha malumbano kati ya Wabunge na Wabunge kuheshimu Mamlaka ya Spika ili kuleta uendeshaji mzuri wa vikao. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa hiyo, hiyo ni taarifa ambayo Mheshimiwa Ole-Sendeka ametwambia sisi Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu kuna tabia moja hapa; mtu anasimama na mwingine anasimama, lakini ninashukuru kuanzia juzi na jana, mmefanya vizuri sana. Kwa hiyo, kama maamuzi ya Spika hujaridhika nayo, huu ndiyo utaratibu, utaandika kwa mujibu wa Kanuni hii aliyoisema utapeleka kule na kama ni lazima Kamati ya Kanuni itashughulikia suala hilo ambalo mimi ndiyo Mwenyekiti wake na *Deputy* wangu ni *Deputy Speaker*.

Siku hiyo ambayo tutatuhumiwa na Mbunge huyo, mimi nitaondoka kwenye Kiti, pia *Deputy Speaker* hatakuwa kwenye Kiti watamchagua Mbunge mwingine aliyeko ndani ya Kamati ile kusudi waweze kusikiliza hilo suala linalohusika. Huu ndiyo utaratibu wa Kanuni ya 5(4).

**TAARIFA**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa sasa siihitaji, ninaendelea na kazi. Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu nina shughuli nyingine, nitamwomba Mheshimiwa Mwenyekiti, aweze kuendelea na shughuli zinazoendelea.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. George B. Simbachawene) Alikalia Kiti*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, maana hata Kiti chenyewe sijakikalia vizuri tayari taarifa. Kwanza, hakuna kitu kinachoitwa Taarifa ya Hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kanuni ya 55. Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Sijakupa nafasi ngoja nijiridhishe. Mheshimiwa Mbunge, ukienda sehemu ya pili ya kifungu cha 55, taarifa ya hoja yoyote itatolewa kwa maandishi na itawekwa saini na Mbunge anayeitoa kabla ya kupokelewa na Katibu, kufuatana na masharti ya Kanuni hizi. Kwa hiyo, taarifa yako kama ipo ya hoja na kupitia kanuni hii ya 55, basi unaweza ukaipeleka kwa Katibu kwa maandishi na ndiyo utaratibu. Kwa hiyo, tunaendelea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha tatu, usisome cha pili, soma cha tatu kuna taarifa ambazo zinaweza kutolewa bila maandishi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, ukipewa Kiti unakuwa na kitu kinachoitwa *discretion power*; inawezekana nikawa nimetereza, upo utaratibu wa kufanya kama Kiti kimekosea na umetoka kuelezwa sasa hivi. Kwa kuwa nimeshatoa *ruling*, basi tunaendelea na ninaamini kwamba, hujaathirika chochote kwa sababu una fursa nyingine pia.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wa bajeti na mchangiaji wetu wa kwanza kwa siku ya leo atakuwa Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Khamis Seif na baadaye Mheshimiwa Kisyeri Chambiri.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuichangia bajeti yetu. Awali ya yote, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, ambaye ametuwezesha sisi sote kuwa ndani ya chombo hiki. (*Makofi*)

Pili, kwa namna ya kipekee kabisa, nitumie fursa hii vilevile kuwashukuru Wananchi wa Mkinga, kwa heshima kubwa waliyonipa na kuniamini kuwa mwakilishi wao katika Bunge letu Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili bajeti iwe na maana, lazima bajeti hiyo itoe majibu ya matatizo yanayowagusa Wananchi. Bajeti iliyoko mbele yetu inalenga huko. Nitumie fursa hii kuipongeza sana Serikali, kwa kutuandalia bajeti nzuri, inayolenga kutoa majibu kwa matatizo ya Watanzania. Nitumie fursa hii kusema ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na bajeti nzuri kwenye makaratasi ni jambo moja na bajeti nzuri inayotekelezeka ni jambo la pili. Bajeti nzuri hii tunayoisifia ili iwe na maana lazima tuitekeleze vizuri. Mimi ninaamini kabisa tutaitekeleza vizuri. Wito wangu tujitahidi kwa kadiri ya uwezo wetu, kuhakikisha kwamba tunaondoa urasimu ili bajeti hii itekelezeke. Tuhakikishe fedha hizi tunazozipitisha leo zinapatikana kwa wakati, zinapelekwa kwenye Wilaya zetu kwa wakati na tunasimamia vizuri utekelezaji wake ili tuweze kufikia malengo tunayokusudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia katika hoja zilizoko mbele yetu, kwa maana ya Hotuba ya Hali ya Uchumi na Hotuba ya Bajeti. Wakati mwingine nitaendelea kugusia kidogo yale yaliyozungumzwa na Mpango wetu wa Maendeleo. Sasa tumeambiwa kwamba, mwaka huu unaokuja wa fedha, utakuwa ni mwaka kianzio cha bajeti hiyo.

Nianze na suala la upatikanaji wa huduma za kifedha nchini. Hali yetu ya uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi siyo nzuri. Taarifa mbalimbali tulizonazo na tafiti mbalimbali zinaonesha kwamba, *access* ya *financial services* nchini, asilimia 56 ya Watanzania hawapati huduma za kifedha. Hili siyo jambo zuri kuona asilimia 56 ya Watanzania hawapati huduma za kifedha. Lazima tujielekeze kuhakikisha kwamba, Watanzania wanawezeshwa wanapata huduma za kifedha ili waweze kushiriki katika shughuli za maendeleo. (*Makofi*)

Ukipitia *Finscorp Report* inaonesha kwamba, ukilinganisha na utafiti uliofanyika mwaka 2006 na utafiti uliofanyika mwaka 2009, hali ya upatikanaji wa fedha inazidi kuwa mbaya.

Kundi la vijana kati ya miaka 13 mpaka 35 linazidi kukumbwa na tatizo la upatikanaji wa fedha. *Access liquidity* iliyoko katika mabenki yetu kwa maana ya *assets*, kwa mwaka 2009 mabenki yalikuwa na *6.6 trillion* ya *assets*. Vilevile yalikuwa na 5.5 trilioni kama sikosei ya akiba zilizoko kwenye mabenki yetu. Asilimia 56 ya Watanzania hawawezi kupata huduma za kifedha. (*Makofi*)

Hii ni *clearly market failure*. Lazima Serikali tujielekeze kwenye ku-*address* tatizo hili. Ninatambua zimefanyika jitihada mbalimbali za kuhakikisha kwamba, Watanzania wanapata huduma za kifedha.

Kama nguvu kazi kubwa ya Watanzania ni vijana na ndiyo kundi kubwa ambalo hawapati huduma za kifedha, maana yake ni kwamba, kundi kubwa hili la Watanzania halishiriki katika kujenga uchumi wa nchi yetu, hatuwezi kuendelea kuiachia hali hii iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya Waziri imeonesha kwamba, kupitia Mifuko mbalimbali tumeweza kujitahidi kuboresha huduma za kifedha. Mmezungumzia SACCOS, ukienda kwenye ukurasa wa 38 wa Bajeti, imeoneshwa kwamba, tumepiga hatua kutoka mwaka 2005, tulikuwa na SACCOS 1,875, mwaka 2010 tuna SACCOS 5,344. *Membership* imeongezeka kutoka watu milioni moja laki tatu na sitini mpaka milioni mbili na laki moja. Tujiulize, kwa Tanzania yenye *population* ya watu karibu milioni 45, vyama hivi vinaweza kuhudumia watu milioni mbili peke yake? Hii siyo sahihi ndiyo maana *penetration rate* ya huduma za kifedha vijijini iko chini sana. Hata tukisoma katika mistari kuhusu takwimu hizi tunazopewa, unapozungumzia *membership* ya watu milioni mbili na laki moja kwa vyama 5,000, unazungumzia wastani wa watu mia tatu na kitu kwenye kila chama; hili ni tatizo kubwa.

Wenzetu jirani leo hii wanazungumzia chama kimoja kuwa na wanachama laki moja kuendelea, sisi tunazungumzia chama kimoja kuwa na wanachama mia tatu; lazima jitihada zifanyike kuhakikisha Wananchi wanahamasishwa wajiunge kwenye vyombo hivi ambavyo ndiyo vinavyowagusa Wananchi wa chini kabisa ili waweze kupata huduma hizi za kifedha. Tunapozungumzia huduma hizi, lazima vilevile tuweke miundombinu na *safeguards* za kuhakikisha kwamba, fedha hizi za Wananchi, michango hii inalindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya Waziri inaeleza kwamba, akiba zilizokusanywa kwenye vyama hivi, zinafikia bilioni 174.6, lakini la kusikitisha usimamizi katika vyama hivi haupo makini. Mimi nimetoka kwenye sekta hii, ninaelewa uwezo wa Idara yetu ya Ushirika ulivyo katika kusimamia vyombo hivi. Hatujaiwezesha inavyopasa Idara ya Ushirika kuvisimamia vyama hivi. Idadi kubwa ya Vyama vya Ushirika havikaguliwi; sasa hili ni bomu, tunatengeneza bomu lingine, tunatengeneza *DECI* nyingine kwa mitaji ya Wananchi. (*Makofi*)

Ninaiomba Serikali iliangalie kwa umakini suala hili, watu wamekwishaanza kujenga imani na Vyama vya Ushirika, tusiache imani hii ipotee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la uvuvi. Tuna kilometa karibu 800 katika Ukanda wa Pwani, lakini Sekta ya Uvuvi hatujaitumia ipasavyo. (*Makofi*)

Kutoka mwaka 2005 mpaka leo, taarifa inatwambia kwamba, uchangiaji wa Sekta ya Uvuvi umekuwa ukishuka kutoka asilimia 6 mpaka 1.5; hii haikubaliki. Nimefurahi kusikia Wizara imeondoa kodi katika nyavu, vilevile imeondoa kodi kwa wale wanaotaka kusafirisha nje. Hii haitoshi kwa sababu taarifa hii ya Waziri inatwambia kwamba, moja ya tatizo kubwa lililochangia katika kushuka mapato ya uvuvi ni matumizi ya dhana duni za uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wetu bado wanatumia majahazi na mitumbwi ya enzi ya Nabii Nuhu, tunatakiwa kutoka huko. *(*M*akofi*)

Tunatakiwa sasa teknolojia ya kutumia *fibre boat* iingie nchini mwetu; hii itatuhakikishia usalama zaidi kwa wavuvi wetu, vilevile itawawezesha wavuvi hawa kuweza kwenda kwenye maeneo ya kina kirefu cha bahari. Tayari tunao Watanzania waliothubutu kuanzisha viwanda vya kutengeneza *fibre boat* hapa nchini. Ukipitia kwenye viwanda vile, bei ya boti zile ziko juu sana na ukiwauliza sababu ni nini wanasema *materials* za kutengenezea boti hizi ni ghali mno na ni gharama kubwa, zinatozwa kodi kubwa zinapoingia hapa nchini.(*makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza kodi katika vifaa hivi vya kutengenezea boti ili boti hizi zitengenezwe hapa hapa nchini, tuweze kuongeza ajira kutokana na utengenezaji wa boti nchini humu. Vilevile wavuvi wetu waweze kupata dhana bora ambazo zitatuwezesha kuvua na kupata mapato makubwa zaidi kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Bado hatuna wavuvi wakubwa, imani yangu tukiamua tunaweza kutengeneza wavuvi wakubwa. Tuna vijana wengi wazuri wanatoka pale Chuo cha Uvuvi Mbegani, tukiamua kuwabadilisha vijana hawa wakaingia kwenye Sekta ya Uvuvi tunaweza. Mheshimiwa Waziri Mkuu, usiloweza ni kusema sasa hivi iwe usiku hautakuwa usiku, kusema sasa hivi iwe mchana hilo haliwezekani, kwa sababu haya ni majaliwa ya Mwenyezi Mungu pekee yake, lakini ukiamua kusema mwaka huu tunataka tuwe na

wavuvi wakubwa, vijana wetu wasomi watano kwa kuanzia na kuhakikisha kwamba, wanapatiwa mitaji ili wajielekeze katika Sekta ya Uvuvi, hili unaweza.

Ninakuomba ulisimamie hili, tunazo taasisi zetu zinafanya kazi nzuri, Taasisi ya *SELF* imefanya kazi nzuri, ukiweza kuwaelekeza wafanye *pilot* katika Sekta hii ya Uvuvi, watoe mikopo kwa wavuvi wakubwa wa Kitanzania, Vijana wa Kitanzania wajiingize kwenye Sekta hii ili tuweze kupata uzoefu wa kujiingiza katika Sekta, hili linawezekana. Ninakusihi sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ulisimamie hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye ahadi ambazo zipo katika Wilaya yangu ya Mkinga. Tuna tatizo la hospitali na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, alipokuja Mkinga alituahidi kwamba, kwa mazingira ya Wilaya yetu, tunahitaji tupate Hospitali ya Wilaya, vilevile Kituo cha Maramba kiongezewe hadhi ya kuwa Hospitali ya Wilaya. Tunashukuru ahadi hizi zimeanza kutekelezwa, lakini utekelezaji wa ahadi hizi unakwenda taratibu mno, tunaishukuru Serikali imeweza kutuletea *ambulance* katika Kituo chetu cha Maramba, tunaishukuru Serikali tayari imeanza kufanya ukarabati kwenye nyumba za madaktari, lakini tunasema *speed* hii bado ni ndogo, tunaiomba Serikali iongeze *speed* ya kukamilisha ahadi ile ya Mheshimwia Rais.

Tunaishukuru Serikali kwa upande wa barabara, tunajengewa kwa kiwango cha lami Barabara ya Tanga - Horohoro. Barabara hii siyo tu kwamba, itafungua uchumi kwa Wilaya yetu ya Mkinga, lakini itafungua nchi yetu na nchi jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamekuwepo manung‘uniko ya fidia kwa barabara ile, lakini tunashukuru Mheshimiwa Rais ametoa ahadi kwamba, watu waliohamishwa katika barabara zile na waliovunja nyumba zao kwa ridhaa yao wenyewe watafidiwa. Imani yangu ni kwamba, ahadi ya Mheshimiwa Rais itaanza kutekelezwa kupitia bajeti hii. Ninamshukuru Naibu Waziri, amekuja Mkinga kulishughulikia suala hili; imani yangu ni kwamba, ahadi alizozitoa zitaanza kutekelezwa. Tuna tatizo la maji, tunaomba bajeti hii ilishughulikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kusimama hapa leo, lakini la pili, ninakushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali mara hii imetuletea bajeti ambayo ina thamani ya shilingi 13,525,895,000. Fedha hizi zikipatikana, inawezekana pengine tukapata hayo maendeleo ambayo yamepangwa katika Mpango huu wa Bajeti. Kupanga ni suala moja na utekelezaji ni suala lingine. Ukosefu wa upatikanaji wa mapato haya ambayo yametajwa katika bajeti hii, kwa kweli utaweza kuivuruga bajeti nzima.

Sasa kabla ya kulijibu suala la kwamba, Serikali ina uwezo wa kukusanya shilingi 13,525,895,000, kama Serikali itakuwa haina uwezo wa kukusanya fedha hizi, basi bajeti yetu yote itakuwa haina maana, inakuwa ni bajeti ya kufurahisha, lakini utekelezaji wake

utakuwa na matatizo na suala hili ni vyema tukajielekeza Wabunge wote na nchi kwa ujumla kuangalia uwezekano wa Serikali kuweza kutimiza kiwango ambacho wameahidi katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kulijibu swali hili, mimi ninaona bora tuangalie utendaji wa Serikali katika suala zima la ukusanyaji wa mapato, ninafikiri tukishasoma hapo tunaweza tukajua kama Serikali ina uwezo au haina. Katika kulikabili hili, tuangalie bajeti tatu ambazo zimepita zinazohusiana na ukusanyaji wa maduhuli, tuone Serikali imefanya nini.

Ninadhani tukipata mfano huu na mifano mingine, hapo tutakuwa na uwezo wa kusema Serikali ina uwezo wa kukusanya trilioni 13.52 au haina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Mwaka 2007/2008, Serikali ilitaka idhini Bungeni ikusanye maduhuli yenye kiwango cha shilingi 6,160,992,762,345. Serikali iliomba idhini na kama kawaida ya Bunge hili, ninadhani idhini ilitoka, lakini makusanyo yaliyofanywa kwa bajeti hiyo ya 2007/2008 ni shilingi 5,303,427,370,743.

Ukichukua makisio au walichoomba Serikali na ambacho kimekusanywa, utakuta kuna upungufu wa shilingi 555,565,421,602. Hapa utaona Serikali kile ambacho wamekiomba Bungeni hawakukifikia, kuna upungufu wa bilioni 855.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo hazikukusanywa katika Bajeti ya Mwaka 2007/2008 ilikuwa ni sawasawa na Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maji kama zingepatikana.

Tusiishie hapo, twende katika Bajeti ya 2008/2009, Serikali iliomba idhini ikusanye maduhuli ya shilingi 7,704,909,780,495 ikakusanya shilingi 6,427,630,892,809; Bajeti ya Mwaka 2008/2009, upungufu ulikuwa shilingi 1,277,278,888,669; kwa Bajeti hii, Serikali ingeweza kuikidhi Bajeti ya Wizara ya Afya na Wizara ya Nishati na Madini, lakini haikukusanywa licha ya kupewa idhini na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya 2009/2010, Serikali iliomba ridhaa kutoka Bungeni ikusanye maduhuli ya shilingi 10,063,686,670,897, makusanyo yalikuwa shilingi 7,728,122,247,611. Hapa upungufu ni shilingi 2,135,564,422,280, hii ni sawasawa na asilimia 21.22 ya upungufu.

Kwa hiyo, hapa itadhihirika kuwa, kwa hii nyanja moja tu ya maduhuli, Serikali imeshindwa kufikia lengo kwa pesa ambazo wameomba wenyewe wakusanye na Bunge likawaruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia nyingine inayoipatia fedha nchi yetu ni misaada kutoka nje. Katika Bajeti ya 2009/2010, Serikali ilikisia kukusanya makusanyo kutokana na misaada kutoka nje shilingi 3,932,477,455,117, lakini zilizopatikana ni shilingi 2,393,256,357,651, hapa pana upungufu wa shilingi 1,538,918,097,466.

Kwa hiyo, utendaji wetu hauridhishi na misaada kutoka nje haikupatikana kama ilivyopangwa. Kwa hiyo, ni ushahidi tosha kuonesha kuwa, Serikali haifikii lengo la kukusanya mapato yale ambayo wanaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie Bajeti ya 2010/2011, hapa kwa sababu mwaka wa fedha haujakwisha, lakini kuna ushahidi unaoonesha kuwa, bado utendaji wa Serikali hauridhishi katika kukusanya mapato. Mfano, Wizara ya Maliasili na Utalii, ilitakiwa ipewe shilingi 65,506,240,000 mpaka Aprili imepewa shilingi 35,084,177,687 na hapa imebaki miezi miwili tu kukamilika mwaka.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliidhinishiwa kupewa shilingi 53,848,061,000, walizopewa ni shilingi 27,737,178,679.

Kutokana na hali hii inaonekana kuwa, Serikali kile ambacho wanakipanga hawawezi kukikusanya na hii imejionesha kwenye Bajeti ya 2010/2011, ambapo waliomba hapa tuwaidhinishie matumizi ya shilingi trilioni 11.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hii, mimi nina mashaka makubwa kuwa, shilingi trilioni 13.52 ambazo Serikali wameomba ili wakusanye, hizi hazitopatikana kabisa. Kwa hiyo, hii Bajeti kwa kweli ipo, lakini athari zake zitaonekana kuwa Wizara hazitopata pesa na baya zaidi fedha ambazo zinakosekana ni za maendeleo, fedha za kawaida na mishahara zipo. Unaposikia Bajeti ina upungufu, basi ni fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu inakuwa na mazungumzo na Shirika la Mfuko wa Fedha wa Kimataifa *(IMF)* ambalo wanakaa katika kupanga bajeti ili nchi yetu pengine ikopesheke au iweze kupata misaada kutoka nje. Jambo la kusikitisha ni kuwa, kile wanachokubaliana na Serikali yetu na *IMF* sicho kinacholetwa Bungeni. Sasa hili ni la tatizo. Kwa mfano, mwaka 2010 bajeti ya mwaka 2010/2011, bajeti ya Serikali iliyoletwa hapa Bungeni ni shilingi trilioni 11.6, lakini bajeti ya makubaliano ya Serikali na *IMF* ni shilingi trilioni 10.1. Sasa hili ni tatizo kwa sababu kile ambacho wanakubaliana hawa sicho wanachotuletea sisi kukijadili hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile bajeti hii ya Serikali tunayoizungumza, kama ambavyo nimesema imeonyesha ni shilingi trilioni 13.52. Lakini walichokubaliana na Serikali na *IFM* ni shilingi trilioni 11.62. Hapa pana tofauti ya shilingi trilioni 2.27. Hili ni tatizo kwa sababu kile ambacho wamekubaliana na Serikali na *IFM* ilikuwa ndicho kinachopaswa kuletwa Bungeni. Lakini kinachokubaliwa ni kingine, na kinacholetwa Bungeni hapa ni kingine. *(Makofi)*

Kinachoonekana ni kwamba karibu kile tunachokubaliana ndiyo mapato au matumizi ya Serikali. Kwa mfano, bajeti iliyopita inategemewa kuwa Serikali itatumia shilingi trilioni 10.4 wakati wao walisema ni 11.6 mapato pamoja na matumizi. Kwa hiyo, inaonekana kwamba kile wanachokubaliana kinakuwa ni sahihi. Kwa hiyo, mimi nasema kuwa kwa kweli hii bajeti ina matatizo makubwa licha kuwa inasifiwa, lakini

uwezekano wa kupata fedha zikatumika siyo rahisi, na inawezekana pengine zikapungua siyo chini ya shiling trilioni mbili ninavyohisi. Kwa hiyo, zinapopungua shilingi trilioni mbili katika trilioni 13, basi hapo itakuwa tena kinachokubaliwa ni zaidi na kinachohusiana na maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za kutofikia lengo la makusanyo ni kama ifuatavyo: imeonekana katika bajeti ya mwaka 2009/2010 Wizara ya Nishati na Madini katika *Vote 58* katika Fungu la Maendeleo au pesa za maendeleo, ilitakiwa mwaka huo ipewe shilingi bilioni 107.6, lakini matokeo yake wakapewa shilingi bilioni 74.4 na hapa ndipo palipo na Shirika la Umeme la *TANESCO* ambalo kila situ hulaumiwa hapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaweza tukailaumu Wizara ya Nishati na Madini kumbe fedha za maendeleo hazipo. Lakini katika mkusanyo mkubwa ule inaonekena kwamba zitakuwepo. Wizara ya Maji, *Vote* ambayo ni 49, fedha ya maendeleo walizokisia ni shilingi bilioni 245.7. Walizopewa ni shilingi bilioni 160.7. Kilimo, *Vote 43*; Kilimo Kwanza hapa, makisio ni shilingi bilioni 92.7 lakini walizopewa ni shilingi bilioni 71.2. Katika Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana, hapa ndiyo panatakiwa itoke ajira ya vijana. Pesa za Maendeleo walikisia shilingi bilioni 7.9 na walizopewa ni shilingi bilioni 3.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa vyovyote inajenga hofu kuwa trilioni 13.52 hazitapatikana. Kwa hiyo, itakuwa tu katika maandishi, lakini katika utekelezaji hazipo. Kwa hiyo,bajeti hii inaingia katika tatizo hilo ambalo litaonekana kwa juu, ni zuri, lakini kwa kweli bajeti yenyewe haiwezi kukidhi haja ambazo zimekusudiwa. Kwa hiyo, ushauri wangu kwa Serikali kwa kweli watuletee bajeti ambayo inastahiki kutekelezeka au iliyokuwa na uwezo wa kutekelezeka. Vinginevyo, kwa kuweka mahesabu makubwa, matokeo yake mwisho wa mwaka ikawa hakuna kilichofanyika au nusu ya kilichofanyika kwa kweli itakuwa hatupigi hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali Khamis Seif. Sasa anayefuatia ni Mheshimiwa Kisyeri Werema Chambiri na baadaye Mheshimiwa Joelson Luhaga Mpina ajiandaye kama yupo. Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, karibu.

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kukushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Spika - Mheshimiwa Makinda kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani kwa familia yangu kwa kunivumilia muda wote ule tuliokuwa na kampeni za Ubunge mwaka jana na kunivumilia mpaka sasa kwa shughuli kwa sababu kazi za siasa zinafanya mtu uwe mbali na familia. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa kunivumilia na kuniwezesha kufanya hii kazi kwa utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani kwa wananchi wa Babati Mjini, naomba nitoe shukrani kwa maana kwamba katika uchaguzi wa Oktoba 2010 wananchi wa Babati kwa nafasi zote tatu, nafasi ya Urais, nafasi ya Ubunge, nafasi ya Udiwani katika Kata zote walikipa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Babati wanaelewa kabisa kwamba yeyote anaweza kuwa Mbunge na yeyote anaweza kuwa Rais. Lakini Mbunge bora, Rais bora, na Diwani bora anatokana na Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho napenda niwashukuru sana wananchi wa Babati, wameonyesha ndani ya nchi yetu kwamba sisi Tanzania ni nchi moja. Mimi nilizaliwa Mkurya, baadaye nimehamia Babati, lakini wananchi wa Babati kwa wingi wao ambao ni Wairaki hawakuona kwamba ni mbaya Mkurya awe Mbunge wao. Kwa hiyo, wakaonyesha kwa vitendo kwamba Tanzania ni nchi moja, na sisi ni kabila moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Serikali itawapongeza kwa tendo hilo na kuonyesha kwamba sisi Watanzania ni wamoja. Nampongeza Waziri wa Fedha kwa hotuba yake ya bajeti kwa jinsi alivyoiwakilisha. Nimpongeze Waziri wa Nchi, Ndugu Wasira, kwa jinsi alivyowakilisha mpango wake wa maendeleo. Hii bajeti ya Waziri wa Fedha ni bajeti nzuri kabisa kwa sababu ingekuwa tuko katika Vyuo Vikuu na hii ni *thesis* ya Waziri wa Fedha ili apate digrii, basi ina maana kwamba Kiongozi wa Upinzani angenyimwa. Sababu yeye amenakili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka kwamba siku za karibuni kule Ujerumani alikuweko Waziri mmoja na wakati akiwa Chuo Kikuu alinakili *thesis* ya mwenzake, baadaye ikagundulika kwamba yeye amenakili. Kwa hiyo, ikabidi ajiuzulu ule Uwaziri wake kusudi ionekane haki inatendeka. Sasa hii ingekuwa ni kupima na kufanya tathmini ingebidi kiongozi huyu wa upinzani ajiuzulu kwa sababu amenakili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kwamba katika kampeni za uchaguzi, kila Chama wakati kinanadi sera zake Chama ambacho kilinadi sera ambayo Watanzania walilazimishwa waiamini, mojawapo ni Chama cha CHADEMA. Waliahidi kwamba toka darasa la chekechekea mpaka Chuo Kikuu watu wangepata elimu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulisoma enzi ile ambayo tulikuwa tunapewa elimu ya bure ambayo unagharimiwa na Serikali. Wakati huo ukimaliza ukaingia Sekondari mpaka unamaliza Chuo Kikuu huelewi kwamba kuna gharama ya masomo ndani ya nchi hii. Sasa nilitegemea kwamba zile hoja walizokuwa wana-*articulate* wakati wa kampeni ndiyo zinge-*reflect* katika hotuba yao ya bajeti. Wangepata hii Serikali wangeiendeshaje kusudi waweze kutimiza malengo yao ya kuwapa Watanzania elimu bure na kuwapa vitu vizuri walivyokuwa wameahidi, sababu wao ni Serikali inayongojea kivulini. Sasa kama Serikali inangojea kivulini, haiwezi kuwa na kitu *original* mpaka iige cha Waziri wetu, sasa itawezaje kupewa uongozi? *(Makofi)*

Katika mpango wetu wa maendeleo, maeneo manne ambayo yamepewa kipaumbele, moja ni eneo la nishati, na nishati ya umeme. Mji wetu wa Babati tumebahatika kuwa na umeme. Lakini maeneo mengi ya mji wa Babati tulionayo ni umeme wa kuona, kwa sababu miti ipo, nyaya zipo na msongo uliopo, ni ule ambao unaweza kuteremshwa watu wakapata umeme. Maana yake ni msongo wa kilovoti 33 na kilovoti 11. Lakini zaidi ya miaka kumi, na tunaendelea kuwa giza, tunashindwa kupata umeme huo. Rai yangu kwa Serikali ni kwamba, sababu hiyo ndiyo hoja yetu kubwa ya maendeleo, itumulike ndani ya jimbo letu la Babati Mjini, yale maeneo ambayo yanastahili ambayo yapo tayari kupokea umeme, waweze kutupatia umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni muda mrefu, kwa mfano eneo la Bonga ambalo liko Babati Mjini, na pamoja na kupewa bajeti miaka minne mizima imepita kabla umeme haujawaka katika eneo hili. Ninachosema ni kwamba, Serikali iweke mkazo pale panapostahili kupata umeme waweke umeme. Halmashauri ya Babati Mjini ilipatikana kwa kugawanya ambayo ilikuwa Halmashauri ya Wilaya ya zamani. Katika kugawanyika huko tukapata Halmashauri ya Babati Mjini.

Lakini katika Halmashauri ya Babati Mjini baada ya kugawanyika, ndani ya Halmashauri yetu, Mkurugenzi wetu bado hana usafiri. Hakuna gari ambayo anaweza kutumia kwa kutekeleza wajibu wake wa shughuli zake za kila siku. Inabidi atembee kwa miguu. Tunaomba Serikali imfikirie na kumpatia gari. Hospitali yetu ambayo ndiyo hospitali inayohudumia karibu wananchi wote wa Wilaya ya Babati haina gari ya Daktari. Tunahitaji gari ya *ambulance.* Naomba Serikali ituangalie iweze kutushughulikia katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kutoa mchango wangu ni eneo la *TRA*. *TRA* ndiyo inakusanya fedha zote za Serikali. Lakini *TRA* wana maeneo mengine ambayo watu wanaonewa katika kukusanya hizo fedha. Eneo la kwanza ninalotaka kuzungumzia ni eneo la leseni za barabara (*road licenses).* Katika eneo la leseni za barabara, inatakiwa mtu akate leseni yake ya barabara ya kila mwaka. Lakini gari yako ikiharibika au ikapata ajali ikawa gereji miaka mitatu, minne unapoitoa gereji hata ule muda iliyokuwa gereji unalazimishwa ukate leseni ya barabara ambapo gari ilikuwa mbovu. Kwa jinsi hiyo, watu wengi wanashindwa kukata hizi leseni za barabara sababu ingetakiwa kwamba hii *road license* ikatwe kwa mwaka ambapo gari iko barabarani, au kama vile ilivyo *insurance,* inakatwa mwaka ule ambapo *insurance* inafanya kazi. Lakini mtu analazimishwa kukatia gari ambayo hata ni mbovu.

Mhesimiwa Mwenyekiti, eneo lingine, siku za karibuni wana-*assess* ushuru wa kulipia gari la kuingia nchini kwa kutumia *depreciation.* Lakini kitu cha ajabu ni kwamba *TRA* badala ya kuchukua bei ya gari iliyonunuliwa miaka tisa iliyopita, wanatafuta *model* na jina la gari hilo, wanachukua bei ya mwaka huu ndiyo wana-*depreciate.* Kwa hiyo, badala ya mtu kulipa ile gharama ambayo ingestahili alipe, analipa gharama ambayo hata ni mara nne zaidi kuliko ile gari aliyonunua. Kwa hiyo, haya maeneo yanatakiwa yatazamwe kwa uangalifu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni eneo la wakandarasi hasa wakandarasi wa barabara. Nataka niseme kwamba mimi mwenyewe ni mkandarasi. Kazi za ukandarasi ndani ya nchi hii, fedha zote ambazo zinatengwa na Serikali kwa ajili ya ukandarasi, sisi wakandarasi wa ndani tunafanya karibu asilimia 20 tu ya kazi hizo zote. Lakini kazi nyingine zilizobaki zinafanywa na wakandarasi wa nje. Ni vigumu sana nchi yoyote ikaendelea ambayo haiwezi ku-*develop manpower* yake, haiwezi ku-*develop* makandarasi wao. Serikali haifanyi *effort* yoyote ku-*develop* makandarasi walioko ndani ya nchi yetu hii.

Juzi Waziri wa Ujenzi alisema kwamba, wakandarasi waungane na wakiungana wanaweza kufanya kazi. Lakini watu masikini kumi wanapoungana ambao hawana kitu, bado watakuwa ni masikini kumi walioungana na hawawezi hata kufikia sifa zinazotakiwa. Kinachotakiwa ni kwamba, ni lazima Serikali iamue kwa makusudi kuendeleza makandarasi wa ndani, *competition* ambayo siyo *fair*, kwa sababu unataka u-*compete* na watu walioendelea wenye mitaji na nyie hamna kitu chochote, ni sawa sawa tu kumlazimisha mtoto aliyezaliwa leo atembee wakati muda wake haujafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine zote zilizobaki duniani zinahakikisha kwamba zile fedha za walipa kodi wao lazima zitumike na wananchi wao. Naamini kwamba ndani ya nchi yetu imefika wakati ambapo zile fedha ambazo ni za walipa kodi wetu, kazi inapopatikana ni lazima zifanywe na Watanzania. Basi hata kama Watanzania hawana huo ujuzi, ni lazima Serikali iwasaidie, iwalazimishe wawe na ujuzi kusudi siku za usoni waweze kupatikana watu watakaokuwa wanafanya kazi kwa ajili ya kuhudumia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi ilitangazwa tenda ya kubomoa jengo lililokuwa linatumiwa na *NASACO*. Lile jengo lilikuwa la ghorofa moja. Waliomba wananchi, fedha zilikuwa za Watanzania, tena za mashirika yetu ya hifadhi. Lakini ile tenda badala ya kumpa Mtanzania, wakampa Mchina kubomoa jengo la ghorofa moja. Yule Mchina wala hakulibomoa, akaenda pale Kariakoo akachukua watu akawapa *contract* wakalibomoa na tindo, kazi ambayo ingewezwa kabisa na Watanzania. Lakini unaona hali tuliyofikia ndani ya nchi yetu hii! Lakini hata hao makandarasi ambao tunawapa ambao sasa hivi kwa kiwango kikubwa wanatoka China…

*(Hapa kengele ya pili iligonga kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hotuba ya Bajeti na nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chambiri. Sasa namwita Mheshimiwa Peter Serukamba na baadaye Mheshimiwa Ahmed Ali Salum na baadaye Mheshimiwa Masauni ajiandae.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi. Lakini nianze na kumpongeza Waziri wa Fedha kwa bajeti yake nzuri

ambayo kwa kweli inajibu kwa kiasi kikubwa matatizo ya Watanzania na nadhani tukienda hivi tutakwenda mbali zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na mambo machache. Naomba labda nichangie ili kuweza kuboresha zaidi. Cha kwanza, ukiangalia vitabu vyetu vya bajeti na mfumo mzima wa bajeti yetu kama nchi, ninachokiona mimi, tunahitaji kufanya mabadiliko makubwa na mabadiliko hayo kwa kweli nadhani ni ya kisera. Ukiangalia kazi kubwa inayofanyika, tunataka tuone mafanikio yawe makubwa na naamini tunaweza kupata mafanikio makubwa zaidi. Lakini tunafanya *cash budget* na kama ni *cash budget* ulitarajia yasiwepo madeni, kwa sababu tuta-*incur* madeni kwa sababu, kama unanunua, ukiwa na pesa hutarajii kuona madeni. Lakini leo ukienda kwenye Idara zetu zote za Serikali wanadaiwa, tena wanadaiwa na wafanyabishara wa ndani. Nenda Magereza kuna madeni, ame-*supply* chakula, ame-*supply* vitu vya kawaida, nenda Polisi, hata wenye mahoteli Dar es Salaam wanaidai Serikali. Sasa ukijiuliza sana, tatizo ni nini, wakati tunafanya kwa *cash budget?* Kwa hiyo, unaona hapa kuna suala la *accountability.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lifanye mageuzi makubwa ili tuweze kuleta *accountability.* Tubadilishe Sheria yetu ya *Finance Act* na tufanye *ammendment* kwenye Sheria ya *CAG.* Wamefanya watu wa *Newzealand* na wamefanya watu wa Australia, kwamba kila Wizara, kila Idara ya Serikali, mwisho wa mwaka watoe *Financial Statements* ambazo zimefuata *International Financial Statements Standards.* Ukiwa-*subject* kutoa *financial statements,* maana yake *disclosure* ni kubwa, maana yake ni kwamba tutaweza kujua hata haya matumizi tunayopigia kelele hapa. Matumizi ya Serikali ni makubwa, yataweza kudhibitiwa. Hiyo ndio njia pekee tunaweza tukadhibiti matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu awe *responsible.* Tunapitisha vitabu hapa, tunapitisha fedha kama Bunge, lakini nenda kwenye Kamati, angalia utekelezaji wa mwaka uliopita, kingine unaambiwa pesa hazijaja. Ili tufike sehemu tuulizane, kama tulipitisha *so much,* kwa nini hazikuja? Kwenye *Financial Statement* ya Waziri wa Fedha, kwa maana ya Katibu Mkuu wa Fedha, atakuwa amesema nilipata hiki, nimekigawa hivi, nimetumia hivi. Itaongeza *accountability* ndani ya Serikali. Lakini kama hatufanyi hivi, miaka yote tutakuwa tunasema matumizi mabaya, matumizi makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiende kuanza kumtafuta mtu, mbona hapa umetumia sana, hapa umetumia kidogo. Mimi nasema, tusiende huko! Tuwa-*subject* kwenye *accountability* na kuwa *responsible.* Akitoa ripoti yake ya mwaka, ripoti ile inakuwa *scrutinized* na *CAG.*

Kwa hiyo, utawajua ma-*CEO* ambao wanatumia pesa vibaya kwa maana ya Katibu Mkuu. Utajua kama ulisema utanunua kitu hiki, mbona ume-*change* sasa umetumia fedha hizi kwenye hiki na Bunge halijui? Tusipo-*issue accountability* na *transparency,* bado mimi ninaamini tutakuwa kila siku tunakuja hapa tunasema matumizi ni makubwa. Lakini ninaamini tukiwa-*subject* kwenye kutoa *Financial Statements* kila

mwaka, hawa Makatibu Wakuu watakuwa *serious* na matumizi ambayo siyo ya lazima, hayatafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Bunge hili, tufanye kama wenzetu. Wamefanya watu wa *Newzealand*, wamefanya Australia. Leo unaona kabisa, wala huhitaji kupiga kelele. Kwa mfano, tumeletewa misaada ya *donors, you know exactly* imeingia kiasi gani na imekwenda wapi na zimetumika namna gani. Bila kufanya hivi, bado tutakuwa tunajaribu tu. Ndiyo maana unaona wenzetu wa upinzani, wanadhani ukijadili posho, ume-*solve* tatizo la nchi. Mimi naseme hapana. Ili tuweze ku-*solve* tatizo kubwa zaidi, twende kwenye *accountability*. Hata kama tutatoa posho, *if we are accountable*, haina shida. Kwa hiyo, mimi ninaomba hili, kwangu mimi ninaliona ni la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni suala la *interest rate. Interests* zetu za kukopa bado ni kubwa sana. Lakini ili *interest rate* ziweze kupungua, yapo mambo ni lazima tufanye. Tanzania tuna ardhi, Mungu ametupa ardhi, nimeona Mheshimiwa Waziri amesema humu kwenye vitabu. Umefika wakati ardhi yote ya Tanzania tuipime na kila mwenye ardhi apewe *tittle deeds* yake. Kila mwenye ardhi akiwa na *tittle deeds* maana yake huyo mtu cha kwanza, anakopesheka. Lakini kukopesheka peke yake haifai, tubadilishe tufanye *reform* kwenye Mahakama. Maana nchi hii mtu anakopeshwa, anatakiwa alipe, anakwenda kuweka *Court Injunction. So these risks* zote, wa mabenki wanazichukua wanazi-*factor in* kwenye *interest rate.*

Pamoja na hata ukishusha *treasury bills*, bado kama hatuja-*solve* haya mengine, *confidence* ya wanaotukopesha haitakuwa kubwa sana. Tumesema hapa, tunapoingia kweli kwenye biashara tukakope kwenye mabenki, tukakope nje, wananchi wakope, inahitaji *a lot of transparency* na inahitaji *a lot of accountability*. Kwa hiyo, mimi naomba tufanye hivyo na wenzetu wamefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007 Rwanda walianzisha mradi huu. Ni nchi ndogo, lakini wamefanya. Wameipima nchi yote, kila mwenye ardhi amepewa *tittle deeds*, na wamefanya *reform* kwenye Mahakama zao. Ukienda kukopa benki ukikataa, kesi haiwezi kumaliza miezi mitatu imetolewa maamuzi. Kwa hiyo, mabenki *confidence* itaongezeka na *interest rate* zitashuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala amelisema hapa mchangiaji aliyepita, la Makandarasi wa ndani. Mimi namwomba sana Waziri wa Fedha, kwa kazi kubwa wanayofanya, tufanye mageuzi makubwa. Leo Wajapani wakikupa pesa za msaada za kujenga barabara, lazima Mkandarasi awe Mjapani. Leo ukipewa pesa na *European Union,* lazima Mkandarasi atoke nchi za *European Union.*

Leo ukipewa pesa na *Denmark*, lazima Wakandarasi watoke *Denmark* au nchi zile zinazowazunguka. Lakini leo tunajenga barabara nyingi kwa pesa zetu, lakini wajenzi wote ni Wachina. Maana yake tuna-*transfer* uchumi wetu kwenda kueneza kwa Wachina. Hili linahitaji *a serious intervation,* tuamue kama mradi huu ni wa Serikali, barabara hii inalipiwa na Serikali mia ya mia, tuseme lazima anayekuja kufanya barabara hii aidha

awe Mtanzania ama awe *jointventure* na mtu mwingine. Maana yake ni pesa nyingi zitabaki kwenye uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wachina hawa wanachofanya, pesa ni za kitanzania, lakini bei pale kuna *component* ya dola, kuna *component* ya *Tanzanian shillings*, maana yake tuna-*transfer,* inabidi sasa tununue madafu kuwalipa hawa Wachina wapeleke kwao.

**T A A R I F A**

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nimpe taarifa Mheshimiwa Serukamba, alipozungumzia kwamba kitendo cha kuwapa Makandarasi wa nje kwa kutumia fedha za nchi yetu ni sawa na kuhamisha mali kutoka kwa maskini, zinakwenda tena kwa tajiri. Taarifa hii pia kwa uchungu huu, Mwalimu Nyerere alisema: "Wakubwa walishasema, hakuna hakuna! Unahamisha mali kutoka kwa maskini unapeleka kwa tajiri! Hii ni *uncultured, uncooth."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa hii muhimu aendelee kuitumia. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Kangi Lugola amekupa taarifa hiyo. Sasa sijui unaipokea au unaikataa?

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nalisema hili kwamba naomba tufanye mageuzi. Hatuwezi kuogopa kwa sababu tunajinyima. Hapa tumeweka mpaka shilingi 200 kwenye mafuta, ambayo ina-*effect* kwa mnunuaji wa mwisho. Lakini tumeamua kujinyima ili tupate fedha, tujenge barabara kwa pesa zetu. Kwa hiyo, ningeomba tupate barabara, lakini na ile pesa ibaki kwenye uchumi wa nchi yetu. Ukienda Dubai wanafanya, Malaysia wanafanya, Singapore wanafanya, sisi hatutakuwa wapya. Lakini kama Mchina atatuletea msaada, atuletee fedha, akatupa sharti ajenge Mchina, hewala wafanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Wakorea wametupa pesa za kujenga daraja la Malagarasi, *condition* ni kwamba *contractor* lazima atoke Korea. Maana yake ni moja tu. Nyie si mnataka daraja? Lakini tunataka hii hela irudi kwenye uchumi wetu. Nawaombeni sana, Waziri wa Fedha, hili tulisimamie na ndio namna ya ku-*manage* uchumi wa nchi.

Leo tunapiga kelele shilingi yetu inaanguka, ni kwa sababu ya suala la *demand* na *supply*. *Demand* na *supply* kwa sababu inabidi utumie shilingi kununua dola, ili uweze kulipa huko unakotaka kuagiza. Sasa inabidi tuchukue shilingi zetu, tununue dola kumlipa Mkandarasi ambaye anajenga kwa pesa za Tanzania. Naomba sana hili tulifanyie kazi kwa kiasi kikubwa na litatusaidia sana katika kuboresha uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niongee kidogo kuhusu Mpango wetu huu wa Uchumi wa Miaka mitano. Ukiusoma ule Mpango wote, unasema unataka kukuza uchumi wa nchi, *it's about growth!* Lakini ili tuweze kuwa na *growth*, lazima ku-*attract investiments* na tuweze kufanya biashara. Lakini ili *investor* wa ndani na wa nje waweze kuja na wawe na *confidence* ya kufanya biashara na sisi, lazima kuwe na *price stability*. Kama *price* ni *volatile,* yaani *price* haziko *stable,* ni ngumu sana kupata *serious investors* kwa maana ya wa ndani na wa nje.

Kwa hiyo, mimi naishukuru Serikali, kwa kuamua kufanya *agruculture* na *energy* na miundombinu, kuwa *top priority* katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Lakini ninachotaka kuomba sasa Serikali, ili hizi *infrastructure* mnazotaka kujenga lazima ziende kwenye *purpose,* ziunganishe biashara. Kwamba, tunajenga bandari hii ili iweze ku-*facilitate trade* ya ndani, *trade* ya nje, na tukifanya hivyo tutakwenda kwa kasi kubwa zaidi. Naamini haya yataweza kutokea kwa sababu, tumejipanga vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la *inter-connection* kwenye simu hizi za mkononi. Niombe sana Waziri atakapokuja, umefika wakati, ni sisi tu Tanzania unakuta mtu anatembea na simu tatu au nne. Tunawapa gharama watumiaji wa mwisho. Ukiziondoa zile *inter-connection* kwenye makampuni ya simu, hakuna atakayebeba simu nne. Tutayafanya sasa makampuni ya simu wa-*compete* kwa kuweka mtandao mbali zaidi ili aweze kupata watu, wa-*compete* kwa maana ya *quality* ya *service* wanazotoa, lakini wasi-*compete* kwa sababu ya *price* peke yake.

Kwa hiyo, naomba sana, hili linahitaji *serious intervation* kama Serikali, kwamba tuamue sasa hakuna *inter-connection.* Kwa bahati njema, wameshakuja wamekaa muda mrefu, wamesha-*stabilise,* ukiiondoa bado wataendelea kufanya biashara. Lakini tutakuwa tumewasidia watu wengi masikini, hakuna atakayeweza kubeba simu nne au tano. Kwa sababu hizi simu nne au tano, maana yake tunapunguza *disposable income* ya mtu mmoja mmoja. Ili ile *disposable* ya mtu tukishai-*save* kama nchi kwa Sera zetu, itasaidia kwenda kwenye uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, bajeti ni nzuri, lakini inahitaji usimamizi. Narudia tena, nataka tufanye mabadiliko kwenye *Finance Act.* Ni mageuzi makubwa haya na kwenye Sheria ya *CAG,* ili tuanze kuwafanya Makatibu Wakuu wawe *responsible*, maana wao ndio ma-*CEO.* Kila mwaka sasa utakuwa unajua kila senti ya nchi hii imefanya kazi gani. Kama imefanya kazi ambayo sisi hatukuihitaji, yule mtu tutakuwa tumeweka utaratibu achukuliwe hatua za kisheria. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kuendelea kwa kasi kubwa zaidi, kuliko tunavyoendelea sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja ya bajeti. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwenye bajeti hii ya Fedha. Bajeti ni nzuri, ina matumaini, lakini kubwa zaidi ambalo nimeliona ni namna ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetoka tu ziarani Jimboni. Nimeanza tarehe 22 nimemaliza tarehe 07 mwezi huu. Moja katika masuala makubwa yaliyojitokeza ni suala zima la kilimo, kwa maana kwamba wananchi, wakulima wa Jimbo la Solwa, wanahitaji sasa wapate vifaa kwa maana ya vifaa vya kilimo. Kwa bahati mbaya sana, katika Mkoa wetu wa Shinyanga, tunapokuwa tunapata adha ya msimu ambao unakataa kwa maana ya kilimo, basi hali ile inageuka inakuwa ni hali mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nafuatilia sana suala zima la umwagiliaji, tuweze kuwa na kilimo cha umwagiliaji kwenye Jimbo la Solwa ili tuweze kuondokana na tatizo zima la kutopata mazao ya chakula.

Tunaishukuru sana Serikali, imelisikia hilo na hata hivi sasa kuna hawa watu wa Kanda ya Ziwa, wamekuja pale Jimbo la Solwa, Lipitwe, Namkande, pamoja na Kata ya Makeyo, kuona kwamba sasa waibue namna gani waweze kufanya upembuzi yakinifu ili sasa tuingie kwenye suala zima la kilimo cha umwagiliaji. Lakini katika huu Mpango wa Maendeleo ya Uchumi, moja katika *point* kubwa sana ili hasa kuondoa *gap* ya walionacho na wasiokuwanacho, kwanza ni kuwasaidia wakulima kwa sababu, ndio wengi wanaoishi vijijini, asilimia kubwa sana ni wakulima. Sasa tunawasaidia vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejenga mazingira mazuri. *TIB* pale watakuwa na pesa nzuri tu, dirisha la kilimo, shilingi bilioni 100 kila mwaka, ina maana ndani ya miaka minne au mitano tutakuwa na shilingi bilioni 500. Wanafaidika vipi wakulima wetu? Nimeongea sana hili, Jimbo la Solwa hawaelewi hata namna ambavyo huu utaratibu wa Serikali unavyotaka kuwasaidia wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, kwanza kabisa iwaandae wakulima waweze kukopesheka. Ni masuala magumu sana. *The only way* ambayo ukienda pale *TIB*, kwa urahisi zaidi ni kupitia *SACCOS*, sawa! Suala zima la *SACCOS* hilo tunaendeleanalo, lakini kwa maana ya wananchi 420,000 wa Jimbo la Solwa, wakulima ukiwatoa tu elfu fulani hivi, sio rahisi wote waingine kwenye *SACCOS*. Kuna haja ya Serikali kubadili mfumo wa kuwawezesha wakulima kwa mfumo mwingine utakaowezekana waweze kukopesheka vizuri kupitia vikundi vya wakulima. Kuna Halmashauri zetu, lazima Serikali i-*take risk, the high the risk the high the profit*, na hapo ndipo tutawawezesha hawa wakulima waweze kujikomboa kwenye suala zima la kilimo na waweze kupata fedha. Kinyume na hapo tutakuwa tunaimba tu hapa na Mpango huu utabaki tu juu ya meza na wakulima watabaki hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi shilingi bilioni tano ukienda vizuri baada ya miaka mitano kama hatutakuwa *serious* kuwasaidia wakulima, zitakwenda kwa wakulima wenye uzoefu mzuri, wenye ofisi zao, wana vifaa vikubwa, wanajua namna ya kuomba mikopo, wana uwezo mzuri sana wa kukopesheka, na benki ndiyo wanavyotaka. Huwezi kuilaumu *TIB,* huwezi kuilaumu hata kidogo kwa sababu wao, wamepewa jukumu la kusimamia fedha hizi. Sasa Serikali isiposema kwamba tunataka hizi fedha ziende kwa wakulima wadogo wadogo kula vijijini, kwa maana kwamba lazima i-*take risk* ambayo dhamana hata kama kikundi, iwe dhamana tu. Kwa sababu wale wananchi watakwenda wapi? Tanzania ni hii hii, watakwenda Rwanda au watakwenda Burundi? Hawawezi, wako humu humu. Kama ni kuwakamata, sheria zipo, kama ni sheria walete hapa tubadilishe ili waweze kukopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hati za mila na zenyewe pia masharti yake ni kwamba hawezi kuuza. Ina maana huwezi kuiuza ile hati. Sasa taasisi za fedha zikishasoma ile, haiwezi hata siku moja ikadhamini kwa maana iko *against* hati ya mila. Ndio maana hata hii hati ya mila kuna umuhimu wa Serikali kuiboresha na mfumo mzima wa kuwakopesha wakulima. Naishauri Serikali ifikirie mara mbili mbili kuwasaidia wakulima. Shilingi bilioni 141 zilizotolewa kwa ajili ya kupima viwanja na mashamba kwa wakulima, naomba Serikali iongeze fedha hizo. Bajeti hii sawa, tutapitisha, lakini naomba bajeti ya mwakani izingatie sana. Wananchi waweze kuwa *security,* waweze kupata hati. Kuna wakulima wanaweza wakachukua mkopo mmoja mmoja, badala ya kuwa na vikundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na suala la ya maji, katika Jimbo la Solwa, hakuna Kata niliyopita katika ziara yangu nisiambiwe tatizo la njaa. Ndiyo maana nimeongelea sana suala la umwagiliaji. Mimi nikitengenezewa miundombinu ya umwagiliaji, tukapewa mikopo vizuri kwa wakulima, nadhani hata tatizo hili, hatupendi kuomba omba, wala hakuna mtu anapenda kuomba chakula hata kama ni Serikali yake ina jukumu la kufanya hivyo. Suala la njaa kwenye Jimbo la Solwa, ni kubwa sana. *It's an emergency case,* naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alichukue hilo.

Suala la njaa kwenye Jimbo la Solwa ni kubwa sana narudia tena, suala la njaa kwenye Jimbo la Solwa ni kubwa sana. Nilipita kwenye ziara kwenye Kijiji cha Idaza pale Kata ya Mamala, kuna mzee mmoja anaitwa Mathias, tunaongea miradi na namna ambavyo tumejipanga katika utekezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi. Yule mzee aliinuka akaniambia, Mheshimiwa Mbunge ilani ni nzuri na katika miaka mitano utakayofanya kazi tuna matarajio mikubwa mno. Miaka mitano ijayo utafanya mengi zaidi ambayo yatatufurahisha. Lakini ladha ya maendeleo haya sasa hivi hatuyaoni kwa sababu tuna njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu naiomba Serikali ifanye haraka, tathmini iliyokwenda kufanya na tukapata chakula, Jimbo la Solwa limepata tani 864, ni kidogo mno kulinganisha na tathmini iliyofanywa mwaka 2006. Sasa hivi mwaka 2006 tulipata tani 5,200 ambayo angalau iliweza kutosha na kwa bahati nzuri kwa wakati ule mvua ikanyesha, wote wakulima wakapata mazao, suala likaisha. Sasa hivi hata mvua haipo, mazao waliyolima hawakuvuna, wamevuna kwa kiwango kidogo ambacho

hakiridhishi. Ni *serious case!* Naomba Serikali ilichukue hili. Kama mimi ushauri wangu, Serikali ichukue tathmini ya mwaka 2006, ile ile wagawe chakula ili wananchi wa Jimbo la Solwa sasa waweze kuondokana na suala la njaa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba ulichukue hili *seriousness,* naongea mara mbili, mwananchi wa Solwa akifa, mimi sasa nitakuwa nimeshawakilisha kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Victoria kuna awamu ya pili. Kuna huu mradi wa ziwa Victoria ambao unapitia Tinde kwenda Nzega. Wananchi wanapenda kujua mradi huu unakamilika lini? Naomba Wizara husika iweze kutoa ufafanuzi mzuri zaidi ili watu wawe na matumaini ya maji. Kata ya Tinde ni mji mkubwa, sasa hivi una lami na umeme. Didia vilevile ni mji mkubwa, kuna umeme, yaani watu wengi sana. Kuna miradi hii ya *World Bank* imekuwa inakwenda, tunashukuru sana misaada hii, lakini naomba Serikali ijaribu kushinikiza *World Bank* watuletee fedha zote kwa pamoja tuondokane na adha ya maji.

Kwenye Halmashauri yetu pale tumejipanga ndani ya miaka mitano tuondoe kabisa tatizo la maji kwenye Jimbo la Solwa. Mpango huo unawezekana. Moja katika mipango hiyo, ni pamoja na hizi, na kuna hii miradi ya vijiji ambavyo viko ndani ya kilomita 12 kwenye bomba la Ziwa Victoria na yenyewe itatekelezwa mwaka huu.

Naiomba Serikali kwa namna yoyote ile tuondokane na adha, kwa sababu *capacity* ya matumizi ya maji ya lile ziwa Victoria ni ndogo mno ukilinganisha na matumizi wanayotumia sasa hivi. Lakini tukipanua wigo, kwanza hata Kashiwasa wenyewe watapata mapato mazuri na malengo hasa ya kuondoa adha ya maji kwenye vijiji vyetu itakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Solwa, tunajenga hospitali ya Wilaya, na naamini Wilaya nyingi sana zinajenga hospitali ya Wilaya, lakini ukiachia Halmashauri kama Halmashauri ni suala zito mno. Sisi tumejipanga vizuri tu, lakini kuna fedha za ruzuku shilingi bilioni 1.4, tulizopata ni shilingi milioni 500 tu na tunasubiria shilingi milioni 900 ambayo mpaka sasa hivi hazijaja kwenye Halmashauri yetu na ndani ya milioni 900 ile tulitenga milioni 200 kwa ajili ya kuendeleza jengo la hospitali ya Wilaya. Lakini namna ninavyoiona hospitali ya Wilaya, nzito mno. Naiomba Serikali, hospitali zetu za Wilaya nchini ikiwemo hospitali ya Jimbo la Solwa iichukue moja kwa moja badala ya kutuachia sisi. Sisi tutabaki na zahanati na vituo vya afya tuko tayari kusimamia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda, ajira kubwa kupanua wigo wa ajira ni kuwa na viwanda vingi na makampuni mengi. Lakini Serikali inajitahidi sana kupitia mifumo yetu ya *IPZ,* kupitia *TIC* lakini kupanua wigo wa viwanda ni muhimu sana tukapanua wigo wa viwanda kwenye Mikoa ambayo inahitaji sasa viwanda hivyo ili *raw material* kwa maana ya malighafi ni yale yale au mazao ya wakulima wanaolima kwa ajili ya biashara tutakuwa tumepiga *impact* nzuri sana kuwasaidia wakulima katika Mkoa wa Shinyanga. Mkoa wa Shinyanga tunalima sana pamba, hatuna viwanda, tunalima sana

dengu, hatuna hili, tuna ng'ombe nyingi sana hatuna viwanda vya nyama, naiomba sana Serikali ilitizame hili kwa undani zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti inavyokuja hapa tunaongeza mapato katika vinywaji tu lakini kuna maeneo mengi ya kuongeza mapato ya Serikali. Moja katika sehemu kubwa sana Mungu aliyotupa zawadi ya jiografia ya nchi yetu lakini tunaichezea ni bandari. Ucheleweshaji na urasimu unavyo-*lodge document* pale siku tano, inaingia kwenye *evaluation* siku nne, ukiingia kwa ajili ya kupata *order scanner, order* ya kutoa mzigo siku nne, ndani ya *scanner* pale kuna Afisa *TRA* anaweza aka-*up lift* tu ikienda *ICD* kuna Afisa wa *TRA* anaweza aka- *up lift* anavyojisikia tu kama ni *TPA*, au *ICD*, kwa hiyo ina maana maamuzi ya mzigo ama zile *bureaucracy* kuanzia mwanzo mpaka mwisho ni siku 18. Mimi nimezihesabu, ukitoka hapa sasa unapata *release* ya kutoa mzigo wako unavyokwenda sasa kutoa mzigo na yenyewe siku kumi. Unamkuta mtu kule naye ana-*up lift* anavyojisikia yeye.

Sasa namwomba Waziri wa Fedha suala la *bureaucracy* kwenye bandari ifanyike ndani ya siku moja. Hivi kwanini *valuation* ifanyike na watu wanne, watano? Ina maana wale hawajiamini? Halafu kibaya zaidi, kuna hii *fast team* nje, unatoa mzigo *fast team* inakukamata inakwambia lazima tufungue huo mzigo, wanafungua tena mzigo unakuja kujikuta wanakagua tena mara nyingine. Ina maana wale waliokukagua kule walio-*value* ule mzigo *TRA* hawafai, hao ndiyo wanafaa! Tubadilishe mfumo, tuondoe urasimu, mzigo utoke ndani ya siku tatu kama wenzetu Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti Tanzania tuna bandari Tanga, Dar es Salaam na Mtwara lakini tunashindwa na bandari ya Mombasa. Hivi wale ni binadamu sisi siyo binadamu? Wana nini cha kutuzidi sisi? Tuna umuhimu sasa wa kujipanga mzigo utoke ndani ya siku ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ICD* nafasi ndogo, *rate* za mzigo zinatofautiana, unaweza kuwa na kontena hapo kulipa *park charge* kwa *ICD*, huyu ataku-*charge* 1,000, huyu ataku-*charge* 4,000 yaani hovyo hovyo tu, yaani hakuna vitu ambavyo unaona kabisa hapa tumejipanga kwa namna ya kutoa mzigo haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ICD* sasa imekuwa biashara, mtu mwenye eneo kubwa tu akienda pale anapewa. Sasa ni vurugu na sababu kubwa ya kuboresha bandari zetu ni namna ya kupunguza urasimu, ndiyo maana mimi natoa ushauri na nazidi kutoa ushauri kwamba bado Serikali ifikirie bandari iwe kama bandari, iwe na Wizara yake kama bandari. Ondoa hii reli, reli ni muhimu sana kama gari, ondoa hii bandari ni kitu kikubwa sana inaweza ikatuingizia fedha nyingi sana tukaziba hii nafasi ambayo inategemea *donors,* ni mabilioni ya pesa! Mizigo ya *transit (transit goods)*, hizo ni *direct income* tunawapoteza watu wanakwenda Mombasa, wanakwenda wapi, mtu anakuja anatoa mzigo wake anakuachia mzigo wake pale, unamsumbua hata *transit* unamsumbua! Nini hasa unachomsumbua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri sana liwe ni suala nyeti na lenyewe ambalo linaweza likatusaidia kwenye mapato ya nchi yetu, ambalo linaweza kuwasaidia

wafanyabiashara wa ndani ya nchi pamoja na wawekezaji kwa kuona kwamba sasa Tanzania tumejipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD YUSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nichukue fursa hii kuwashukuru wa kuwapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Kikwajuni kwa ushirikiano wao mkubwa sana ambao umepelekea tupige hatua kubwa wa maendeleo kwa kipindi kifupi sana. Katika kipindi cha miezi sita tumefanya kazi kubwa sana hasa katika sekta ya maji, kwa hiyo wananchi wote nikianzia Kilimani East, Miembeni, Kikwajuni juu, Kikwajuni Bondeni, Kisima Jongoo wanawashukuruni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kusema ni bajeti sahihi ambayo imekuja kwa wakati muafaka, ni bajeti ambayo inakidhi kabisa mahitaji ya Mtanzania wa karne hii tuliyokuwa nayo. Ukiangalia, bajeti hii ina mambo mengi sana, siwezi nikayazungumzia yote, muda ni mfupi, lakini bajeti hii ina mwelekeo wa kupunguza utegemezi kutoka katika vyanzo vyetu vya nje ama kutegemea wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tulimaliza kujadili mpango ambapo mpango huu ulikuwa unalenga kuhakikisha kwamba unapofikia miaka mitano inayokuja tuweze kutumia asilimia kumi tu ya bajeti yetu kutoka vyanzo vya nje. Lakini leo hii tunazungumzia asilimia 17, siyo jambo bayana kulinganisha na asilimia 28 miaka minne iliyopita. Kwa hiyo, ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo linguine, bajeti yetu hii inatoa mkazo katika kuangalia jinsi gani tunatumia mapato yetu yasiyo na kodi. Mapato kupitia katika Idara, Wizara na sekta mbalimbali zitakuwa zikitoa mchango mkubwa sana, nafikiri ni jambo jema sana. Lakini pia hata mapato ambayo ni ya kodi, naomba nipongeze sana juhudi hizi ambazo zimeainishwa katika bajeti za kuhakikisha kwamba tumeibua vyanzo vipya vya mapato, tumedhibiti matumizi ya Serikali, kwa hiyo, niseme kwa ujumla bajeti nzuri naiunga mkono. Lakini watu wengi wamezungumza suala zima la utekelezaji wa haya malengo ambayo yameainishwa katika bajeti yetu. Ni jambo la msingi kwamba sasa kinachotakiwa ni usimamizi na utekelezaji makini kabisa. Lakini pia pale ambapo inabidi, basi anayezembea awajibishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni muhimu sana. Kwa bahati mbaya sana katika nchi yetu, baadhi ya watu pale ambapo mtu anasimamia misingi ya utekelezaji wa majukumu yake, hakubali kuyumba katika mambo ya msingi, ndipo anapopigwa vita kwa sababu ya kukinzana na maslahi binafsi ya watu. Kwa hiyo, nafikiri tuweke maslahi ya Taifa letu mbele ili tuweze kuhakikisha kwamba tunafikia malengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine muhimu ni vipaumbele. Mimi vipaumbele vimenigusa kweli kweli! Bajeti ina vipaumbele vitano, na ni vipaumbele vya msingi sana. Ingekuwa mimi kama naulizwa kabla bajeti hii haijatayarishwa ni kipaumbele gani kiwemo katika bajeti yetu hii, mimi ningesema umeme. Lakini ningerudia hivyo hivyo mara tano kusema umeme, umeme, umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba leo niseme jambo moja la msingi sana. Kwa kuwa nimesimama hapa nikiwa na faraja kubwa sana kwamba mtazamo ambao niliokuwa nao wa jinsi gani suala la umeme lilivyokuwa na umuhimu wake katika Taifa letu ndiyo ambavyo bajeti hii imeliona kwa sababu vipaumbele vyote vitano ikianzia kipaumbele cha ajira, ambazo zimetokana katika sekta mbalimbali ikiwemo viwanda, umeme, miundombinu, moja kati ya kipaumbele cha bajeti hii inategemea umeme. Kilimo chenye tija, kinategemea umeme pamoja na maji vilevile yanategemea umeme. Kwa hiyo, niseme kwamba bajeti hii nzuri na vipaumbele vyake ni ni muhimu sana kwa changamoto zinazotukabili sasa hivi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bajeti hii, sote tutakumbuka kwamba itakuwa inatekelezwa kama ni katika kipindi cha mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa mipango. Mpango ambao tumeupitisha juzi wa miaka mitano, unalenga katika kuratibu na kuongoza dira yetu ya miaka 25 ya maendeleo ya Taifa letu, dira ambayo inadhamiria kufanya nchi yetu iwe na uchumi wa kiwango cha kati, *medium class economy*. Lakini katika dira hii, kuna mambo mawili ya msingi sana, moja ni kuhakikisha kwamba tunaondoa umaskini katika nchi yetu ama tumepunguza. Lakini pili ni kuhakikisha kwamba maisha yanakuwa ni bora zaidi kwa wananchi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siku zote tunajadiliana hapa kwamba jinsi gani ukuaji huu mzuri wa uchumi wa nchi yetu haugusi moja kwa moja kwenye kiwango ambacho tunahitajia maisha ya Mtanzania wa kawaida, ni kwa sababu ya Sekta ya Kilimo kwamba bado haijakuwa katika kiwango ambacho kinastahili. Sekta ya Kilimo ambayo sote tunajua mchango wake mkubwa sana katika ajira, leo hii sekta ya kilimo inakua kwa wastani wa asilimia 4.2, lakini hata sekta ya viwanda ambayo ingetoa ajira kubwa sana kwa nchi yetu inakua kwa wastani ya asilimia 7.9 tofauti na sekta nyingine kama mawasiliano. Mawasiliano sasa yanakuwa kwa asilimia 22.1.

Kwa hali hii hatutoki, na hizi ni takwimu za mwaka 2010, ni lazima kilimo sasa hivi kama ilivyo kawaida yetu tuendelee kukipa mtazamo wa kipekee. Kwa hiyo, *role* ya kilimo ni kubwa sana katika uchumi wa nchi yetu, siyo tu kwamba kinaweza kuunganisha kilimo cha biashara na wakulima wadogo wadogo kupitia zile *programs* wanaita *outgrow schemes*, lakini pia kilimo kinaweza kufungamanisha vizuri kati ya viwanda na kikaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa sana katika ajira na hatimaye kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachina wana *principle* moja ambayo waliirithi kwa mwasisi wa nchi yao *Chairman Mouth Sechoum.* Wakati ule mwaka 1957 Wachina walikuwa zaidi ya asilimia 80 ya ajira inayotegemea kilimo kama ilivyokuwa sisi sasa hivi. Lakini *principle* labda niinukuu kwa Kiingereza, anasema *taking agriculture as a foundation and industry as leading factor*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa kweli tuna dhamira ya kweli ya kuota ndoto hii ya kwamba viwanda viwe *leading factor* katika nchi yetu kwa miaka inayokuja, lazima suala la umeme lipewe mtazamo wa kipekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari ya ukosekanaji wa umeme katika nchi yetu kwa sekta zote ikiwemo viwanda ni kubwa sana. Mwaka 2010 mchango wa uchumi kutokana na sekta ya viwanda imepoteza wastani wa shilingi bilioni 7.7, lakini kuna kodi ambayo ilikuwa ikusanywe kupitia viwanda karibu bilioni nukta tatu, zimepotea na ajira milioni elfu saba sijui mia nne na ngapi, zimepotea. Hii ni athari inayotokana na mgao wa umeme katika Taifa letu. Kwa hiyo, niipongeze sana Bajeti kwa kulitambua hili kwa sababu bajeti hii imeongeza katika Sekta ya Viwanda kwa asilimia 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mingi! Naona muda unakwenda! Mfano, miradi ya *megawatt 160*, miradi ya *megawatt 300* pale *Mnazi Bay* na kuna miradi pia ya *transmission and distribution* ndiyo unaitwa *back bone* wa Iringa, eidha mpaka kule Shinyanga. Lakini kuna programu nyingine ziko kwenye *MCC* na kadhalika. Kwa hiyo, ni jambo ambalo linatia moyo. Kwa hiyo, mipango hii siyo ya kubeza, lakini lazima nikiri kwanza kwamba changamoto bado ni kubwa sana.

Changamoto ni kubwa sana na changamoto hii naweza kusema kwamba imetokana na mambo mawili makubwa ya msingi. Kwanza, muundo mzima wa sekta yote ya nishati haukidhi matakwa ya sasa hivi, lakini pia eneo la miundombinu kwa upande wa uzalishaji, usambazaji na ugawaji nalo pia lina changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, suluhisho ninalotaka kulipendekeza hapa kwamba sasa hivi kuna mambo mawili ambayo lazima tuyaangalie. Jambo la kwanza ni kuhakikisha kwamba tunatanua, tunachanganya vyanzo vya uzalishaji umeme ,wanasema *diversification of resources of energy resources*.

Lakini la pili, ni suala zima la uwekezaji kuweka nguvu katika kuwekeza kwenye miradi ya kuzalisha umeme. Nchi yetu ina raslimali nyingi sana katika nchi yetu tukianzia gesi, makaa ya mawe, *hydro potential* ni kubwa sana. Gesi peke yake ni zaidi ya *million cubic fit 800* ambazo zipo sasa hivi. Lakini tuna mradi mkubwa sana wa kutoa gesi Mtwara kupeleka kule Tanga. Nashangaa sana kwamba kwa nini tusingetumia fursa hii pengine kuangalia uwezekano wa kuweka *sub marine pipe line* kwenda Zanzibar pia ili gesi ile iweze kutumika Zanzibar na iweze kubadilisha sana hali ya uchumi wa Zanzibar. Lakini pia wakati tunazungumza mgao wa umeme ambao tunakosa *reserve margin* kabisa kipindi hiki ambacho Zanzibar inatumia *megawatt 48* tungeweza kabisa kuweka gesi pale Zanzibar ambayo ikazalisha umeme wa *megawatt 48* na hizi *megawatt 48* zikasaidia kupunguza hali ya makali ya mgawo huku Tanzania Bara. Kwa hiyo, suala la kutumia vyanzo vyetu hivi ni la msingi sana.

Lakini pia nimezungumza suala la *investment*. Suala la uwekezaji lazima ifike wakati sasa tuwe na mfuko maalum wa umeme. Kuna miradi mingi sana ambayo iko katika mipango na mipango ni mizuri tu na mimi naomba niwapongeze Wizara pamoja na *TANESCO*. Lakini hatuwezi kuwa na miradi ambayo hakuna fedha za kuwekeza katika miradi hii. Mfano Uganda, wakati ule walipokuwa wanataka kuzalisha umeme kwa kutumia *project* ya Bujagali walipata vikwazo vikubwa sana. Walishindwa kuzalisha kwa kutumia fedha za wahisani, lakini walitoa maamuzi magumu wakasema tuandae mfuko wa nchi na fedha zinaingizwa pale na mradi ule ukakamilisha.

Sasa hivi wametumia *mode* hiyo hiyo kuwa Mfuko wa Nishati Uganda ambao ndiyo unasaidia sasa ku-*develop* hata *hydropower project* nyingine. Sasa mimi nafikiri tukitumia *mode* hii ya Uganda ya kuwa na mfuko wa nishati ambao utaweza kutekeleza vyanzo mbalimbali, mfano tuna kodi ya Sh. 200/= kutoka katika mfuko wa barabara za *TANROAD*, tunaweza tukasema tuongeze Sh. 250/= tu au 20% ya zile Sh. 200/= zikaingia katika mfuko huu. Kuna *VAT* ambayo inalipwa kwenye mafuta na kadhalika. Mambo haya yote yangesaidia sana katika kukabiliana na changamoto ya umeme. *Project* tunazo nyingi sana kama vile *project* ya *Hydropower Stigler's Gorge*, hii ni moja katika miradi ambayo ingeweza kufaidika na utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia suala lingine la kuangalia, tunatumia fursa kijiografia iliyopo ndani ya nchi yetu kwamba sasa nchi hii imeungana na nchi ambazo ni za *Southern African Power Pool* upande wa Kusini kupitia Zambia, lakini *East African Power Pool* kwa upande wa Kaskazini kupitia Nairobi. Kwa hiyo, tunapo-*strengthen* hizi *transmission* ambayo ni haki yetu kwa maana hii kutokea Iringa - Uganda na huku Mbeya mpaka kwenda Zambia ika–*connect* mpaka Arusha kupitia Singida, nafikiri itakuwa ni fursa nzuri sana ya kutumia soko hili la Afrika Kusini na Afrika Mashariki, inaweza kusaidia ku-*develop resources* zetu vizuri ili ziweze kuwa na tija na tuondokane na tatizo la umeme na hatimaye kuendeleza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge kwa mchango mzuri. Sasa namwita Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa John Mnyika na baadaye Mheshimiwa Ester Bulaya ajiandae.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya bajeti ya Waziri wa Fedha aliyoiwasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama kwa mara nyingine katika Bunge hili na kuweza kutoa mchango wa mawazo kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Mchinga katika Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa hotuba yake safi na makini ambayo ninaamini kwa dhati kabisa kwamba inalenga kumkomboa Mtanzania wa chini au mnyonge kutoka katika lindi la umaskini na kumpeleka katika eneo ambalo tunaamini litasaidia kuboresha maisha yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza bajeti hii kwa sababu yako maeneo ambayo ninadhani yakifanyiwa kazi kama ambavyo bajeti imesomwa, yanaweza kutusaidia sana katika kupunguza ukali wa maisha na kutuondoa hapa tulipo na kutupeleka mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ukurasa wa 5 - 8 wa bajeti, inaeleza wazi mikakati ambayo inalenga kupunguza ukali wa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaje tu baadhi ya mambo ambayo nimeyaona hapa, endapo yatafanyiwa kazi na yatatekelezwa kama yalivyoahidiwa yanaweza kufikia lengo.

Kwanza, ni kuondoa tozo katika mafuta, tumeshazungumza sana. Lakini ningependa kufahamu kutoka kwa Waziri wa Fedha baadaye wakati wa majumuisho kwamba hizi tozo mbalimbali zikiondolewa ni kwa namna gani sasa bei ya mafuta itapungua au kwa kiwango gani kwa wastani wa makadirio? Ni kwa kiwango gani bei ya mafuta itapungua ili kuweza kuleta tija kwa mwananchi huyu ambaye tunamzungumzia, yaani Mtanzana mnyonge na maskini?

Eneo lingine ni la kupunguza bei ya bidhaa, kuimarisha hifadhi ya chakula lakini pia 6% ya *skills development levy* ambayo tumekubaliana kwamba tuipeleke kwa wenzetu wa Bodi ya Mikopo kwa kiwango cha 4% na kiwango cha 2% kwenda *VETA*. Mimi ninaiunga mkono sana hoja hii kwa sababu endapo tutafanya hivyo kupeleka 4% Bodi ya Mikopo, tatizo kubwa la vijana katika Vyuo Vikuu linaweza kupungua kwa sababu Bodi itakuwa na uwezo wa kuimarisha mfuko wake. Lakini pia suala la 2% kwa *VETA*, tukilitekeleza ninaamini kabisa vijana wengi wataweza kujiajiri kwa sababu *VETA* itakuwa imewezeshwa, kwani inachukua asilimia kubwa ya vijana ambao tumekuwa tukizungumza hapa tangu jana kwamba vijana ni kundi kubwa ambalo halina ajira. Kwa hiyo, kuwaongezea hii ruzuku kwa 2% itachangia sana katika kuondoa matatizo yaliyopo. *(Makofi)*

Mwisho, ni vipaumbele vilivyowekwa, yaani miundombinu, maji, nishati, jilimo na elimu ambavyo ninaunga mkono kwa asilimia mia moja. Ninaamini kupitia bajeti hii sasa hata kipande kile cha kilomita 60 kati ya Ndundu - Somanga kuelekea Lindi – Mtwara kitakamilika kwa sababu kipaumbele cha kwanza hapa ni miundombinu. Hatuwezi kuinua uchumi katika Taifa hili kwa kuacha baadhi ya maeneo ya Mikoa yakiwa nyuma kwa sababu ya uchakavu wa miundombinu. Kwa hiyo, ninaunga mkono sana vipaumbele hivi vilivyotajwa na ninaamini Waziri wa Ujenzi katika hotuba yake ataonyesha waziwazi fungu la kumalizia kilomita 60 kati ya Ndundu – Somanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie katika bajeti yenyewe. Mimi nina maeneo machache ambayo ninadhani niyapitie. Eneo la kwanza ni mpango wa kuongeza mapato ya ndani ya Taifa katika ukurasa wa 18 wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa huo huo Mheshimiwa Waziri ameeleza mikakati mbalimbali ambayo inalenga kuongeza mapato ya ndani. Ametaja eneo la kuboresha hoteli za kitalii ili ziwe na hadhi ya kimataifa ili ziweze kuliingizia Taifa hili mapato makubwa na hilo siyo jambo geni, ni jambo ambalo liko katika ukurasa wa 129 wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, ninamuunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wito wangu au maoni yangu ni kwamba ipo haja badala ya kufikiria zile hoteli ambazo zimejengwa na kuiingizia mapato Serikali, iko haja ya kupanua wigo kwa kutafuta vyanzo vingine vya kiutalii vinavyoweza kuiingizia mapato Taifa hili na miongoni mwa maeneo muhimu ambayo tunaweza kuwekeza kwa kiasi kikubwa na tukanufaika ni kufungua ukanda wa Lindi – Mtwara kiutalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu hata ukisoma Ilani au bajeti, mikakati ya Wizara ya Maliasili imekuwa ni kupitia vyanzo vilevile vya kiutalii mwaka hadi mwaka. Lakini hakuna mikakati mikubwa ya kujikita namna gani tunaweza kufungua maeneo mengine mapya ya kiutalii ili yaweze kuliingizia Taifa hili mapato Taifa letu?

Mimi natoa wito kwa Wizara na Serikali kuona haja ya kufungua ukanda wa kusini, yaani Mkoa wa Lindi na Mtwara ambao utachangia kwa kiasi kikubwa kuiingizia mapato Serikali kupitia ufukwe bora kabisa *along the East African Coast,* yaani ufukwe kutoka Mchinga, Kijiweni, Ruvu mpaka Lindi Mjini. Tunao ufukwe mzuri sana, yaani *Sand Beach.* Endapo utatumiwa huu kwa uwekezaji mkubwa unaweza kutusaidia katika kuongeza vyanzo vingine vya mapato kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia eneo lingine ni lile la kuanzisha utafiti na hatimaye uchimbaji wa masalia ya mjuzi mkubwa Dinosaur katika eneo la Tendeguru katika Jimbo la Mchinga. Kwa sababu eneo hili ni muhimu sana, Serikali ya Ujerumani imekuwa ikiingiza mapato mengi kila mwaka kupitia Dinosaur ambaye amevumbuliwa pale Tendeguru katika Jimbo langu la Uchaguzi la Mchinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Maige analifahamu hili, kwani tumekuwa tukipigizana kelele mara kwa mara na ninaamini katika bajeti yake atasema ni kwa kiwango gani mjusi yule anainufaisha Serikali ya Ujerumani na kwa nini sasa tusifikirie kama ambavyo wenzetu Wajerumani walivyotuomba kwamba tufanye utafiti kuvumbua masalia mengine pale ili tuyaweke katika makumbusho ya Taifa. Lakini pia endapo tutafungua ukanda huo, itatusaidia sana kuboresha huduma za miundombinu ya maji, umeme na barabara kutoka Mkwajuni kwenda Mipingo hadi Matapwa ambako ndiko asili ya mjusi huyu iliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiachana na suala hilo la utalii, eneo lingine ambalo limejadiliwa katika bajeti hii ni eneo la kuongeza ajira katika ukurasa wa 11 wa kitabu cha Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hatua mbalimbali ambazo zinachukuliwa na Serikali katika kuongeza ajira, kwa sababu tunafahamu ajira sasa ndiyo tatizo kubwa na Ilani ya Uchaguzi imesema, ni lazima tuweke mkakati wa vijana kujiajiri au kujenga mazingira ya kuajiriwa. Kwa hiyo, ninaunga mkono sana eneo hili la ajira. Nina imani kabisa tukitilia mkazo jambo hili, litatupeleka mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nia yangu ni kuzungumzia Mpango wa Serikali wa kutekeleza ule Mpango unaoitwa Ukanda wa Kilimo wa Kusini mwa Tanzania, yaani

*SAGCOT*. Mpango huu ni muhimu sana na tayari Benki ya Dunia imesema imetenga kiasi cha dola za Marekani milioni 60 kwa ajili ya kutekeleza Mpango huu. Sasa ninajiuliza, zamani tulikuwa na kitu kinachoitwa *Mtwara Corridor* na katika mikakati ya kuinua uchumi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara kupitia *Mtwara Corridor* pia Mkoa wa Ruvuma na Iringa. Sasa Mpango huu wa Kusini unautenga Mkoa wa Lindi na Mtwara.

Kwa hiyo, ninatoa wito kwa Serikali kuona haja kwa kuzingatia namna Mkoa wa Lindi na Mtwara ulivyo nyuma kimaendeleo. Iko haja ya Serikali kuingiza Mkoa wa Lindi na Mtwara katika Mpango huu wa kilimo, kusini mwa Tanzania, ni haki yake. Kwanza Mpango wenyewe unahusu Mikoa ya Kusini na Mikoa ya Kusini ni Lindi na Mtwara, Ruvuma, Iringa na kadhalika. Kwa nini Mikoa hii iondolewe katika Mpango huu? Kwa hiyo, ninaomba Serikali itufikirie na kutuingiza katika Mpango huu ili kuwanufaisha vijana wengi katika meneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo eneo lingine la elimu. Nilikuwa nikisoma Ilani ya Uchaguzi na kuona ukurasa wa 84 wa Ilani unasema ni lazima Serikali itenge kiasi cha 1.0% ya pato la Taifa katika uwekezaji katika Sekta ya Utafiti ili tuweze kufanya utafiti ili tafiti hizi ziweze kuinufasha nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nikisoma Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano sijaona maeneo ambayo imeelezwa waziwazi kutengwa kwa 1% ya pato la Taifa katika utafiti na hii ndiyo inayopelekea sasa kwamba kila mwaka vijana 700,000 wanamaliza elimu ya Vyuo Vikuu, lakini wanaoajiriwa katika sekta rasmi ni vijana 40,000. Lakini ninajiuliza, unafanyika utafiti wa kina wa kufahamu soko la ajira kwa sasa ni lipi, ili vijana hawa wanapohitimu elimu wawe na uhakika kwamba sasa soko letu la ajira linatuelekeza maeneo Fulani fulani.

Kwa hiyo, ninatoa changamoto kwa Serikali kupitia bajeti hii kuona umuhimu wa kutenga 1% kama ambavyo ilani inaelekeza kwa ajili ya utafiti, kwani utatusaidia sana katika masuala ya kuwawezesha vijana kufahamu soko la ajira, kufahamu ni namna gani wasome masomo ambayo yanaweza kuwasaidia kupunguza tatizo la ajira nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namalizia kwa kuzungumzia usimamizi wa fedha za umma. Kwa sababu tumekuwa tukijikita hapa kuangalia vyanzo vipya vya mapato, lakini tunakusanya tunaingiza kwenye kapu ambalo limetoboka, hatimaye mapato yenyewe yanaishia kusikofahamika. Kwa sababu *report* ya Mkaguzi inaonyesha maeneo mbalimbali ambayo ni tatizo kubwa katika Halmashauri zetu, Taasisi za Umma na Mashirika mbalimbali ya Umma, fedha zikiwa zinatumika vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, *report* ya Mkaguzi inasema hadi mwaka 2010 zaidi ya shilingi milioni 583 na ushee zinalipwa kwa Halmashauri 38 ili kuwalipa watumishi waliokufa, waliostaafu na wengine ambao hawapo kazini. Sasa kwa nini Serikali isitekeleze ushauri wa Mkaguzi Mkuu wa Serikali? Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali wakati tunapanga, tuangalie maeneo mapya ili kuongeza pato la Taifa, lakini

maeneo haya ya kudhibiti mianya ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali ni lazima yapewe nafasi.

Rombo kwa rafiki yangu Selasini, Halmashauri inawalipa watumishi 42 waliostaafu kila mwaka, wanalipwa mshahara. Mtu amestaafu au kufukuzwa kazi, lakini wanaendelea kulipa mishahara. *Report* ya Mkaguzi inasema watumishi watano kila mwaka, yaani watu wameshakufa lakini wanaendelea kupata mshahara wa Serikali. Sasa mambo haya ni mambo ambayo yanaturudisha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia eneo lingine ambalo tunapoteza fedha nyingi ni eneo hili la *DAWASCO*, yaani wenzetu wa maji, 27% ya maji yanapotea kutokana na uchakavu wa miundombinu, eneo hili ni lazima lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge kwa mchango mzuri na sasa nitamwita Mheshimiwa John Mnyika, atafuatiwa na Ester Bulaya na baadaye Mheshimiwa Faustine Ngungulile atachangia.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Lakini kwanza niseme tu kwamba nimesikia michango humu Bungeni inayosema mambo mawili makubwa. Kwanza inasema Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani ameiga kutoka mawazo ya Serikali bila kuishukuru Serikali kwa mawazo yake, lakini pili mawazo kwamba CHADEMA kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani haikutekeleza ilani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Serikali imeiga mawazo mengi sana kutoka kwa CHADEMA, ni jambo zuri na kwa sababu mawazo haya yako kwenye Ilani ya CHADEMA ya mwaka 2010 na hayapo kwenye ilani ya CCM.

Serikali kwenye hotuba ya Waziri wa Bajeti imezungumza kuhusu mchakato wa Katiba mpya ambayo haipo kwenye Ilani ya CCM, bali iko kwenye Ilani ya CHADEMA na Serikali imeiga, ni vizuri. Serikali imezungumza kuhusu kupunguza gharama za maisha ambayo haijachambuliwa kwa kina kwenye Ilani ya CCM, lakini humu imechambuliwa na CHADEMA imeeleza ni namna gani ambavyo kuna haja ya kupunguza gharama za maisha kwa wananchi.

Serikali imeiga wazo la wingi wa posho na CHADEMA ilizungumza kwa kina sana na kwa takwimu kuhusu ukubwa wa posho na haja ya kuunganisha posho, kupunguza posho na kadhalika ili kuboresha mishahara ya wafanyakazi na kusukuma mbele maisha na wakati huo huo kuweka uchumi sawa.

Hili wazo nalo Serikali imelichukua, lakini imelichukua ndivyo sivyo. Sasa mimi niseme tu kwamba ni vizuri watu wakawa wanasoma ilani za vyama vingine ili kujua asili ya haya mawazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwepo na wazo kwamba hotuba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haikutekeleza ilani hii. Kuna mambo humu tumeyasema kwenye hotuba ya Kambi na ninaomba tu Serikali iyachukue kwenye bajeti ijayo kama haiingizi sasa ambayo yamo kwenye Ilani na ambayo ni mambo yanayotekelezeka japo awali walisema hayatekelezeki.

Tulisema elimu bure na tulisema bure Kidato cha Kwanza mpaka Kidato cha Sita na tukasema elimu ya juu tunavunja Bodi ya Mikopo, tunatengeneza mamlaka nyingine ya ugharamiaji wa elimu kwa mfumo tofauti.

Kwenye bajeti ya mwaka huu, Msemaji wa Kambi Rasmi ameeleza kwa kina ni namna gani ambavyo tutagharamia elimu kwenye shule za umma za kutwa, ni namna gani watoto wa kike watasoma bure na tumeeleza kwamba yanatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu jambo lingine la msingi kwamba kuna mambo walikuwa wanasema hayatekelezeki kwamba huwezi kushusha *Pay As You Earn* kodi ya wafanyakazi mpaka 9%. Sisi tumeteremsha na tunaomba Serikali ikubali hili wazo na tumeonyesha jinsi gani ambavyo linatelekezeka kwa ajili ya kutetea maslahi ya wafanyakazi.

Tumezungumza muda mrefu kwenye Ilani kuhusu haja ya kutoa *pension* kwa wazee ikasemekana kwamba wazo hili halitekelezeki. Tumeeleza jinsi gani ambavyo suala la kutoa *pension* kwa wazee wote inawezekana kabisa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naiomba tu Serikali katika haya mawazo ambayo hayapo katika bajeti ya Serikali na yenyewe katika hitimisho la Waziri ayatolee kauli na kuyaingiza kwenye utekelezaji. Kuna wengine wamesema kwamba bajeti kivuli haijazungumza kuhusu suala la kupunguza gharama za vifaa vya ujenzi na kumwondolea mzigo Mtanzania maskini.

Kuna mchumi mmoja anaitwa Rostow, tatizo ni kwamba bajeti hizi zinaweza zikawa zinasomwa kama vitabu vya A, E, I, O, U, tusome kiuchambuzi wa kiuchumi. Unapozungumza kuinua viwanda ni lazima utengeneze kitu kinachoitwa *pre-conditions for take off,* kwamba uweke msingi ili uwekezaji kwenye viwanda uende kwa nguvu kubwa zaidi.

Ukiangalia falsafa ya bajeti ya Kambi Rasmi ya Upinzani ambayo mimi naiunga mkono, kwa kweli imejikita katika kuhakikisha gharama za uzalishaji zinapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmezungumza kutaka uwekezaji mkubwa kwenye gesi na hili naomba Waziri katika majumuisho yake alitolee kauli kwa sababu kama Waziri Kivuli wa Nishati na Madini naelewa kwamba ujenzi wa bomba kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam na baadaye Tanga ambao ungepunguza sana gharama za uzalishaji ikiwemo kwenye viwanda hivi vya *cement* kama cha Wazo Hill pale Dar es Salaam na viwanda vingine, bomba hili Serikali ya China iko tayari kuingiza pesa kwa *condition*

kwamba Serikali ya Tanzania iwekeze bilioni 181 kama 15% ya mtaji. Nimepitia Vitabu vyetu vyote hivi vya Bajeti ya Maendeleo na kadhalika, hiki kitu hakipo. Mimi niwaombe tu kwamba kama tunataka kupunguza gharama za uzalishaji, ikiwemo uzalishaji wa *cement* lazima tu-*invest* kwenye gesi na falsafa ya mchango wetu ambao mimi nauunga mkono ni kwamba tulinde viwanda vya ndani, hiyo ndiyo *principle*. Viwanda vyetu vya saruji, iwe ni Mbeya, Tanga au Dar es Salaam vingeweza kuwekewa mazingira ya kupunguza *cost* za uzalishaji na kulinda na kumsaidia Mtanzania kwenye ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihamie eneo lingine, mimi siungi mkono bajeti hii iliyo mbele yetu mpaka Serikali itoe maelezo ya kina sana na siungi mkono siyo kwa sababu niko Upinzani, kwa sababu kuna hoja Serikali imeleta nyingi tu hapa katika Mikutano iliyopita nimeziunga mkono, Maazimio yale ya *SADC, UNESCO* na mambo mengine, lakini hili siungi mkono na siungi mkono kwa sababu wananchi wa Jimbo langu walionileta hapa, wamenituma nisiunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Waziri kusoma Hotuba ya Bajeti, mimi niliandika kwenye ukurasa wangu wa mtandao kwamba hotuba hii ya Waziri imejaa matumaini hewa na bajeti ni ya kiini macho na nilisema hivyo kutokana na takwimu za bajeti yenyewe. Ukichukua kwa mfano suala dogo tu la tozo la faini kwa Madereva kwa mfano kwa watu wanaoendesha vyombo vya usafiri, Waziri alisema kwamba faini inapanda mpaka shilingi 50,000, Muswada wa Sheria ya Fedha unasema faini inapanda mpaka shilingi 300,000, Kitabu cha Mapato ya Serikali, Kitabu cha Mapato ukiangalia faini sehemu ya Wizara husika inaonesha Serikali haikusudii kugeuza leseni na faini hizi kama chanzo cha mapato lakini mantiki ya kupandishwa kwa kiwango hiki iko wapi? Madereva wa pikipiki wa Mbezi, Madereva taxi wa Ubungo na watumiaji wengine wa vyombo vya usafiri wa daladala na kadhalika wamenituma katika hili nisiunge mkono bajeti kwa sababu hii *unless* hiki kitu kiondolewe. Tatizo siyo ukubwa wa faini, faini ya shilingi 20,000 tu sasa hivi iliyopo, ama 40,000 ama ngapi, tatizo ni *enforcement* ya Sheria, rushwa iliyotapakaa. Kwa hiyo, unapoongeza kiwango cha faini, unaongeza tu kiwango cha rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja kwamba, kweli ajali ziko nyingi hata kwenye pikipiki kule Dar es Salaam ajali zinaongezeka sana lakini tufikirie zaidi. Mimi ningeshukuru kama Waziri angekuja na mkakati kwamba sasa tunahakikisha kupitia Chuo cha Usafirishaji pale Dar es Salaam tunatoa mafunzo kwa Madereva pikipiki, Idara yetu ya *Traffic* inakwenda kutoa mafunzo inafanyaje mambo kama haya, ningetarajia kwamba haya ndiyo yangekuwa kipaumbele. Kwa hiyo, katika hili siungi mkono kwa sababu hiyo niliyozungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii inasema kwamba kipaumbele ni nishati na kadhalika, lakini ni maneno. Nimezungumza suala la bomba la gesi ambalo linahitaji *investment* ya bilioni 181 na ningeweza kuzungumza mengine lakini kwa sababu nina *platform* nyingine ya Uwaziri Kivuli nitazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihamie kwenye eneo lingine la msingi sana ambalo linafanya nisiunge mkono bajeti hii. Bajeti inasema *principle* kubwa tunakwenda kupunguza gharama za maisha kwa wananchi, tunapunguzaje kwa sababu gharama zetu zinapanda kwa sababu ya nishati ikiwemo mafuta na umeme, basi tunapunguza tozo kwenye mafuta. Kauli hiyo ni kauli ya kiini macho ndiyo maana Waziri alipotoa hoja yake akasema ufafanuzi atautoa tarehe 22 wakati tutakapojadili Muswada wa Sheria ya Fedha, nimeupitia huu Muswada tutakuja kuujadili baadaye, lakini *principle* ya kukuza tozo haiwezi kusaidia kushusha kwa kiwango kikubwa bei ya mafuta sababu tozo zote za taasisi hizi *SUMATRA*, *TBS* changanyanga na *EWURA* na kila kitu haifiki 3% ni 2.3% tu ya bei ya mafuta. Tozo za makampuni binafsi ya mafuta ni 2% jumla ya tozo zote hazifiki hata 5%. Sababu kubwa ya bei ya mafuta kuwa juu kwenye Taifa letu ni ukubwa wa kodi, asilimia 26 ya bei ya mafuta kwa lita ni kodi, ni takribani shilingi 600. Sasa Muswada huu haujagusa kodi, hotuba haijagusa kodi, vitabu vya mapato havijaigusa kodi kwa sababu hiyo bei ya mafuta itashuka hata Serikali ikijitahidi vipi kati ya shilingi 100 mpaka shilingi 200 ugumu wa maisha utaendelea kuwa pale pale kwa ari, kasi na nguvu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza kuhusu nishati ya gesi ambayo ingetumika majumbani kama *LPG*, gesi hii kama watu wangeitumia ingepunguza bei ya nishati nyingine. Tunazungumzia kuhusu gesi kutumika kwenye magari ambayo ingeshusha nusu ya nauli Dar es Salaam au nusu ya gharama. *Investment* kwenye gesi na miundombinu ya gesi siyo bomba tu lile na mitandao ya gesi, vituo vya kujazia mafuta ya gesi na kadhalika ni kama vile imeachiwa *TPDC* tu peke yake na hiyo *retention* ya 50% kama tunataka kupunguza gharama za maisha lazima pamoja na kupunguza kodi kwenye mafuta twende kuwekeza kwa nguvu sana kwenye nishati mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasema tutapunguza gharama za maisha kwa sababu tutapunguza bei ya chakula, tutafungua *strategic grain reserve* na mambo mengine yamezungumzwa sana humu kwenye hotuba, lakini ni matumaini hewa na kwa *fact* kama kwenye mwaka huu wa fedha uliomalizika, Serikali imefungua ghala, Serikali ikifungua ghala maana yake mimi na wewe na Mtanzania mwingine tunaingia *loss* kwa sababu yale mahindi tumeyaweka mle kwenye ghala kwa pesa zetu, ime-*inject* kwenye soko lakini bei haijashuka. Niwaeleze tu siri moja na Waziri ukitaka nitakuletea taarifa kimaandishi, bei haishuki Manzese pale kwa sababu chakula kinachotolewa hiki cha kutoka katika hii *grain reserve* watu wanabeba wanakwenda kuuza nje kwa bei kubwa zaidi, kwa hiyo haishushi sembe pale Dar es Salaam, sijui Makurumla sijui wapi sembe haishuki, *enforcement* iko *weak*. Kwa hiyo, nitaunga mkono hoja kama haya yatatolewa ufafanuzi wa kina sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti hii kuna mambo humu ya maji, barabara na kadhalika na kwa kwetu sisi Dar es Salaam mtu ukisikia maji, barabara na kwa Ubungo kulivyo na shida ya maji mtu anaweza kusema kwa nini huyu anakataa kuunga mkono bajeti wakati bajeti inazungumza kuhusu maji, barabara, tatizo ni matumaini hewa maana kuna tofauti kati ya maneno na matendo. Ukiingia sasa kwenye Kitabu cha Bajeti cha Maendeleo cha Wizara ya Maji, ile *specific section* ya Wizara ya Maji, ukiangalie *investment* ambayo imewekwa pale kwa ujenzi wa bwawa la Kidunda ambayo ingesaidia

siyo watu wa Morogoro tu kwa sababu Kidunda iko Morogoro, ingeboresha *flow* ya maji kwenye Ruvu Juu ambayo inge-*service* watu wa Ubungo kuanzia Kiluvya, Kwembe na kwingineko, *investment* ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija mradi wa Kimbiji na Mpera, Mkuranga na Kigamboni ambao utasaidia vilevile Ubungo na maeneo mengine ya Dar es Salaam, Serikali ilisema hata kwenye Baraza la Mawaziri najua Mheshimiwa Pinda atakubaliana na mimi walisema kwamba sasa tutaingiza pesa za ndani ili tatizo la maji Dar es Salaam liishe, lakini ukiangalia 35 bilioni ni *expectation* za pesa za nje. Mimi nitaunga mkono hoja tu kama kweli tukidhamiria kwa dhati kutenga rasilimali kwa ajili ya kuboresha hii miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri amesema kwenye hotuba yake kwamba sasa hii bajeti inakwenda kuondoa tatizo la foleni Dar es Salaam, lakini ukipitia bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwenye kifungu kinachohusika na *decongestion of* Dar es Salaam, kupunguza foleni Dar es Salaam, kimetengewa bilioni tano peke yake, sisi wa Dar es Salaam nikiwemo mimi wa Ubungo ambao takribani 80% ya mapato yanatoka kwetu *five billion decongestion, 20 billion fly over*, siungi mkono hoja mpaka tupate kwanza ufafanuzi wa kina kutoka kwenye Serikali, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa John Mnyika kwa mchango mzuri, anayefuatia sasa ni Mheshimiwa Ester Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndungulile na baadaye Wenje ajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niwe miongoni mwa watu watakaochangia bajeti yetu nzuri yenye mwelekeo mzuri wa kumwondoa Mtanzania katika hali ngumu hii aliyo nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeweza kusema tu wachangiaji wenzetu waliopita wamesema CCM au Serikali imeiga kwenye ilani ya CHADEMA lakini mimi nasema hata huo utengenezaji wa Ilani wameiga kwetu, Mfumo wa Vyama Vingi umeanza mwaka 1992, lakini CCM ilikuwepo tangu 1978. Kuna *contradiction* kati yao, je, tumsikilize mjumbe aliyepita ambaye ni Mkurugenzi kwenye Chama chao au Naibu Katibu Mkuu wa Chama chao ambaye ni Naibu Kivuli wa Wizara ya Fedha ambaye kaweka *clear* kabisa, hili siyo wazo la Zitto, wala siyo wazo la CHADEMA, ni mpango wa Serikali wa kupunguza posho zisizo na lazima. Kukubali kuiga kwa wenye *experience* siyo dhambi ni kujifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wenzetu walichangia hapa jana na kujidadavua sana kwamba Watanzania wanajua kina nani wanaumiza vichwa na mimi nilirudie palepale, baada ya Waziri Kivuli wa Fedha jana kuchangia, Watanzania wamejua, je, ni wazo la Mpango au ni wazo la wenzetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya huu mzizi wa fitina kuisha jana, tuache *cheap politics* za kwenye mtandao.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 68, naomba nimpe taarifa tu mzungumzaji kwamba Mpango wa Miaka Mitano wa Serikali ambao umenukuu hiyo sentensi kuhusiana na agenda ya posho umetengenezwa ama umezinduliwa mwezi Juni, 2011 wakati Ilani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ambayo imeeleza kuhusu nadharia ya upunguzaji wa posho ili kuongeza mishahara na kadhalika ambayo ninayo nakala yake hapa, ni ya mwaka 2010. Sasa hii si hadithi ya yai na kuku kipi kimeanza, hata Mheshimiwa Waziri Mkuu alizungumzia suala hili asubuhi, ningeshauri vilevile twende mbele zaidi hata hizi posho za Wabunge, tuitazame Sheria ile ambayo iko *clear* sana kuhusu jambo hili na lishughulikiwe, kwa hiyo, Mwenyekiti aendelee. *(Makofi)*

*Hapa (Mheshimiwa Halima Mdee) Alikuwa Anaongea*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Mdee, mazungumzo ya Bungeni ni rasmi sana, yanaingiwa kwa utaratibu kamili.

Mheshimiwa Mbunge ulichokisema ni taarifa kwa mzungumzaji lakini nisahihishe tu ni Kanuni ya 68 na siyo 78. Mheshimiwa uliyekuwa unazungumza Mheshimiwa Bulaya unaweza ukaipokea ama ukaikataa, una hiari yako.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Unajua lazima tuwe na ngozi ngumu, kwanza taarifa ninaikataa tujifunze tu uvumilivu wa kisiasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Bulaya endelea.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kujifunza vitu vyema kwa watu waliokutangulia si vibaya, wamefanya vizuri kabisa, lakini pia tuendelee kuwalea mpaka watakapofikisha miaka 40 kwa sababu sasa hivi wanaelekea miaka 17, miaka 40 wakiwa na uwezo wa kuongoza *may be* ndiyo tutawapisha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nijielekeze kwenye kuchangia bajeti. Napenda kuchangia katika kipaumbele chetu Namba moja ambacho ni umeme. Kama tunavyojua Taifa letu lina tatizo kubwa la umeme, tumeona Wizara ya Nishati na Madini imetengewa shilingi bilioni 529 lakini ukilinganisha na uzito wa tatizo uliopo hatumaanishi kama hiki kweli ni kipaumbele. Kati ya hizo shilingi bilioni 529, bilioni 325 zimetengwa kwa ajili ya mradi wa umeme lakini hapohapo tunategemea shilingi bilioni 98 kutoka kwa wahisani, sasa nina shaka kidogo kama hiki ni kipaumbele chetu Namba Moja, kwa nini tusitenge fedha ambazo tuna uhakika wa kuzipata kwa 100%? Naamini kabisa Serikali yetu inaweza, tuna mifano dhahiri ambayo tumeamua kufanya vitu kwa fedha zetu wenyewe na tumeweza, mfano tu Chuo Kikuu cha Dodoma, tulitenga shilingi bilioni 800 kwa fedha zetu wenyewe na leo tuna Chuo ambacho

tunajisifia. Vilevile tukaanzisha Mfuko wa Barabara tukawa tunatoza shilingi 200 kwa kila lita ya mafuta ya petroli na tukafanikiwa kujenga barabara zetu wenyewe kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, lazima tunaposema kipaumbele Namba Moja tuoneshe kwa matendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina shaka kama tunaweza tukatimiza malengo yetu, *experience* inaonesha hao wahisani ambao tunawategemea *either* wanachelewesha kuleta fedha au wakileta hawazileti zote na matokeo yake tunashindwa kutimiza malengo yetu. Mimi ninatolea tu mfano, bajeti ya mwaka jana ya Wizara ya Nishati na Madini ilikuwa kwenye bilioni 327, lakini fedha kwa ajili ya mradi wa umeme zilikuwa bilioni 214, lakini hata tu kwa fedha zetu wenyewe za ndani tuliweza kutimiza kwa 49%, wahisani ndiyo kabisa walileta 29%. Kwa hiyo, kupanga ni kuchagua, kama tumeamua hiki ndicho kipaumbele chetu Na.1 lazima tungetenga fedha ambazo tuna uwezo wa kuzipata na kuhakikisha tatizo la umeme linakwisha na Watanzania wanaotusikiliza waone kwamba ni kweli Serikali yao imeona hiki ni kipaumbele Na.1. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tuko zaidi ya milioni 40 lakini wanaopata umeme waliounganishwa katika Gridi ya Taifa ni 14% tu, kati ya hao 12% ni mijini, 2.5% vijijini na kati ya Watanzania wote 80% ndiyo wanaishi vijijini. Kwa hiyo, tunapozungumzia suala la umeme, tunawagusa Watanzania walio vijijini, tunazungumzia kuwawezesha waweze kuboresha vipato vyao, lakini pia waweze kuongeza uzalishaji mali na kuchangia kwenye pato la Taifa. Nina wasiwasi kidogo kama kweli tunaweza tukafanikiwa kutanua huduma ya umeme na hasa vijijini. Katika Kitabu cha Maendeleo hiki hapa, ukienda *Vote* 58 ukiangalia *Subvote* 3112 inaonesha kabisa imetengwa shilingi bilioni moja kwa ajili ya usambazaji umeme vijijini, lakini *Vote* hiyohiyo 58 ukienda kuangalia *Subvote* 3113 imeonesha pale zimetengwa shilingi bilioni 56 kwa ajili ya Mfuko wa Umeme Vijijini, ukijumlisha inakuja kwenye shilingi bilioni 57. Unajiuliza katika mradi wa umeme ziko shilingi bilioni 325, lakini vijijini ambako ndio kuna watu wengi wametengewa shilingi bilioni 57 tu. Hapohapo bado kuna shilingi bilioni saba tunategemea tena fedha kutoka kwa wahisani. Tunawezaje kutimiza lengo? Tunawezaje kuongeza huduma ya umeme vijijini na unapozungumzia umeme unazungumzia maisha ya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuzungumzia suala la *EPZ*. Tunajua Serikali yetu ina dhamira njema ya kuongeza uwekezaji ili kuendelea kuhakikisha Watanzania wanapata ajira na kuondokana na umaskini lakini kumekuwa na malalamiko mengi kwa wananchi ambao wanapisha mradi wa *EPZ*. Napenda niongelee Bunda, Kata ya Tairo. Kuna watu zaidi ya 404 wameshafanyiwa tathmini tangu mwaka 2007 na hapa tunapoongea ni zaidi ya miaka mitatu wanashindwa kuendeleza maeneo yao, umaskini unaongezeka kwa sababu ya kupisha mradi wa *EPZ* na mpaka sasa hivi hawajalipwa, waliolipwa ni watu 116 tu. Najua kabisa hili suala la *EPZ* ningeweza kulizungumzia katika Wizara ya Viwanda na Biashara lakini najua hii ndio *main budget,* Mheshimiwa Mkulo anajua kabisa zimetengwa kiasi gani kwa ajili ya kuwalipa waathirika wa *EPZ*. Kwa hiyo, napenda ufafanuzi nijue ili wananchi wa Bunda ambao wanashindwa kuendeleza maeneo yao wajue hatma yao, je, watalipwa au hawatalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kupongeza Serikali kwa kuondoa tozo 21 za mafuta kwa sababu unapoondoa tozo 21 za mafuta unashusha gharama za uendeshaji viwandani, unashusha gharama ya usafiri na unamsaidia Mtanzania kuondoa hali ngumu ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuondoa kodi katika pembejeo za kilimo lakini napenda pia anipe ufafanuzi. Je, kodi ile inaishia katika vipuri vya *power tillers* au vinagusa kwenye vipuri vya trekta kwa sababu tunaamini kabisa pia matrekta yanatoa mchango mkubwa na pia wakulima wetu wataweza kutumia matrekta zaidi ku-*make sure* wanaboresha kilimo chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa kujivunia kabisa na Serikali yangu katika bajeti hii nzuri mbali na kuacha porojo za wengine kwa sababu asiyekuwa na shukrani hawezi kushukuru kwa chochote hata ukimwachia Ikulu atakuuliza Ikulu ina nini? Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia bajeti hii. Awali ya yote, napenda kuwashukuru Wana-Kigamboni kwa kunichagua kuwa Mbunge wao, nawaahidi uwakilishi uliotukuka na kamwe sitowaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kusikia kilio cha wananchi. Kabla ya kuja katika Bunge hili, nilipita katika baadhi ya Kata zangu katika Jimbo la Kigamboni na kilio kikubwa ni kwamba bajeti hii isikilize kilio cha wananchi cha hali ngumu ya maisha. Niipongeze Serikali kwa kuliona hilo na kutengeneza bajeti ambayo imeliangalia hilo.

Mheshimiwa Spika, pili, niipongeze Serikali kwa kutengeneza bajeti ambayo imezingatia vipaumbele vya Kitaifa. Mheshimiwa Mnyika wakati anatoa hoja yake alisema kwamba zile ahadi ambazo walikuwa wameahidi katika Ilani yao kwamba ni lazima zitengenezwe *pre-conditions* ya kuzifanikisha. Vilevile kwa huu Mpango ambao Serikali umekuja nao na sisi tunatengeneza hizo *pre-conditions* za ku-*take off* ili ile dhana nzima ya maisha bora kwa kila Mtanzania iweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nijikite katika baadhi ya maeneo. Vipaumbele ambavyo vimeainishwa katika bajeti yetu ni vya msingi lakini vilevile nataka kuongeza kwamba kuna hatua kubwa ambayo tumepiga katika suala la afya na elimu. Mafanikio haya yanapaswa kulindwa na napendekeza kwamba pamoja na hivi vipaumbele ambavyo tumeviweka hapa suala la elimu na afya viwe ni vipaumbele vya kudumu. Mtaji wa maskini ni elimu na afya njema aliyokuwa nayo. Niipongeze tena Serikali kwa Mpango wa Maendeleo ambao tuliuidhinisha hivi karibuni. Tunaomba sana Serikali hii iwe ndiyo dira ya uandaaji wa bajeti zetu na kuwepo na mwendelezo. Lile wazo ambalo tumekuwa nalo la kuanzisha Ofisi ya Bajeti katika Bunge litasaidia sana kulipa Bunge letu mwongozo katika uandaaji na ufuatiliaji wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia kidogo katika masuala ya ugumu wa maisha. Kuna masuala matatu ambayo kwa kiasi kikubwa yamechangia sana katika kuleta hali hii tuliyonayo ya ugumu wa maisha. Moja, ni suala la mafuta, pili, suala la umeme na tatu ni suala la bei za vyakula. Serikali imeonesha nia njema kabisa ya kutaka kupunguza kodi na tozo katika suala la mafuta, hii ni hatua nzuri. Ni hatua ambayo ningemwomba ndugu yangu Mnyika asiibeze, ndio *pre-conditions* ambazo tunaziongelea. Serikali imesema kwamba itaiangalia suala hili ili kati ya zile tozo na kodi mbalimbali ni zipi ambazo inaweza kupunguza kuleta unafuu katika bei ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeongelea kwamba kuna utaratibu ambao tunataka tuuanzishe wa *bulk procurement* ya mafuta, mfumo huu utapunguza sana gharama za mafuta. Vilevile kuna mambo ambayo tunahitaji tuyaangalie pamoja na hatua nzuri ambazo tumezichukua, bado udhibiti wa bei za mafuta nchini sio mzuri. Tunaandika katika magazeti kwamba bei ya mafuta katika kila Mkoa isizidi kiasi fulani lakini bado tunaona kwamba upandishwaji wa bei ya mafuta ni holela. Serikali bado inahitaji kulifanyia kazi suala hili. Pili bado tunahitaji kudhibiti ubora wa bidhaa za mafuta, uchakachuaji wa mafuta uko juu sana. Hii inatutia hasara kubwa sana na ni suala kwa kweli bado tunahitaji tuliangalie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme ni janga la Kitaifa nadhani wasemaji wengi waliopita wameliongelea. Hatuhitaji siasa katika suala la umeme. Wananchi waliotutuma wanahitaji kuona vitendo zaidi. Tuwe na malengo thabiti na tuweke muda maalum wa utekelezaji. Vilevile twende mbele zaidi pale malengo yasipotimia tuwe na njia ya uwajibikaji ili tufike mahali kwamba hili tatizo la umeme liwe ni historia. Bajeti iliyotengwa katika sekta hii bado ni ndogo sana kuondoa kabisa tatizo hili. Kwa hiyo, ni suala la umeme tunahitaji tukae tulitafakari kwa kina kwa kuangalia jinsi gani tunaweza tukaboresha ili basi ndani ya hii miaka mitano tatizo la umeme liweze kuondoka kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la chakula, tunaishukuru Serikali na kuipongeza kwamba iliweza kutoa mahindi katika Ghala la Taifa au Hifadhi ya Taifa kwa ajili ya kupunguza tatizo la njaa lililokuwepo na ikatoa bei ambayo ilipaswa kutumika katika kuuza ule unga, lakini bado tuna haja ya kuwa na utaratibu wa kudhibiti bei za vyakula muhimu kwa wananchi. Ikiwezekana turudishe Tume ya Bei ili bei ya vitu kama unga, mchele, maharage na sukari viweze kuthibitiwa. Nakumbuka hapa katikati bei ya sukari ilipanda sana, Waziri Mkuu akatoa tamko kwamba sukari isiuzwe zaidi ya shilingi 1,700/=, lakini ukivuka kwenda Kigamboni bei ya sukari pale ni shilingi 2,000/=. Kwa hiyo, kwa kweli bado tunahitaji jitihada za makusudi kufanyika ili kuhakikisha kwamba bei za vyakula zinadhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee katika vyanzo vya mapato na matumizi. Kama tuna nia ya dhati ya kuleta maendeleo nchini basi bajeti zetu zinatakiwa kuonesha mlengo huo. Suala la kudhibiti matumizi yasiyo lazima, matumizi mabaya na upotevu wa fedha yanahitaji kufanyiwa kazi. Tunashukuru Serikali imeanza kuonesha nia hiyo ya kudhibiti baadhi ya matumizi lakini suala la Hati Chafu ambazo zinapatikana katika baadhi ya Taasisi na Halmashauri, zinanipa mashaka makubwa sana. Kuna upotevu mkubwa sana wa fedha, hili linahitaji kudhibitiwa. Wakati tunataka kuonesha kwamba

tuna nia ya dhati ya maendeleo basi na sisi tuonekane tunajibana. Kuna matumizi mengine ambayo sio ya lazima ambayo inabidi kuyaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kulisemea kidogo ni suala la matumizi ya Dola katika uchumi wetu. Tanzania sasa hivi inakuwa kama Zimbabwe. Tuna shilingi yetu lakini vitu vingi sasa hivi tunatumia Dola katika manunuzi. Suala hili linahitaji kudhibitiwa. Mimi si Mchumi lakini nadhani suala hili lina athari kubwa sana katika thamani ya fedha zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba sasa hivi tuna mfumuko mkubwa sana wa maduka ya fedha za kigeni, haya nayo yanahitaji kudhibitiwa. Maduka haya yanatumika kuhalalisha fedha haramu na utoroshaji wa fedha zetu nje ya nchi. Tunahitaji kusimamia vizuri maduka haya ambayo yanabadilisha fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuendelea, lazima tupanue wigo wa kodi. Wigo wetu wa kodi bado ni mdogo sana. Nilikuwa naangalia uwiano wa kodi na pato la Taifa, kodi inachangia karibu asilimia 16.3, hii bado ni ndogo sana, wenzetu Kenya sasa hivi wako zaidi ya asilimia 20, tunahitaji kushirikisha sekta zisizo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hatujaweza kukaa na kutumia kikamilifu jiografia ya nchi yetu na rasilimali tulizokuwa nazo. Sasa hivi ukiangalia pamoja na bandari tuliyokuwa nayo, nchi ambazo ziko jirani na sisi wanaanza kutukimbia. Wanatumia bandari ya Mombasa na juzi nilikuwa nasoma kwamba wenzetu wa Zambia wameanza kuwekeza katika bandari ya nchi kavu kule Namibia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi nayo kwa kweli ni eneo ambalo tunahitaji kukaa na kulifanyia kazi kwa haraka. Mchango wake katika pato la Taifa ni asilimia 1.4, bado ni dogo sana. Tunahitaji kuwekeza katika sekta hii na ikiwezekana si dhambi kuifufua tena *TAFICO* ili basi itusaidie katika eneo hili la kuongeza pato la Taifa na vilevile kuongeza katika ajira kwa vijana. Mifugo tunayo mingi sana, tuna ng'ombe karibu 20,000,000 na mbuzi 13,000,000 tukiweza kuitumia vizuri rasilimali hii kwa mauzo ya nyama, jibini, maziwa na ngozi kama wenzetu wa Botswana, tunaweza tukapata pato kubwa la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile matumizi ya ardhi bado ni madogo sana. Eneo la ardhi inayolimika ni karibu asilimia 23 ya nchi hii lakini ukikaa ukiangalia kilimo cha umwagiliaji tunatumia asilimia moja tu. Katika hotuba nyingi za wenzangu wamekuwa wakichangia kuhusu masuala ya njaa. Tuna vyanzo vingi vya maji ambavyo tukiweza kuvitumia vizuri vinaweza vikatusaidia kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo kuhusu suala la Kigamboni. Naishukuru Serikali kwa kuweza kusikia vilio vyetu Wana-Kigamboni, ahadi za Rais ndani ya miezi sita zimeanza kutekelezwa. Ujenzi wa daraja la Kigamboni utaanza mapema mwakani na ujenzi wa barabara ya Kilwa umeanza, tumeanza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie suala la Mji Mpya wa Kigamboni. Tunaiomba Serikali ichukue hatua za haraka za kuanza ujenzi wa Mji wa Kigamboni. Wana-Kigamboni wako tayari lakini kadri Serikali inavyochukua muda inazidi kuwatia umaskini. Wana-Kigamboni hawakopesheki, hawawezi kuendeleza wala kuuza ardhi yao na nyumba zao, Wana-Kigamboni wanahitaji kutoka kifungoni kwa Serikali kuwaambia ni lini mradi huu utaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe kwa kusema kwamba nchi yetu inasifika kwa amani na utulivu. Kuna wenzetu wanalilia na kutamani amani na utulivu tuliokuwa nao, sisi tunaanza kuichezea. Wananchi waliotutuma ni waajiri wetu wanaotaka kuona humu ndani ya Bunge tunakuwa na mijadala ya kuleta maendeleo na ustawi wa nchi yetu na kuboresha maisha yao. Mambo ya mipasho, malumbano na vijembe hayafai. Siasa sio uadui na wala siasa sio uhasama. Tofauti za itikadi ni mtazamo tofauti wa kufikia lengo lilelile moja na kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza niwapongeze wachangiaji wa leo asubuhi, michango ilikuwa mizuri, lakini bado tunatumia muda wetu vibaya, muda mwingi tunautumia kwa miongozo, utaratibu na taarifa. Tulitegemea wachangiaji 12 watachangia lakini wachangiaji 10 tu wamechangia. Imani yangu ni kwamba jioni basi tutajitahidi tuweze kutumia muda wetu vizuri zaidi. Labda niwataje watakaoanza kuchangia jioni, wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Albert Ntabaliba halafu na wengine watafuatia.

Basi kwa kuwa muda wetu umetuishia, nichukue nafasi hii kusitisha Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wa Bajeti na aliyepaswa kuchangia alikuwa ni Mheshimiwa Wenje lakini ana udhuru, sasa nitamwita Mheshimiwa Godbless Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa sababu ya fursa ya kuchangia kwenye hotuba ya bajeti ya Waziri Kivuli pamoja na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefuatilia kwa makini sana hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati, hotuba ya Waziri wa Fedha, tumeshiriki kuandaa hotuba ya Waziri Kivuli wa Fedha, kinachonishangaza sana ni hivi vitabu vya ripoti ambavyo vina mchanganuo wa mapato na hasa nikiangalia katika sehemu mbalimbali ambazo baadaye nitapenda kuzi-*mention*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ufuatiliaji wangu, nimeona mambo mengi sana na mengi sana yanastajaabisha, *especially* hizi takwimu na mtazamo mzima wa bajeti yetu ya mwaka 2011/2012. Nilikuwa naangalia kwenye mchango, sekta ya madini inachangia kiasi gani katika Taifa letu, ukijumlisha Almas, Dhahabu, Tanzanite pamoja na sekta ya kilimo, mchango wake katika Taifa hili unazidiwa na sekta moja ya *Horticulture* katika Taifa la Kenya. Ukiangalia mchango wa madini kwenye *mining royalty* mwaka 2009/2010, Tanzania ilipata zaidi ya shilingi bilioni 80.7 na kwenye kilimo ikapata kiasi fulani cha pesa tu lakini kwenye Kitabu cha *Financial Statement and Revenue Statement* inaonesha kwenye *Horticulture* peke yake tulipata shilingi milioni tano na laki tisa mwaka 2009/2010 lakini wale wanaoshughulika na mambo ya *Horticulture,* Tanzania *Horticulture Association*, kwenye ripoti zao ambazo ninazo, wanasema Tanzania kwenye sekta nzima ya *Horticulture and Agriculture,* wamepata dola za kimarekani milioni 350. Cha kushangaza kwenye bajeti hii ya kwetu tumekipa kipaumbele kilimo ingawa sio sana na tukasema kwamba angalau basi tuongeze bajeti kwa sababu kilimo ni uti wa mgongo lakini kwenye *Horticulture* ambayo kwa Taifa la Kenya inazalisha *revenue* zaidi ya dola bilioni mbili kwa mwaka sisi kwenye makisio yetu ya mwaka 2011/2012, Waziri ama Wizara husika ametuambia kwamba tutazalisha sifuri. Kwa kweli hii ni aibu na nimwombe Waziri, siyo kwamba amekosea kwa sababu kuna makosa mengi yamefanyika, ningeomba ripoti ama taarifa kama hizi kabla hazijafika kwa Wabunge ziwe zinapitiwa kwa makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba uchumi wetu unakua, lakini unakua vipi. Nimejaribu kupitia michanganuo ya bajeti za Serikali kuanzia mwaka 1921 na ripoti inasema bajeti bora ilikuwa ni mwaka 1963 mpaka mwaka 1964 na mwaka 1965, ambapo katika bajeti hiyo ndiyo peke yake ambako matumizi kwa upande wa maendeleo yalizidi matumizi mengine ya kawaida na matumizi ya Serikali na shughuli zingine za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona deni la Taifa limeongezeka kwa asilimia 38 na wakati huo kwenye takwimu tunasema uchumi umekua. Tunaona deni la Taifa limetoka trilioni 7.6 mwaka 2008 mpaka trilioni 10.5 mwaka 2009 na sasa kwa mujibu wa hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi deni limefikia dola za Kimarekani bilioni 11.4 ambazo ni sawa na shilingi trilioni 17.1 kwa bei ya dola za Kimarekani Desemba mwaka 2010. Ukiangalia *facts* zote hizi huoni uchumi unakuaje kutoka kwenye deni la shilingi trilioni 7.6 mwaka 2008 na baada ya miaka miwili tu deni hilo limefika trilioni 17.1 maana yake ni kwamba hakuna uchumi unaokua isipokuwa ni vitu ambavyo kwa kweli havina msingi.

Mehsimiwa Mwenyekiti, tunaongelea maendeleo, tunaongelea kilimo, Tanzania walisaini mkataba na Cardiff na kwenye kitabu ambacho hata Halima Mdee jana alisoma hapa inaonesha kwamba walikubaliana kwamba *at least* bajeti ya kilimo ifike asilimia kumi ya bajeti nzima ya nchi yetu lakini kimsingi tumeona kwamba iko takribani asilimia sita tu. Kwa hiyo, dhamira ya kweli ya kusema kilimo ni uti wa mgongo na kwamba kwa kilimo tunaweza tukakomboa Taifa hili, kimsingi unakua huioni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mambo ya msingi katika ripoti hizi, ripoti ya *CAG* ya mwaka 2009 na mwaka 2010 imebaini takribani jumla ya shilingi trilioni 2.4

fedha za umma zimetumika vibaya ambazo ni asilimia 25 ya bajeti ya mwaka wa fedha ambao umepita. Fedha hizo ilikuwa ni trilioni 9.5, maana yake ni nini? Maana yake katika kila shilingi mia inayoenda Serikalini shilingi ishirini na tano inaliwa na mafisadi ama inaliwa na wezi. Nimeangalia kwenye hiki Kitabu cha *The Tanzania Five Years of Development* na nimeona Bwana Mpango ame-*recommend* habari ya *Good Governance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika michango ya watu wengi sana humu ndani wamekuwa wakipiga vita maandamano, wakilaani maandamano, wakifikiri Taifa hii ina amani ya kutosha, ndiyo sababu watu wengine wanataka kuvuruga amani. Kwanza, nawapongeza sana watu wanaojitokeza kwenye maandamano na niwaombe tu watu wangu wa Arusha Mjini kama miundombinu itaruhusu kwamba kutakuwa na taa za barabarani ikatulazimu hata kuandamana usiku kwa ajili ya kupigania utu wa nchi hii na usawa wa nchi, maandamano hayajawahi kuwa dhambi. Sisi kama Chama hatujawahi kuandamana kupiga mtu, sisi kama Chama siku zote tunaandamana kupinga gharama za maisha na maandamano haya yamewaleta kwenye kona nzuri hata leo mmeanza kufikiria kutoa tozo za bei ya mafuta katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi sana yalipokuwa yakisemwa maandamano, kamera zilielekea upande wa CHADEMA ikaonekana kama CHADEMA ndiyo wana-*initiate* maandamano. Mimi niwapongeze Viongozi wangu wa Kitaifa na napenda kuwaambia kwamba hatutarudi nyuma *as long as* hayo maandamano yana lengo la kutafuta amani ya nchi hii, yana lengo ya kutafuta usawa nchi hii, yana lengo la kutafuta fursa sawa na haki sawa, yana lengo ya kupinga ufisadi na ubadhirifu wa pesa katika nchi hii, hayo maandamano tutaendelea kufanya usiku na mchana na hatutarudi nyuma. Polisi jiandaeni sana lakini *peoples power* ita-*overcome*. Hatuwezi kusema Taifa letu lina amani ya kutosha ya kuendelea kuleta Wawekezaji wakati Wawekezaji wanaona wananchi wa chini wanaendelea kuwa wanyonge sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa Tarime na mimi ndiye niliyezuia wale watu wasizikwe wala hiyo siyo siri na Mheshimiwa Tundu Lissu akaenda kukazia msumari. Nilipokuwa Tarime nilipata fursa ya kuongea na Afisa Uhusiano wa Barrick, aliniambia maneno haya, alisema toka Polisi wameua wananchi Nyamongo leo ni siku ya sita mauzo yetu kule *London* yamepungua kwa asilimia sita na tunatarajia ikiwezekana baadaye tuuze mgodi kwa sababu Wazungu wameanza kusema hii ni *blood gold* kwa sababu watu wengi wamekuwa wakiuwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taifa hili hakuna amani ya kutosha, mimi nimekwenda Magereza kusalimia Wafungwa, nimeonana na Mahabusu na Wafungwa, nimekutana na Mahabusu wawili wamekaa jela miaka nane kesi yao haijawahi kusikilizwa Mahakamani, tunasema Taifa letu lina amani. Juzi watoto wa *UDOM* wamefukuzwa na magazeti ya leo yote yameandika. Wale vijana wameandamana kudai posho za kwenda *field*, hawajaandamana kuja kufanya fujo Bungeni. Wanataka kutembea kupeleka hisia zao kwa viongozi ili viongozi waweze kuridhia kile kitu ambacho wanakitaka, ni kitu cha msingi, wamefukuzwa Chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tu kitu kimoja kwamba msingi wa kweli wa amani ya nchi hii utakuwa ni usawa, utakuwa ni haki na siyo blabla ambazo tunakuwa tunazifanya mara kwa mara. Tukiweza kuishi kwa usawa, tukaanza kuona kwamba kila mtu ana fursa katika Taifa hili, tukaanza kuona kwamba siyo Chama chenye Polisi na Wanajeshi ndiyo kinaweza kikaamua kitu gani kifanyike isipokuwa kwa Kanuni za Msingi za Ukombozi wa nchi hii, wala maandamano hayatakuwepo. Mkitaka kujua haya maandamano hayafanywi na CHADEMA ila yanafanywa na wananchi wanaotaka ukombozi wa nchi hii, ninyi nendeni mkajaribu muone kama kuna mtu mmoja atatoka kuwa-*support*. Watu wanatafuta matumaini, watu wanataka haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kuelekea katika bajeti hii, siungi mkono kabisa mapendekezo ya Waziri wa Fedha. Isipokuwa nashauri bajeti iliyotolewa na Kambi ya Upinzani pamoja na ile iliyosomwa na Mwenyekiti wa Kamati hii, basi zingechukuliwa pamoja, mambo ya msingi yakachukuliwa kwa ajili ya kuweza kuleta ukombozi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kitu kimoja cha msingi kama nitakuwa na huo muda. Wakati takwimu zinatuambia vijana wasiokuwa na ajira nchi hii ni asilimia 14 tu, takwimu hizo hizo zinatuambia vijana wanao-*graduate* kila mwaka ni zaidi ya vijana laki saba na elfu arobaini tu ndiyo wanaoweza kuingia kwenye soko la ajira. Sasa inachanganya kati ya laki saba walio-*graduate*, elfu arobaini tu ndiyo wanapata ajira, ina maana laki sita na sitini hawana *access* na ajira halafu takwimu zinasema vijana wasiokuwa na ajira ni asilimia 14 tu, mpaka taarifa inachakachuliwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye ripoti ya Mifuko ya Jamii, wanasema Watanzania walio katika Mifuko ya Jamii ni *almost* asilimia tatu ya Watanzania wote. Sasa unajiuliza hiyo ajira inapimwaje na ndiyo sababu uta-*realize* sasa humu ndani hata mishahara ya kawaida, posho za kawaida, zimeanza kuonekana ni vitu vya thamani kubwa kwa sababu wale walioko chini wanaishi maisha magumu sana uki-*compare* na wale wengine wenye maisha nafuu. Pengine leo kusingekuwa na ugomvi wa kupigania posho yaani *sitting allowance* ama mshahara wa Mbunge lakini ugomvi huo unatokana na nini, ni kwa sababu kuna mwingine analipwa laki na thelathini halafu mwingine anachukua milioni mbili na laki tano. Ukitafuta hapo uwiano unaona huyu anayechukua milioni mbili na laki tano ni pesa nyingi sana, lakini kwa *status* ya Mbunge una-*realize* kwamba hata huo mshahara pengine ungekuwa ni mdogo, lakini kwa sababu tuna watu maskini sana chini tunaanza sasa ku-*justify*, kutafuta njia ya kuonesha uzalendo kwamba jamani hii mishahara ni mikubwa, lakini mishahara ni midogo na ya kawaida, lakini kwa sababu watu wetu tumewasahau. Tunamlipa Polisi laki mbili na sabini, tunambebesha bunduki usiku na mchana. Tunamlipa Mwalimu laki moja na themanini, tunambebesha chaki kutwa nzima. Hapa imeongelewa asubuhi kwamba Mwalimu anatoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kilomita mia mbili kufuata mshahara. Hawa watu kimsingi wanapokuja kukaa wanaona kama sisi tumekaa hapa kuwanyonya hata kama maisha tunayoishi ni ya kawaida sana, napendekeza tuache blabla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye ripoti hii, Waziri umesema utaondoa kodi kwenye mabasi yanaitwa *Apron*, *Apron buses* ni basi zinazokaa ndani ya

*airport*, zile basi nchi hii hatuhitaji hata kumi. *Kilimanjaro International Airport* ukiwa mwanzo wa kiwanja na mwisho wa kiwanja ukimwita mtu anaitika, *Apron buses* unaziondolea kodi za kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Godbless Lema. Ningeshangaa sana kama usingezungumzia maandamano. Tuendelee, anayefuatia sasa ni Mheshimiwa Jasson Rweikiza na Mheshimiwa Obama Ntabaliba.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi naunga mkono hoja ya Serikali kwa asilimia mia moja. Ni hoja nzuri, bajeti nzuri, imeandaliwa kwa umakini mkubwa na ikitekelezwa, itatukomboa na matatizo ya umaskini na uchumi duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii imejikita kwenye mambo muhimu kadha wa kadha. Kwanza, kupambana na mfumuko wa bei, pili kuongeza ajira, haya ni mambo makubwa. Sasa Mpinzani aliyeongea sasa hivi, nimemwona alivyokuwa anaongea, anaonesha dalili ya ushari kwamba yeye na wenzake wapo kwenye shari. Tupo kwenye bajeti ya kuondoa matatizo wanayoyazungumzia, tunapanga mipango ya kupambana na matatizo hayo, yeye anaongelea mambo ya maandamano. Huwezi kujivunia *UDOM* kufukuza Wanafunzi, kusimamishwa masomo, ni jambo la kusikitikia, si jambo la kujivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ninaiunga mkono. Imezungumzia kupunguza bei ya chakula kwa maana kwamba yule Wakala wa Chakula anaweka *stock* na wakati wa uhaba kinauzwa kwa bei ambazo ni nafuu. Kwa hiyo, inasimamia bei inakuwa chini, hii ni namna moja ya kupunguza mfumuko wa bei na maisha ya mwananchi yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwenye suala la chakula, tuongeze sukari. Nafahamu sukari siyo nafaka, tulikuwa na *SGR* ile ilikuwa ni ya nafaka, hii tuliyoanza sasa hivi *NFRA* ina chakula chote siyo nafaka peke yake, tuweke pia sukari kwani imekuwa ni tatizo kubwa sana. Bei ya sukari nchi nzima inakwenda ovyoovyo, imekuwa inapanda sana na wananchi wanapata shida kubwa sana kwenye sukari. Sukari pia iingizwe kwenye utaratibu wa Wakala huyu ili na yenyewe iweze kuwa na bei ambayo inasimamiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kilimo, bajeti hii imependekeza mambo mbalimbali ili kuboresha kilimo; mikopo kwa wakulima, huduma za ugani zitaongezwa, matumizi ya mbegu bora na mbolea, pembejeo na kadhalika. Tumeambia (*TIB)* Benki ya Rasilimali itaongezewa bilioni mia moja katika Dirisha la Kilimo. Hii ifanyike haraka ili kilimo kipate msukumo mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa tutakuwa na Benki mpya ya Kilimo, ianze haraka, tuweke msukumo kwenye kilimo. Hatuwezi kupiga hatua kubwa kwenye kilimo bila ya kuangalia bei anayopata mkulima mdogomdogo *(peasant).* Pale Bukoba tunalima

kahawa lakini bei ya kahawa kwa mkulima ni ndogo sana lakini bei ya kahawa kwenye soko la kahawa inakouzwa kwa mlaji ni kubwa. Kwa hiyo, katikati hapa kuna mirija, anauza kahawa Chama cha Msingi cha Ushirika, inakwenda Chama Kikuu cha Ushirika *(Union)*, kuna Bodi au Mamlaka ya Mazao inayohusika, mpaka imfikie mlaji, ile bei anayotoa mlaji na anayopata mkulima ina tofauti kubwa sana. Tupunguze mirija ili mkulima apate bei ambayo kidogo ina nafuu, imsaidie mkulima na isaidie nchi hii kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia posho hapa ya Wabunge na Watumishi wa Umma, tunazilinda. Asubuhi Mheshimiwa mmoja ametoa na Katiba kuzungumzia posho ili kuhamasisha utendaji kazi katika sekta ya Umma, Serikalini na kwingineko na mkulima apewe posho kwa mazao yake anayolima kwa maana bei ipandishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu, bajeti hii mipango mingi imeelezwa mle kuboresha elimu. Naipongeza Serikali kwa jitihada zake. Tuongeze bidii kwenye elimu hasa kwenye shule ambazo ziko vijijini. Mishahara ya Walimu iangaliwe upya, iongezwe. Wana mazingira magumu, wapate mshahara ambao kidogo unaweza kuwakidhi mahitaji yao na maisha yao ya kila siku. Nyumba za kuishi za Walimu tujenge kwa nguvu nyingi, zimo kwenye bajeti, tuongeze fungu ili zijengwe haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia umeme na ni eneo kubwa kwenye bajeti hii kwamba utawekwa mkazo mkubwa kwenye umeme. Nishukuru na kupongeza Serikali kwa jitihada zake kwenye suala la umeme. Kazi inafanyika kubwa sana, umeme unaongezeka, usambazaji na ugavi lakini umeme bado hautoshi, kuna upungufu mkubwa. Siyo siri tuna upungufu kwa sababu tunauhitaji, tunautumia sana ndio maana kuna upungufu mkubwa wa umeme. Ukiwa na unga kilo mbili na mko wawili mna njaa mnapika mnakula mnashiba, mkiwa watu 20 hamshibi na umeme ni hivyohivyo, tuko wengi tunauhitaji matumizi makubwa viwandani, majumbani na maofisini, tuongeze juhudi umeme uweze kukidhi mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Bukoba tuna Mradi wa Umeme Vijijini unakwenda kwenye Kata zaidi ya 12. Kata za Kemondo, Katerero, Ibwera, Butelakuzi, Rubale, Izimbya, Buturage, Kaibanja, Katoro, Nyakibimbili, Kasharu, Kishogo na maeneo jirani, vijiji vingi sana vitakuwa na umeme. Naipongeza Serikali na nawashukuru sana. Tatizo ni kasi ya kujenga ile *line,* inakwenda taratibu sana. Nguvu ziongezwe mradi ukamilike mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kupeleka umeme katika maeneo niliyoyasema lakini umepita juu mpaka mwisho. Chini kuna wananchi wana nyumba zao, wana shughuli zao, wachomeaji wa mageti na shughuli mbalimbali zinazohitaji umeme, hawana uwezo wa kuteremsha umeme ule. Tuanzishe utaratibu kama tulivyofanya *REA*, tumeanzisha *REA* (Wakala wa Umeme Vijijini), utaratibu wa kusaidia wananchi hawa kupata umeme kwenye nyumba zao. Kukiwa na umeme mita 500 kutoka kwenye nyumba ya mtu kumwambia aingize kwake hawezi kulipia shilingi 500,000 au 1,000,000, hana uwezo huo. Tufanye utaratibu ambao utawasaidia wananchi hawa kupata umeme katika nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la afya. Bajeti hii imegusia sana suala la afya, kuboresha afya za wananchi. Tunajenga hospitali, tunajenga zahanati kila kata, vituo vya afya, tunapeleka dawa na wataalam, huduma inazidi kuboreshwa lakini tuongeze jitihada, bado huduma haijawa nzuri. Pale Bukoba tuna hospitali moja inaitwa Izimbya ni ya Kanisa la Kilutheri. Mwaka 2008 kanisa lilikubali Hospitali hii itumike kama Hospitali Teule ya Wilaya *(DDH)*. Tukaitumia ikawa Hospitali Teule ya Wilaya, huduma ya wananchi ikaboreka. Wakapata dawa kwa bei nafuu au bure, Waganga wazuri wenye upeo wa hali ya juu na huduma nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka jana tarehe 24/8, Mheshimiwa Rais alikwenda pale kwenye Kampeni karibu na Izimbya akasema Hospitali hii itaendelea kuwa Hospitali Teule ya Wilaya lakini baadaye kidogo mwezi wa 10 hadhi ya *DDH* ikaondolewa kwa sababu ambazo haziko wazi. Tukafutilia tukaambiwa sijui kuna upungufu huu, kuna upungufu ule tukarekebisha. Mwaka huu mwezi Machi alikuja Mheshimiwa Waziri Mkuu, tukamweleza, akatoa maagizo kadha wa kadha yenye lengo la kwamba baadaye kidogo Hospitali hii irudie hali yake ya *DDH*. Hivi ninavyoongea bado haijawa *DDH*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Cha kushangaza, Wizara ya Afya inapeleka fedha kule wananchi wapate huduma nzuri. Mwananchi wa Izimbya kufika Bukoba kwenye Hospitali ya Mkoa ni kilomita 100, Kata jirani ya Kibirizi kufika Bukoba Mjini kwenye Hospitali ya Serikali ni kilomita 120. Kanisa limekubali tuitumie, Wizara inatoa fedha inakwenda pale, lakini kuna watu fulani fulani humu ndani ya Wizara ya Afya wanasema isiwe *DDH*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nasema hatuwezi kuwa na maendeleo kama afya za wananchi hazijaangaliwa vizuri. Serikali inajitahidi, inatoa msukumo mkubwa, kuna watu wachache ambao kwa sababu zao binafsi hawataki kufanya kazi zao. Sasa nasubiri Bajeti ya Wizara ya Afya, tutashikana mashati, haitapita. Wanieleze kwa nini hospitali hii haijapata hadhi ya *DDH* tuliyokuwa nayo mwanzoni? Yale marekebisho tumeshafanya, milango tumeweka, walikuwa wanasema haipo, sijui vitu gani tumerekebisha lakini bado huduma hii haijarudishwa. Wanaohusika wamesikia, ndugu zangu wa Izimbya wamesikia, wa Rubale wamenisikia, wa Kibirizi wamenisikia, ikaja Bajeti ya Wizara ya Afya tutashikana mashati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru pia Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa mpango ambao wameanzisha. Idara Maalum imeanzishwa katika Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Naibu Mkaguzi Mkuu, kazi yake ni kusimamia fedha za Serikali za Mitaa kwenye Halmashauri. Kuna ubadhirifu kule tuongeze bidii, hiyo Idara iliyoanzishwa ianze haraka isimamia fedha za Serikali zinazokwenda kwenye Halmashauri. Zimekwenda fedha kwa ajili ya mradi wa Hospitali, kazi hii ifanyike, imekwenda fedha kwa ajili ya shule, kazi hii ifanyike, imekwenda fedha kwa ajili ya barabara, kazi hii ifanyike isiingie mikononi mwa watu wachache ambao ni wajanja. Kazi hii ifanyike, Idara hii ianze mara moja, isimamie fedha za Serikali vizuri kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imebaki dakika moja, muda uliobaki hautoshi kwa pointi iliyobaki niishie hapo. Naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rweikiza kwa kutumia muda vizuri.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii jioni hii ya leo ili nami niweze kuchangia hotuba ya Bajeti kama ilivyowasilishwa.

Kwanza, bajeti yenyewe naiunga mkono asilimia 100. Naiunga mkono kwa sababu imejielekeza yenyewe kwenye vipaumbele ambavyo hata mtu yeyote yule anavilenga. Inajaribu ku-*address* umaskini wa Watanzania walio wengi, inajaribu kuona wapi unafuu wa maisha unaweza kupatikana, ili bei ya bidhaa ziweze kushuka, Serikali imekuja na wazo la kuhakikisha kwamba tozo la mafuta linatolewa, hilo ni wazo zuri, naipongeza Serikali. Ukishapunguza zile tozo za mafuta ina maana kwamba gharama za usafirishaji zinapungua, gharama za nauli za bidhaa zenyewe zinapungua kwa hiyo, bei ya bidhaa inakuwa inashikika kweli kweli vilevile itachochea uwekezaji ndani ya viwanda na kilimo na viwanda vidogo vidogo. Kwa hiyo, ndio sababu hasa naiunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile imeendelea kujibu matatizo ya wanafunzi wetu Vyuo vyetu Vikuu nchi nzima wanagoma, wanaandamana na imesema kwamba asilimia nne ya hii *Skill Development Levy* iingie kule ili kukidhi bajeti ambazo zilikuwa zimekosekana kwa ajili ya vijana wetu. Kwa hiyo, nayo ni sababu ya kuipongeza Serikali hii sikivu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda hapo niiambie Serikali labda kupitia ile Kamati iliyoundwa, zile *grade* za wanafunzi kupata mikopo wengine asilimia 100 wengine 60, wengine 80 hata kama tutakuwa na fedha za kutosha bado itaendelea kutuletea tatizo. Kwa hiyo, naomba hicho kipengele kwa kweli Serikali izidi kukiangalia ili kuwe na *flat rate* iweze kueleweka. Maana inapendekezwa kwamba wanafunzi wanaosoma Sayansi waweze kupata asilimia 100, wale wengine wanaosoma Utamaduni wapate asilimia 50 lakini hata mtu wa Sayansi akitoka huko si anahitaji kuchezo muziki si anachezewa na hawa hawa ambao hawakupewa mikopo iliyotimia? Kwa hiyo, naomba haya nayo Serikali iweze kuyaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye bajeti yenyewe, nilikuwa nimesubiri kitu kimoja tu, niangalie bajeti ya Kambi ya Upinzani inasema nini, nilikuwa nataka nione wao wataendeshaje nchi, lakini napenda kumpongeza Mheshimiwa Zitto kwa kumuunga mkono Mheshimiwa Mkulo kwa kiwango cha hali ya juu kabisa. Bajeti ya Zitto Kabwe inasema itakwenda kukopa nje 3.9 trilioni kama misaada na mikopo. Mheshimiwa Mkulo anasema na yeye atakopa shilingi 3.9 trilioni kwa hiyo, ngoma *droo.* Serikali vilevile imejielekeza kwamba itakwenda kukopa 1.2 trilioni kutokea vyanzo vya ndani lakini Kambi ya Upinzani na yenyewe itakopa 1.2 trilioni, kwa hiyo, nayo

wamelingana tena. Sasa kama wamelingana sioni tofauti, ilichobaki sasa pale ni *structure* tu kwamba matumizi yawe hivi, ni suala la *numbers.* Nilifikiri kwamba wao wataendesha nchi bila kukopa kwa sababu nimekuwa nikisikia *comments* zao zikisema kwamba Serikali hii imepanga 1.9 trilioni kulipa madeni kwamba ni kosa, kwamba ni bajeti ya kulipa madeni lakini nchi iliyoendelea yenye ustaarabu kama ya Tanzania, kama ukikopa unalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri sasa uchaguzi umekwisha, Watanzania wanataka maendeleo, Chama cha Mapinduzi kimepewa ridhaa ya kuendesha nchi. Sasa kuna watu bado hawajui kama Tume ya Uchaguzi ilishatoa matokeo. Kuna watu bado wanafikiri kwamba Tume ya Uchaguzi haijatoa matokeo. Wako watumishi ndani ya Serikali yetu hawasimamii vizuri maendeleo ya nchi, Chama cha Mapinduzi kimeshapewa Ilani ya kuongeza nchi. Wasimamie fedha zinazokwenda kwenye maeneo yao ili Chama cha Mapinduzi mwaka 2015 turudi kama tulivyo, kwa sababu mtu usimnyang'anye nafasi yake. Kwa hiyo, napenda nidhamu ya kazi idumishwe, Serikali ichukue hatua kuondoa mambo ya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya vijijini vyetu aidha, Diwani, Mbunge, au Mwenyekiti wa Kijiji kuna watu bado wanapinga miradi ile ya kujitolea kwenye maeneo yao. Wanahamasisha watu wasijitolee, kwa hiyo, fedha zinazopelekwa na Serikali zinashindwa kukidhi utekelezaji wa miradi hiyo. Sasa Serikali lazima itoe onyo na iwaelekeze wananchi kwamba kinachotekelezwa jamani ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo asilimia 20 ya Watanzania lazima wachangie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vipaumbele vilivyoainishwa, mimi naiunga mkono Serikali ilivyokuja na mtazamo huu wa miundombinu. Umeme ni kitu muhimu na nina imani kwamba hata hizi MW 1700 zinazotafutwa ingawa fedha zake ndani ya bajeti sizioni sana lakini nina imani Serikali inajua pa kuzipata. Ndani ya Jimbo langu kumeanzishwa Wilaya ya Buhigwe ambayo nayo kulingana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, inabidi iwe na umeme. Kwa hiyo, nina imani Serikali imelichukua hilo na inalifanyia kazi, msije mkasahau mkifikiri kwamba hatusomi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu, jana wametoa majibu mazuri kabisa. Naomba niishukuru Serikali, kwa kweli Mkoa wetu wa Kigoma ulikuwa umetengwa, ulikuwa haujawa *connected* lakini napenda kushukuru Serikali siku ya leo na niwatangazie Watanzania kwamba Kigoma mtu alivyokuwa anaifikiria katika miaka miwili, mitatu siyo kama anavyoifikiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kujenga barabara ya Mwandiga kutoka kwa Mheshimiwa Zitto kuja kwangu. Manyovu kilometa 60, nafikiri Rais atakwenda kuifungua, tunamshukuru sana. Anakwenda kufungua Daraja la Mto Malagarasi, ambalo lilikuwa ndio kikwazo kwa watu wa Kigoma ili tuweze kupitia Tabora na kwenda nyumbani. Kwa hiyo, kwa ile barabara tunaishukuru Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru Wizara jana imetoa majibu mazuri kwamba kuanzia Kidahwe mpaka Nyakanazi, barabara ile Mheshimiwa Magufuli alitoa mfano mzuri akasema ukitaka kunyoa kichwa unaweza kuanzia kunyoa kuanzia popote pale lakini ilimradi unanyoa. Kwa hiyo, tunamshukuru kwamba nayo ataifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko barabara moja ya lami ambayo inatokea Burundi ambayo imeunganisha kati ya Mwandiga na Manyovu, nayo tunapenda ile lami itoke Manyovu kuja Kasulu ili iungane na itakayokwenda Nyakanazi kupitia Kibondo tuwe tumekamilisha ule mzunguko. Kwa hiyo, naiunga mkono kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naipongeza Serikali kwa suala la maji, ni kilio cha Watanzania. Nachofikiria kifanyike hapa, Serikali niishauri kwamba kuwe na *database* kuonesha kwamba katika kijiji fulani *source* ya maji iko wapi, hata kama havifanyiki. Kuwe na *database* tunapopata fedha tunajua kwenye Kata ile tutawekeza mahali fulani kama tuna visima viwili tunakuwa *database*, watu wafanye *research* tujue maji yako wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Manyovu lina Hospitali moja ya Wasabato inaitwa *Heri Mission*, ni kubwa, ni nzuri na ndio tunayoitegemea. Kwa hiyo, tunategemea *through PPP* Wizara ya Afya ione namna gani iwaunganishe Watanzania ili akina mama, watoto na wazee waweze kufaidi matunda ya Chama cha Mapinduzi kwamba wazee na watoto watatibiwa bure wanapokwenda hospitali. Sisi tunazidi kupata matatizo pale kwa sababu gharama ni kubwa, tunaiomba nayo iunganishwe mara moja, kama Serikali inavyojulikana kwamba ni sikivu na mimi naiamini hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye kilimo, eneo la Manyovu, Mkoa wa Kigoma tunalima sana ndizi na kwa kuwa tulikuwa hatuna miundombinu, ndizi za Manyovu zikitoka kule zikifika Tabora zinageuka za Bukoba. Kigoma ina ndizi nyingi sana ila zikifika Tabora kwenye treni zinaungana na za Bukoba zikija Dar es Saalaam tunaita ndizi za Bukoba. Kwa hiyo, miundombinu hii inavyofunguka mtaanza kula ndizi za Manyovu na mnakwenda *super market* mnasema tunaomba ndizi za Manyovu. Tunalima sana ndizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo, Serikali niishauri, vijijini tuna matatizo ya Maafisa Kilimo, hawapo. Watu wanalima kwa utaratibu wao, tuweke hao wataalam, wawashauri wazee wetu na sisi wenyewe ambao ni wakulima. Naomba Serikali iwakopeshe wakulima mbegu siyo lazima muwakopesha hela, wakopesheni mbegu bora ili waweze kuvuna kwa tija kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko ya mipakani. Jimbo langu lote ni mpaka wa Tanzania na Burundi. Burundi sisi kwetu hatuioni kama ni nchi nyingine, tunaiona kama ni kijiji kingine. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ituwekee masoko ya mipakani pale ili iweze kuwa na tija hata kama Serikali inachukua kodi, sisi tunavusha vitu kupeleka kule, tunataka waje wao wachukue kwetu ili na sisi tuweze kupata kodi. Pia tunaomba watusaidie viwanda hapo ili tuweze kwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano, juzi niliteta kidogo na Naibu Waziri, sikumdokeza sana lakini namshukuru sana alinipa jibu akasema ziko sehemu nyingi kwenye maeneo yetu ambayo yameonesha kwamba asilimia 22.1 inachangia pato la Taifa. Sasa kuna maeneo mengi kama kule kwangu bado watu wako mipakani, *network* hakuna. Kwa hiyo, tunaomba tushauri ile minara ambayo Serikali inajaribu kutoa ruzuku kwenye hawa wenye mitandao basi wawasaidie kupeleka kule nako tuweze kuwa na minara kwa sababu kule kuna vijiji karibu 16 watu hawapati mawasiliano, Kata ya Muyama, Jimbo la Manyovu. Naomba kwa kweli suala hilo lipewe kipaumbele kwa sababu nililiahidi na kwa kuwa unampenda Obama sina uhakika kama utaniangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vyeti vya uraia, naomba niishukuru Serikali kwa kuleta vyeti vya uraia kwa sababu sisi kule tuko mpakani na saa hizi tunaulizwa majina wewe nani, Balozi nani, Diwani nani, kwa sababu hatuna vyeti vya uraia, sasa Kigoma ikishapewa hivyo vyeti basi wananchi wetu watakuwa wameshapona na hilo. Wananchi wale wanaona ni usumbufu, wanagombana na Maaskari bila sababu na kwa kuwa Chama cha Mapinduzi na Serikali yake mmeliweka kwenye bajeti, naomba niwapongeze. Nina imani Serikali imeliona suala la ajira za vijana, kwa kweli ni tatizo na imekuja na mkakati wa kujenga *VETA* karibu kila Wilaya. Kwa hiyo, nalo nilipongeze, naomba tusirudi nyuma, twende nalo kwa utaratibu ambao kwa kweli ni *serious* kidogo ili tuweze kulisukuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile faini ya elfu hamsini itachochea rushwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Ya kwanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi, baada ya hapo, naomba niunge mkono hoja, twende tukafanye kazi. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa, sasa nitamwita Mheshimiwa David Ernest Silinde na baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mwidau na baadaye Kangi Ndege Lugola. Mheshimiwa Silinde!

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2010/2011, Hali ya Uchumi wa Taifa 2011, Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo tungeanza nalo katika kujadili bajeti hii, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Bunge la mwaka jana lilipitisha Mikoa mipya minne na Halmashauri mpya saba ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya

Momba ambalo ndiyo Jimbo langu la Mbozi Magharibi, lakini katika mapitio ya vitabu vyote hata ukipitia kitabu cha *public expenditure supply votes, regional* cha mwaka huu wa fedha hizo Halmashauri hazijaonyeshwa. Wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi wamenituma, wameniambia nije niwaeleze Chama cha Mapinduzi kwamba, je, Sera ile ilitumika kwa ajili ya kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu ili wapate kura na baada ya hapo wawaache, wamenituma hivi kwa sababu ni wazee wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuwa anafanya majumuisho, atueleze ni kwa nini walitangaza Halmashauri mpya, Mikoa mipya, Miji mipya na sasa bado hawajaziweka katika mwaka huu wa fedha 2011/2012. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningeona ni lazima tulifanyie mabadiliko ili niweze kuchangia hotuba yetu na ili Watanzania waweze wakamwelewa vizuri Mheshimiwa Waziri, ni lazima tuainishe yale maeneo ambayo Watanzania wanahitaji kutusikiliza. Kuna maeneo mengi, hofu yetu si namna bajeti inavyoandikwa, hofu yetu itabaki kuwa palepale, tutaendelea kuonyesha namna ambavyo bajeti za nyuma hazikufanikiwa na hii iliyopo sasa na hofu ya baadaye ni wapi tunapoelekea. Lakini vilevile ni lazima tuoanishe miaka hamsini ya uhuru na mwaka huu wa fedha ili tunakoelekea mbele tuwe na mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokosoa hivi, haina maana kwamba hatujaona yale yaliyofanyika miaka hamsini, lakini kikubwa tunajaribu kuangalia ni kwa kiwango gani yamefanikiwa. Kwa hili, lazima niwape wazi kwamba lazima mjue kitu kimoja, katika maisha ya kawaida kuna mambo mawili, kuna ku-*succed* na ku-*achieve* yaani kufikia lengo na kupata tu. Sasa unapokuwa na maendeleo ambayo nikitolea mfano, nikasema Mheshimiwa Mwenyekiti nakupatia milioni moja na Mheshimiwa Waziri Mkuu nakupatia milioni moja, mwisho wa mwaka huu nikiwaambia mniletee milioni moja na nusu, lakini inapofika mwisho wa mwaka Mwenyekiti unaleta milioni moja na elfu tano, Waziri Mkuu analeta milioni moja na laki sita, tunasema wewe ume-*archive* lakini hujafikia lengo, Waziri Mkuu ame-*achieve* lakini amefikia lengo. Ndiyo maana tunapozungumzia miaka hamsini tunaoanisha na wenzetu wa Kenya, tunaangalia wenzetu wa Rwanda ambao walikuwa katika mapigano ya muda mrefu na sasa hivi wako wapi, ndiyo miaka hamsini tunayo i-*compare* sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hicho tu wala si hoja nyingine na watu wasijaribu kujenga hoja kwamba mtu ametoka Chuo Kikuu moja kwa moja ameingia Bungeni, ni maendeleo, si maendeleo kabisa kwa sababu mimi siwezi kuona *impact* hapa, lakini tunachojaribu kuainisha ni Watanzania wanalionaje na wanahitaji mabadiliko katika kiwango gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia suala la bajeti kuna eneo moja linahusu maboresho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua nyinginezo za mapato, hapa ndiyo kuna tatizo ambalo na mimi wamenituma watu wa Mbozi na nimesema nitaliwasilisha leo jioni, kuhusiana na Sheria ya Usalama Barabarani. Kwa kweli nimejaribu kutafakari,

kutafuta ni kigezo gani Serikali ilijaribu kutumia kigezo gani kutoa faini ya shilingi elfu ishirini mpaka shilingi laki tatu za Kitanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Mtanzania gani ana uwezo wa kutembea na laki tatu kwa wakati mmoja? Wakati tukiangalia pato la mtu mmoja mmoja ni kwamba, Watanzania wanaishi chini ya dola moja na asilimia kubwa ya Watanzania ndiyo wanaotumia huu usafiri kwa sababu unapozungumzia faini ya usalama barabarani unazungumzia baiskeli, pikipiki, bajaji na taxi na mabasi, je, Taifa hili tunalipeleka wapi? Kwa sababu kitu cha kwanza tunachotakiwa kujaribu kukijenga ni kuangalia faini ya shilingi elfu ishirini ilipokuwa inatolewa je, iliifikia Serikali? Kama ilishindwa kuifikia ni sababu gani ziliifanya shilingi elfu ishirini zilizokuwa zinatolewa zisiifikie Serikali? Lakini kama sasa Serikali inajaribu kutumia faini, kwa maana makosa ya Watanzania kama chanzo cha mapato, hatuna Serikali, mapato haya sio halali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo mapato sio halali kwa sababu hutakiwi kutafuta makosa na unasema ndiyo moja ya chanzo cha mapato ya Taifa hili, watu wa Mbozi hawataki vitu kama hivi, watu wa Mbozi wamenituma hili na tumesema hatuhitaji kuendelea na maisha ya namna hii. Kwa hiyo, Serikali lazima i-*twist*, lazima mbadilishe kwa sababu wanaolipa hizi faini sio mabosi wanaomiliki yale magari, wanaolipa hizi faini ni madereva na mimi kama namiliki gari, dereva wangu akishindwa kutekeleza kitu namfukuza kazi. Maana yake tunawapeleka Watanzania wakose ajira, tutafanya watu washindwe kuingia katika ajira za biashara za usafiri na wakati huo huo naona jiji la Dar es Salaam wanafunzi wanakaa tangu asubuhi mpaka saa kumi na mbili wanakosa usafiri wa kwenda mashuleni, unategemea nini? Tutaongeza nauli ili tulipe hizo faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni ushuru wa mafuta ya petroli. Hapa hatujaeleza kwa uwazi, Watanzania wanataka kusikia ni kwa kiwango gani tunaweka katika huu mwaka wa fedha, tusiseme tu tutakwenda ku-*regulate*, tuta-*regulate* nini? Tuki-*regulate* asilimia moja ambayo haitakuja kusaidia hili Taifa tutafika wapi? Maana yake hii hali ndiyo itakwenda mpaka Mbozi Magharibi. Lakini kwenye suala la mafuta lazima tuchukue moja kwa moja, maana yake kuna *issue* moja mmezungumzia kwamba tuongeze bei ya mafuta ya taa ili iweze kulingana na mafuta ya petroli pamoja na ya *diesel* ili tuweze kuzuia uchakachuaji. Sisi tunasema hapana, kwa sababu mafuta ya taa ni kitu cha kwanza kumsaidia Mtanzania mnyonge, uchakachuaji tunaweza tukausaidia kwa kutafuta bei linganishi, mafuta ya petroli pamoja na *diesel* yashuke ili Kamsamba, Ndalambo, Tunduma na maeneo mengine bei iweze kulingana, lakini sio kutoa bei ya mafuta ya taa chini ipande juu. Hapo tutakuwa hatupeleki Taifa kunapotakiwa. Kwa hiyo, hili nafikiri Serikali vile vile lazima iliangalie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine, watu wa *NGO's* wametutuma kwamba, wamesema Serikali ya Chama cha Mapinduzi, maana yake mimi pale Mbozi nina *NGO's* kama mbili tu, hamjatambua mchango wao *NGO's* (*Non Governmental Organisations)* ndiyo maana mmekwenda kuifutia hii kodi? Ina maana na wao waache sasa kushirikiana kwa sababu kuna majukumu ambayo Serikali inashindwa lakini hizi Taasisi Zisizo za Kiserikali ndiyo zinaisaidia Serikali, sasa leo tunazikandamiza kwa kuziwekea kodi, unategemea watafanya nini? Maana yake kodi yenyewe ndiyo tukienda

bandarini ambako tozo au ushuru wake hauna malengo yoyote, mizigo inachelewa kufika na matokeo yake watu hawayafikii yale malengo. Kwa hiyo, ndugu zangu tujaribu kuweka mambo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naomba nizungumzie kilimo. Ukiongeza uzalishaji, *if we produce* hata leo ukitokea mtikisiko wa uchumi katika hili Taifa bei ya chakula haitapanda. Tuna ardhi ya kutosha, tuna mabonde ya kutosha, Kamsamba tunayo kule, utakwenda Iyendwe kuna mifumo ya maji ya kutosha, tuna maziwa, mito, tuna kila kitu, lakini kwa nini bei za chakula zinapanda? Ni kwa sababu tumeshindwa kuwekeza vizuri katika kilimo, ndiyo maana Serikali lazima ijue; wekeza vizuri katika kilimo, kwa mfano, majirani zetu pale Malawi, wao wamewekeza vizuri na leo Malawi ndiyo nchi ambayo inaongoza kwa Afrika kusafirisha mahindi katika nchi za jirani za….

**TAARIFA YA SPIKA**

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ili niweze kumpa taarifa ambazo zitamsaidia mchangiaji aliyekuwa akiongea kuhusu jitihada za Serikali kwamba hatujafanya jitihada za kutosha kuwekeza katika kilimo. Naomba nimjulishe Mbunge, Mheshimiwa Silinde kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zinapiga hatua sana, sasa hivi kiuchumi kutokana na uwekezaji *tactical* ambao umekuwa ukifanyika katika sekta ya kilimo na sekta nyingine na hii ndiyo maana imetuwezesha kufikia ukuaji wa uchumi wa asilimia saba kwa takriban miaka mitatu mfululizo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wanapenda kubeza takwimu hizi, lakini kwa bahati mbaya sana pengine hawajui zinapatikana vipi, pengine wangefanya jitihada za kuzifahamu vizuri ili waweze kujenga hoja zao huku wakiwa wako *informed* kiasi cha kutosha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge nadhani umemaliza.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa akiongea anatoa taarifa za kwamba Rwanda uchumi wao umekuwa kwa kasi sana kuliko wa kwetu, bila shaka hana taarifa kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo uchumi wake unapanda kwa kasi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge unachukua muda mrefu ni kama vile unachangia. Suala la taarifa linakuwa kwa kawaida ni fupi na ambalo linakwenda sambamba kabisa na mchango wa aliyekuwa anazungumza. Sasa kwa kuwa angalau umeguswa umechukua muda mrefu kuzunguka mbali, lakini umegusa eneo ambalo amelizungumza, sasa Mheshimiwa Silinde taarifa imetolewa, sijui unaipokea au unaikataa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Nzega wanamsikiliza Kigwangala na kwamba taarifa yake sihitaji kwa sababu hanisikilizi vizuri.

**MWENYEKITI:** Endelea kuchangia.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nitazungumzia dhana ya kilimo, ukizungumzia kilimo, hatujayapinga lakini tunachojaribu kuweka ni changamoto ili Serikali ijaribu kuboresha, ndiyo nia yetu wala hatuna kitu kingine kibaya. (*Makofi*)

Sasa mtu anapojaribu kutojua wakati anajua ukweli watu wa Nzega wamechakachuliwa mbolea, watu wa Nzega hawajapata pembejeo mwaka huu, lakini anazungumza vitu kama hivi, Nzega watamwelewa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mbozi wanajua ninachokizungumza kwamba, mfumo wa mbolea ulivyoharibika ndiyo haya tunayosema hayajaweza kunufaisha Watanzania. Sasa tunataka bajeti ya mwaka huu wa fedha iweze kulirekebisha hili, sio mtu unakwenda tu unapeleka mambo bila kuwa na mwelekeo mzuri. Kwa hiyo, hili ndiyo tunataka tuliweke sawa, kwamba tuzalishe vya kutosha, tuwe na vifaa vya kutosha, mfuko uboreshwe, tununue chakula cha watu wetu, tuongeze pato kwa Watanzania maana matokeo yake tunawasaidia Watanzania, Taifa na uchumi, pato vyote kwa ujumla vinakuwa. Kwa hiyo, hapo tutakuwa tumefaidika sisi wenyewe, hatumharibii mtu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la afya. Afya kwa mujibu wa bajeti ya mwaka huu imeongezewa asilimia 0.3 ukilinganisha na bajeti ya mwaka jana. Unajua kabisa hili Taifa yaani wewe mwenyewe unajua kabisa kwamba ukienda Kamsamba, ukienda kwa ndugu yangu Mheshimiwa Lukuvi kule Ismani, unajua ni kwa kiwango gani Watanzania wenyewe wanavyo-*suffer* kwa kukosa huduma bora za afya. Lakini tumeweka kidogo, leo ilipotokea bahati tu Babu wa Loliondo katokea niambie ni Watanzania wangapi wamekwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu katika hospitali zetu tunakosa zile huduma za msingi, ndiyo maana watu wanakimbilia kule, mwingine katokea Lindi, Tabora, Mbeya, unategemea nini? Yaani hizi tunasema ni *indicators* kwamba Taifa linahitaji huduma bora za afya ili watu wake wasiwe watu wa kuhangaika, ndiyo tunalolihitaji. Sasa katika mazingira ya afya, tunahitaji sasa hata bajeti Mheshimiwa Waziri, ajaribu kuiangalia upya. Watu wa afya vile vile wanalalamika kwa sababu Mdhamini Mkuu wa afya ni Serikali na wala si mwingine kwani watu wanalaumiwa Madokta na Manesi kwamba hawatendi kazi vizuri, lakini kiuhalisia *guarantor* wa afya ni Serikali na ili Madokta wafanye kazi vizuri ni kuwatengenezea mazingira mazuri na Watanzania wataridhika, mwaka huu tupeleke madawa ya kutosha ili watu wasiilaumu CCM kama mnavyofikiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utanifidia ule muda mrefu sana ambao huyu bwana aliutumia kuhutubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimalizie kwenye uvuvi. Jamani tunatakiwa tuseme Nchi ya Maziwa Makuu, hatusemi Nchi za Maziwa Makuu ni Nchi ya Maziwa Makuu, iko moja, ni Tanzania tu wala nchi zingine hazina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungukwa na bahari, maziwa, maliasili na kila kitu lakini suala la uvuvi bado halitunufaishi vya kutosha. Mheshimiwa Magufuli alijaribu kugusia kipindi kile akawakamata tu wale mabwana mpaka leo wako jela, meli moja *two billion point something*, thamani ya samaki waliokuwa mle, je si tungewekeza vya kutosha? Kwa hiyo, sasa hii inaweza ikawa moja ya chanzo cha pato la Taifa ambacho kitaweza kutusaidia. Mbozi kule kwetu kwenye Kata ya Ivuna, tuna Ziwa Rukwa, Watanzania wamewekeza pale wanajaribu kuvua samaki, lakini unakuta baadhi ya watu wachache wanakwenda kuwakamata wale watu, wanawavunjia mitumbwi yao, wanawakatia hata neti bila kuwapa hata elimu mbadala, Watanzania wanakosa ajira, leo utawaeleza kabisa kwamba CCM ni nzuri kweli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanahitaji wajue CCM ni nzuri, Zanzibar wawe wanafaidika na uvuvi, Lindi wawe wanafaidika na uvuvi, hata tunahitaji tupeleke samaki huko kwa watu ambao hawana maziwa wala mito au bahari. Kwa hiyo, katika uvuvi tukiwekeza kwa kiwango kikubwa, pato la Taifa litaongezeka kwa kiwango kizuri kama nchi za wenzetu wanavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mkullo, Waziri wa Fedha pamoja na Waziri Mkuu jaribuni kuangalia yale ya msingi ambayo sisi tunajaribu kuyajenga kwa sababu Watanzania walioko nje wana akili kuliko hata sisi, sisi tumepata tu bahati ya Mwenyezi Mungu kuwa wawakilishi wao, tusitumie nafasi hii vibaya kuhakikisha tunaendelea kuliangamiza Taifa hili. Taifa ni letu, tunalipenda kwa kadri Mwenyezi Mungu alivyotupatia na tunaamini tutalipigania mpaka dakika ya mwisho, kwa sababu kila mtu atakufa, lakini tunachotafuta ni mchango gani utautoa ili unapokufa watu wakuzike vizuri kama Mwalimu Nyerere ambavyo leo tunamheshimu wote, sawa jamani. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ndugu zangu kwa hili nafikiri ujumbe umefika, maana yake nikiona mmetulia hivi, maana yake mmeelewa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa muda wa kufidia ulionipa. Kwa kweli siwezi kuiunga mkono bajeti hii mpaka masuala ya msingi yatakapokuwa yamefanyiwa kazi.

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Silinde, kijana lakini Samunge bwana waliokwenda wametoka India, London, Kenya, Uganda na kwingineko, kwa hiyo, wametoka katika sehemu mbalimbali kwenda Samunge, sio kwamba Serikali haijatoa mchango katika eneo hilo la afya. Tunaendelea, anayefuatia sasa ni Mheshimiwa

Mwidau, halafu atafuatia Mheshimiwa Kange Lugola na Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis ajiandae.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kuwa mapendekezo haya ya bajeti yalipokuwa yakiwasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ukiangalia kwa juu juu na kwa wale Watanzania ambao waliweza kumsikiliza kwa tafsiri ya haraka haraka waliona kuwa bajeti hii itamwokoa mwananchi wa Tanzania, lakini ukienda kwa undani zaidi au kwa hali halisi ilivyo, bajeti hii ni ile ile hakuna tofauti na bajeti iliyopita, *no any significant deviation from previous budget.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ukiangalia kwa makini waandaaji ni wale wale, *style* ni ile ile ya ku-*copy* na ku-*paste*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kuwa mfumo wa bajeti na uandaaji wake kwa kweli una matatizo ya kimsingi, sipendi kuingia ndani katika hili kwani kuna wachangiaji ambao wamegusia katika jambo hili, naomba nielekeze mchango wangu katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika mambo ambayo yalizingatiwa katika uandaaji wa bajeti hii na naomba kwa ruhusa yako niyataje, ambayo ni Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, MKUKUTA awamu ya pili, Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015, Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA), Mkakati wa Taifa wa Madeni, Sera za kijumla za uchumi kwa mwaka 2011/2012. Naomba katika haya nielekeze mchango wangu katika MPAMITA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MPAMITA ambao ni Mpango wa Pamoja wa Misaada Tanzania, mpango huu uliandaliwa au ulizinduliwa mwaka 2006. MPAMITA ulikuwa na malengo ya kuweza kuipatia Tanzania misaada na mikopo nafuu yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MPAMITA kwa mwaka wa fedha 2006/2007 ulitarajiwa kuipatia Tanzania mkopo, msaada wa bilioni 2.05. Kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008 ulitarajiwa kuipatia Tanzania dola za Kimarekani dola bilioni 2.09. Kwa mwaka wa fedha 2008/2009 ulitarajiwa kuipatia dola bilioni 2.06 na mwaka wa fedha 2009/2010 ilikuwa ni dola bilioni 1.95. Hapo sasa ndiyo pa kujiuliza, je, fedha zilizoahidiwa na wahisani mbalimbali zimepatikana kama zilivyotarajiwa? Kwa sababu tunasikia wahisani walipunguza misaada au kuweka masharti magumu. Nadhani suala hili Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho ataweza kutufafanulia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumemsikia Waziri wa Fedha akisema MPAMITA safari hii kuna vitu ambavyo vimezingatiwa katika utengenezaji wa bajeti hii. Sasa hapa ikiwa Serikali inaendelea kutekeleza MPAMITA, je, imefikia makubaliano

mengine na washiriki wetu wa maendeleo hasa kwa makisio ya misaada wanayotarajiwa kutoa kwa miaka mitano ijayo? Nadhani Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mkulo ataweza kutupatia ufafanuzi atakapofanya majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kupeleka mchango wangu katika Malengo ya Maendeleo ya Milenia, nikianza na umaskini. Tumesikia hapa wachangiaji mbalimbali wakisema kuwa uchumi umekuwa kwa asilimia saba kama alivyowasilisha Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake. Ukuaji huu haufanani na hali ya kipato cha Mtanzania. Jana tumemsikia Mheshimiwa Mdee akisema kuwa kuna pengo kubwa katika watu wachache walionacho na maskini wengi, hali hii vinakuwa siku hadi siku. Hii inaonyesha kuwa Watanzania wengi sana hawafaidiki na ukuaji huu wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, kule kwetu Tanga ambako natoka kwa mwaka 2010, nimepita katika kijiji kimoja wakati wa kampeni ambapo ilikuwa ni mwezi wa tisa, mwaka huo ilikuwa ni Ramadhani. Kwa hali ya mwaka jana ambapo wananchi wa kule Pande Juu, Kijiji cha Pande Juu mwezi wa Ramadhani wamefunga, jioni wanafutari uji kwa tende, tena tende za msaada. Hii inaonyesha ni kwa kiasi gani uchumi unaokuwa, unaoelezwa kwenye vitabu hauwasaidii kabisa, haufanani na kipato cha Mtanzania. Hali ya Mtanzania inazidi kudhoofika siku hadi siku. Vile vile tulikuwa na wananchi wa Kusini ambao walifikia mpaka kula mizizi. Kwa hali hii inaonyesha kuwa ukuaji huu wa uchumi bado haumsaidii mwananchi wa kawaida hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu za Benki ya Dunia zinaonyesha kuwa kwa kutumia kigezo cha mtu mzima ambaye akiwa anatumia chini ya dola moja basi ni maskini wa kutupwa. Kwa kigezo cha aina hiyo ambacho wametumia Benki ya Dunia, takwimu zao zinaonyesha kuwa umaskini Tanzania umepungua toka asilimia 73 ya Watanzania wote mwaka 1990 mpaka kufikia asilimia 68 mwaka 2009, takriban miaka 19. Miaka 19 ni mingi sana ukiangalia *percent* ambayo imepungua ya umaskini ni kama tano. Kwa kasi ndogo ya kupungua kwa umaskini Tanzania haiwezi kufikia malengo ya milenia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati malengo ya milenia ni pamoja na kupunguza kwa nusu asilimia ya Watanzania wenye njaa ifikapo mwaka 2015. Hali hii inatisha, hatuwezi kuwa na mshikamano wa Kitaifa wa kweli, hatuwezi kuwa na mshikamano wa Kitaifa ikiwa ukuaji wa uchumi unawanufaisha Watanzania wachache na kuwaacha Watanzania takriban milioni 29 wakiwa maskini wa kutupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielekee haraka haraka katika vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga. Hili pia tunafahamu ni lengo katika Malengo ya Milenia. Mheshimiwa mchangiaji aliyepita amesema hapa kwa kweli bajeti ya Afya ni ndogo sana, imeongezwa kwa asilimia *zero point* ambayo haiwezi kusaidia kufikia malengo ya milenia hasa ukiangalia jinsi ambavyo vifo vya watoto wadogo na mama wajawazito vinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya sana katika sekta ya Afya. Tunajikongoja lakini hali bado. Hivi karibuni tulionyeshwa katika vyombo vya habari,

hospitali ya Mkoa ya Bombo, kitanda kimoja wanalala wajawazito wawili mpaka watatu, ambao wakijifungua sasa wao wanalala chini, watoto wao ndiyo wanalala juu ya vitanda. Hali hii ni mbaya sana. Hali hii kwa kweli inamdhalilisha mama na sote tunajua hakuna kama mama. Tunaiomba Serikali iongeze bajeti ya Afya ifikie angalau asilimia 10 ya *total Budget.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vile vile nigusie katika vipaumbele. Kwa vipaumbele hivi ambavyo vimeainishwa katika mapendekezo ya bajeti, kama kweli kukiwa na utekelezaji madhubuti, kukiwa na ufuatiliaji angalau vinaweza vikachochea maendeleo, vinaweza vikachochea katika pato la Taifa. Lakini nina wasiwasi mkubwa hasa ukiangalia katika kupanua ajira. Katika kuongeza ajira hakuna mikakati madhubuti ambayo inaweza ikasaidia kwenye bajeti hiii, inaweza ikasaidia kufikia malengo hayo yaliyoelezwa humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigusie katika kilimo. Kilimo kwa kweli kinaimbwa kweli kweli, kilimo kinakwezwa kwa hali ya juu kwa kupitia *slogan* ya Kilimo Kwanza. Lakini ukiangalia kwa undani kilimo hiki kwa kweli ni kwa ajili ya wawekezaji wakubwa wa nje. Hakina maslahi makubwa kwa Mtanzania maskini wa kijijini. Ni njia ya wawekezaji wakubwa kutoka nje ambao watakuwa wanajishughulisha na kilimo cha mazao ambayo si lazima yaongeze kipato cha Taifa, vile vile kuongeza mazao ambayo ni ya chakula yatakayomsaidia Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mkakati wa kuongeza ajira. Unapotazama sekta zilizotengeneza ajira ya ziada, zilizotengwa kwa ajili ya kutengeneza ajira ya ziada siyo zile ambazo zinawanufaisha wananchi wengi. Mfano mmoja katika eneo moja ambalo linatazamiwa kuzalisha ajira ya ziada ni sekta ya kilimo katika mpango wake wa *SAGCOT*, Mpango wa Kilimo wa Ukanda wa Kusini mwa Tanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, muda wako umekwisha. Kama unaunga mkono hoja sema unaunga.

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Lakini nahisi kama umenipunja. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Mbunge. Baadaye utazoea, utaongea kwa kasi.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba unipe mwongozo kwa mujibu wa kifungu cha 68(7) na baadaye pia utaangalia (10) kuhusu Mbunge anapotoa taarifa kuhusu jambo ambalo anaona aidha linapotosha ukweli au linarudisha heshima ya Taifa katika mazungumzo ya Mbunge anayezungumza. Hii nimeguswa kufuatia Mbunge aliyepita kuzungumza kabla ya aliyekaa sasa, alipokataa taarifa ya kwamba Kilimo Kwanza kimeleta mafanikio makubwa hususan nikilinganisha

Mkoa wangu wa Ruvuma ambao ulikuwa unazalisha tani 20,000 kwa miaka ya nyuma, sasa imefikia tani 50,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, suala la mwongozo juu ya jambo kama hili wala halihitaji nitumie akili nyingi sana. Ni suala la takwimu. Takwimu ndizo zinazoweza kujibu. Nadhani kama tutazipata takwimu za ongezeko la kilimo kutoka Kilimo Kwanza tulipoanza na kilipofikia, nitatafuta utaratibu mzuri wa kutoa taarifa hiyo hapa. Waheshimiwa Wabunge tuendelee. *(Makofi)*

Anayefuatia sasa ni Mheshimiwa Alphaxard Ndege Lugola, atafuatiwa na Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamsi na baadaye Mheshimiwa Stephen Masele ajiandae.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti iliyoletwa na Serikali yetu humu Bungeni. Kwanza kabisa Waswahili wanasema kizuri chajiuza na kibaya chajitembeza. Bajeti hii iliyoletwa humu ndani ni bajeti nzuri na inayowatakia mema Watanzania wa nchi hii. Imelenga katika maeneo yote ya kisekta, kutatua matatizo ya wananchi na hata matatizo yale ambayo yanaletwa na CHADEMA na yenyewe pia yatashughulikiwa na bajeti hiii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema bajeti mbaya inajitembeza. Iko bajeti iliyoletwa humu kama bajeti mbadala, bajeti hii ndugu zangu inajitembeza. Kama mna kitabu cha hotuba ya bajeti kilichosomwa hapa kama bajeti mbadala. Mheshimiwa Zitto Kabwe, namnukuu, anasema: "Iwapo sisi tukiendelea kujilipa posho za kukaa humu ndani, posho za kukaa, huku ndiko kujitembeza. Katika lugha ya Kibunge neno *sitting* siyo kukaa, *sitting* ni kikao. Kwa hiyo, tunaposema *sitting allowance* tunamaanisha posho ya kikao na siyo posho ya kukaa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku ni kuwapotosha Watanzania kwamba Wabunge wanalipwa posho kwa kukaa. Ndiyo sababu nasema haya mambo ya kuiga unaweza ukaja na posho ambazo hata duniani hazijawahi kuwepo. Ndugu zangu CHADEMA, msiige kunya kwa tembo mtapasuka msamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema mambo mazuri sana kuhusu matumizi ya posho tunayodunduliza hapa. Tukitoka nje, naamini hata Mheshimiwa Zitto Kabwe anapokwenda Jimboni kwake, ndiyo posho hiyo hiyo ameitumia miaka mitano imemjenga na kumpa umaarufu wa kisiasa, leo anaibeza. Ama kweli shukrani ya punda ni mateke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Lema hapa tunakaa naye Arusha, tunaheshimiana. Kama kweli amefikia hatua ya kukiri hapa ndani kwamba alikwenda Nyamongo kuzuia maiti isizikwe, kwenda Nyamongo kugombea maiti, kama kweli hii ndiyo sera ya wenzetu CHADEMA, ama kweli mmekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazoea hujenga tabia. Namshauri ndugu yangu itafikia siku hakuna maiti za kugombea zinazotokana na matukio kama hayo. Atajikuta anakwenda kugombea maiti za vifo vya kawaida. Amepinga bajeti ya Serikali. Lakini namshukuru sana Mheshimiwa Lema ameunga mkono hotuba ya bajeti ya Kamati ya Mheshimiwa Kigoda. Mheshimiwa Kigoda ni Mbunge wa CCM. Ukimwunga mkono Mheshimiwa Kigoda, umeunga mkono bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimesimama hapa kwa niaba ya wananchi wa Mwibara kuwatetea na kuwalilia juu ya kilio cha muda mrefu cha umaskini. Wana Mwibara hawa maskini, wameandamwa na umaskini ambao ni adui mkubwa. Kama umaskini ni adui mkubwa, mapambano dhidi ya umaskini yanahitaji jeshi kubwa, kwa maana ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ukurasa wa 35 imezungumzia namna itakavyopambana na umaskini kupitia mikakati hii ya MKUKUTA. Naamini ni nia njema ya Serikali na itaendeleza mikakati hii. Lakini napenda niishauri Serikali juu ya jambo hili la vita dhidi ya umaskini. Ufike wakati sasa tuanzishe mamlaka ya kupambana na kuondoa umaskini Tanzania. Tumeanzisha mamlaka nyingi sana katika nchi hii, lakini eneo hili la kupambana na umaskini hatujalipa umuhimu mkubwa wa namna ya kupambana na umaskini na huku tukijua umaskini ni adui mkubwa katika nchi hii. Lakini tukisema MKUKUTA kupunguza umaskini, adui hatuwezi kumpunguza, adui ni kumwondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipopigana na Nduli Amini alikuwa ni adui, kwa maana ya kumpiga na kumtoa nje ya mipaka yetu. Naomba Serikali ianzishe Mamlaka ya kupambana na kuondoa umaskini, ili uondoke miongoni mwa Watanzania wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulimi wetu huu unaumba maneno ya kumfanya maskini aendelee kuwa maskini. Ulimi ni mbaya sana, hata kwenye Biblia, Mithali 18, Mstari wa 21, linasema uzima na mauti viko katika kuwezeshwa na ulimi. Maskini akiokota anaambiwa kaiba, maskini akipata anaambiwa matako hulia mbwata, ng’ombe wa maskini akizaa anaambiwa atazaa dume, mambo kama haya tukiyaacha yakaendelea umaskini hautatoka miongoni mwa Watanzania. Ulimi wetu haujaishia hapo, kila kukicha Viongozi, wanawakejeli wananchi wa Tanzania ambao ni maskini; maskini hakopesheki, mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe, mchagua jembe si mkulima, maneno haya tukiyaacha yakaendelea, umaskini hautatoka Tanzania. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ndio mtaji wa maskini na sio nguvu zake mwenyewe. Bajeti hii ndio itamkopesha maskini na sio maskini hakopesheki. Wananchi wa Mwibara wawe wavuvi, wawe wakulima, akinamama kwenye vikundi, kila wanakokwenda wanaambiwa hawakopesheki! Wanaambiwa mtaji wao ni nguvu zao wenyewe, watakwenda wapi wananchi hawa? Lakini dhana hii ya maskini hakopesheki ni ugonjwa mbaya sana! Hivi kweli tukianza kufanya *analysis,* kuna Mtanzania au shirika litakalokopesheka? Watu wanaokopa fedha ambazo tunazipitisha hapa leo, wanakopa

fedha zinazotokana na kodi ya maskini wa Mwibara ambaye yeye akitaka kukopa fedha hizo anaambiwa yeye hakopesheki!

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikopa *General Tyre* hapa kwa vigezo vya kwamba wao wanakopesheka, walikopa KIWIRA hapa kwa vigezo kwamba wao wanakopesheka, tena kwa dhamana ya Serikali, lakini kumbe na wao hawakopesheki! Wameshindwa kulipa mkopo na Serikali kama mdhamini anatakiwa alipe mkopo huu, fedha hizi zinatoka wapi? Bado zinatoka kwenye kodi ya Mtanzania, hii ni hasara kubwa sana. Mwalimu aliwahi kusema: "Ikitokea tukawa na Rais ambaye hana dini, tutatafuta namna ya kumuapisha". Nchi yetu ni ya matajiri na maskini, ufike wakati lazima kila mmoja akope, tutafute namna ya kumkopesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefika mahali kumekuwa na mgongano wa maslahi kati ya wakulima na wanyama. Lakini cha kushangaza maslahi ya wanyama, ndio yanapewa kipaumbele kuliko maslahi ya wananchi au binadamu! Wanyama wanapewa Sheria za kuwalinda, ukipita hata kwenye hifadhi muziki hufungulii mkubwa, wanawekewa matuta, samaki kule Ziwa Viktoria wanatungiwa Sheria wazaliane, lakini wananchi wanatungiwa Sheria ambazo zinawabagua. Ukienda Mbarali kule, kila kukicha, kwa ndugu yangu Kilufi, wananchi wanasogezwa kila wakati wapishe wanyama waweze kukaa, tunakokwenda ni wapi? Mbona hata hao wanyama bado tunaona wanatoroshwa wanakwenda kwa matajiri, wanatusadia nini? Itafika mahali sasa, kila mahali katika nchi hii kutazagaa wanyama; wananchi wapewe nafasi ya ardhi. Kunapotokea mgongano wa maslahi ya wanyama na samaki na binadamu, lazima maslahi ya wanadamu ndio yawe nambari moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mwibara kule hawana kipato, sasa hivi amboni moja ya mahindi wananunua 3,000/= debe wananunua 14,000/=, wavuvi ndio kabisa! Wakulima hawa wamejitahidi sana kulima pamba, lakini wamepelekewa pembejeo za dawa ambazo zimepitwa na wakati na kampuni ya *Baduu*, pamba yote imeungua kule, lakini hakuna anayemsemea mkulima. Wakulima mazao yao yanapounguzwa na jua hakuna anayewasemea, mtikisiko wa dunia kwenye uchumi umewatikisa kidogo wafanyabiashara, wamefidiwa hasara walizozipata; kwa nini wakulima wanapopata mtikisiko wa mazao yao na wao wasifidiwe? Wamemkosea nini Mungu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaendelea na vita dhidi ya umaskini kwa lele mama, hakika wananchi wetu hawatatoka kwenye umaskini uliokithiri. Nimeishauri Serikali, ianzishe Mamlaka kwa ajili ya kupambana na kuondoa umaskini Tanzania. Mamlaka hii ipewe majukumu ya kufanya na hii mifuko ambayo inawawezesha yote iende ndani ya Mamlaka. Mamlaka hii, iweze kufanya zoezi nchi nzima kutambua ni maeneo gani ambayo yako *marginalised*, huwezi ukaona maeneo mengine yana barabara 50 za lami, wakati kuna maeneo mengine ikiwemo Mwibara, hata lami hawajawahi kuiona! Huwezi ukafika maeneo mengine wana maji safi na salama ya kunywa, lakini unakwenda maeneo mengine hata maji ya kunywa hawana! Mamlaka hii itatusaidia kufanya uchambuzi katika nchi hii na kuja na kitu cha kuwasadia wananchi wote ili wote twende kwa pamoja ili wengine wasibaki nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia masuala ya umaskini kwa kuonesha na kwamba Serikali iwe na dhamira. Kama Mwalimu alivyosema kwamba, adui Nduli Amin, nia ya kumpiga tunayo, sababu tunayo na uwezo tunao; bajeti hii ni uwezo tunao. Serikali imeonesha hapa nia tunayo, kinachohitajika ni kuwaonea huruma maskini walioko kule, kinachohitajika ni kuhakikisha wale wote ambao wanachungulia fedha za maskini ambazo leo tunaziidhinisha hapa, washughulikiwe ili waone kwamba kuanzia sasa hakuna...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, muda wako umekwisha.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja, endapo pia Mamlaka hii ya kupambana na kuondoa umaskini itakuwa *in place.* Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge. Wakati mwingine kama muda hautoshi, tungekuwa tunatafuta vipindi kwenye *Television,* unapata muda mzuri, unasema mambo yote.

Basi tunaendelea. Anayefuatia sasa ni Mheshimiwa Haroub Muhammed Shams na baadaye atafuatiwa na Stephen Julius Masele na baadaye Pauline Gekul.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kuwa katika Bunge hili leo. Pia napenda kukishukuru chama changu, Chama cha Wananchi, kwa kuniamini na kunifanya mgombea wao katika Jimbo la Chonga. Pia nawashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Chonga ambao wameniwezesha kuingia katika Bunge hili. Naishukuru pia familia yangu kwa kuwa nami muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyowasilishwa mbele yetu ya mwaka huu wa fedha wa 2011/2012, kwa kweli, bajeti hii ukiitazama juu juu utaiona kama ina ukombozi kiasi fulani, lakini ukiitazama kwa jicho la ndani basi utakuta kuna upungufu mkubwa ndani yake. Bajeti iliyowasilishwa inaonekana haina uhalisia wa vitendo kwa sababu fedha zilizoainishwa kutumika katika bajeti hii inaonekana kama fedha hizi hazipo. Sasa inaonekana kama ni bajeti iliyopangwa kufurahisha tu, wananchi watulizane, lakini malengo kuna shida ya kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirudi nyuma kidogo katika bajeti hii iliyopita ya mwaka 2010/2011, Serikali ilileta bajeti ya kutumia shilingi trilioni 11.6 lakini mwaka sasa hivi unakwisha pesa hizi hazikupatikana na zilizotumika katika bajeti unaambiwa mpaka sasa ni shilingi trilioni 10.1 na kama mwezi huu ukimalizika basi inaweza kuwa trilioni 10.4. Imeonekana kama kuna upungufu mkubwa katika bajeti hiyo wa karibu au wa sawa na trilioni 1.5 ambazo ni pesa zinazoweza kuwa bajeti ya Wizara mbili au tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo limejirudia katika bajeti hii tunayoizungumza sasa ya mwaka 2011/2012 iliyoletwa bajeti ya trilioni 13.53 lakini programu inaonesha, ambayo inasimamiwa na *IMF*, kwamba Serikali ilitakiwa mwaka huu itumie trilioni 11.26 na *IMF* ni shirika ambalo linatusaidia katika programu zetu nyingi za kimaendeleo na usimamizi wa fedha katika mambo ya fedha ya ulimwengu. Sasa tunakuta katika bajeti mwaka huu kuna upungufu wa karibu au wa sawa na trilioni 2.27, ni pesa nyingi ambazo pia zitakosekana katika bajeti hii. Hapo ndipo ninapopata wasiwasi wa kwamba bajeti hii ina ugumu wa kuleta mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha au la kuhudhunisha kwa Serikali kuleta bajeti Bungeni, halafu bajeti hiyo ikawa haipo kiuhalisia! Hii inaonesha kama ni kulivunjia hadhi Bunge na halipewi haki yake kwamba linapitisha bajeti, halafu hakuna bajeti hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nigusie katika vyanzo vya mapato ambavyo Serikali inavitarajia kukusanya mapato kwa Mwaka huu wa Fedha. Vyanzo vilivyoainishwa ambavyo Serikali inatarajia kukusanya ni shilingi trilioni 7.12. Kwa kweli, naona pesa ni nyingi ambazo zinakusudiwa kukusanywa na haitegemewi kwamba zitapatikana, japokuwa ukiwekwa mkazo na nia madhubuti, nia ya dhati, ya kutaka kuwakomboa wananchi maskini wa nchi hii basi zinaweza zikapatikana na zikafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna tatizo. Katika matumizi pia ya hizo fedha tunashuhudia kuona kwamba fedha nyingi zikishakusanywa basi huwa hazitumiki kwa yale matumizi ya bajeti yaliyoainishwa katika bajeti. Kuna matumizi mengine ambayo yanakwenda kinyume na yale yaliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna vyanzo vingine vya mapato ambavyo Serikali bado haijavifanyia kazi vizuri. Naona inakusanya kodi kwa wafanyabiashara na tunaambiwa kwamba wako wafanyabiashara wakubwa karibu 400 ambao ni *large tax payers*, pia wapo wafanyabiashara hawa wa kati na wadogo ambao wanalipishwa kodi na Serikali kwa ajili ya kujaza Hazina. Wasiwasi wangu ni kuwa hawa wafanyabiashara wakubwa wanalipishwa kodi kiuhaliasia au kihakika! Naona kama mkazo mkubwa umeelekezwa kwa wale wafanyabiashara wadogo na wa-kati ambao mapato yao ni madogo na ya chini. Nadhani sasa Serikali ingeweka mkazo zaidi kukusanya kodi kwa wale watu ambao wana uwezo wa kulipa kodi, pamoja na kwamba wanapewa *incentives* nyingi za kupatiwa misamaha wanapoagiza malighafi za viwanda na mambo mengine. Basi Serikali pia itazame vizuri uwezo wao ili waweze kuchangia pato la nchi yetu na wale watu wa tabaka la chini wafaidike na uchumi wa nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie pia katika sekta ya uvuvi ambayo Serikali bado haijaitazama. Sekta ya uvuvi ikitizamwa vizuri kwa jicho la ndani na la maendeleo basi italeta mchango mkubwa katika mchango wa pato letu. Mheshimiwa Waziri, alituambia hapa jana sijui au juzi, kama kuna meli zinazovua katika bahari kuu na meli hizi zinavua samaki wakubwa aina ya jodari na wengine, karibu kila meli inavua

tani tano kwa siku moja. Hawa ni samaki wengi na wenye thamani kubwa. Ukiangalia kwa soko la ndani tu basi tani tano za samaki hawa ni zaidi ya milioni 20. Sasa kama Serikali inapata kodi au inapata leseni tu kwa meli hizi ambazo ni za dola 35,000 kwa maneno ya Waziri aliyotueleza hapa, naona kama tunaachia rasilimali zetu zivunwe na sisi tupewe tumbaku ya ugoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali itoze leseni hizi za meli kubwa za kivuvi za nje, leseni walau *minimum* basi iwe dola 60,000 kwa mwaka. Pia Serikali, ichukue mrabaha wa thamani ya samaki wanaovuliwa japo kwa 10% ili kuweza kusaidia mapato haya yaweze kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo wa nchi yetu. Lakini pia jambo zuri zaidi kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu, ni kuwawezesha wavuvi wa nchi yetu au wavuvi wazalendo. Kwanza, uchumi utabaki ndani ya nchi, vijana watapata ajira, lakini pia mazingira yatahifadhika. Tunajua, bila kuwa na mazingira mazuri basi uhai wetu sisi Wabunge na wananchi wengine pia uko hatarini. Hatuna uhakika meli hizi kubwa zinazovua huko ambazo sisi tunapewa dola 35,000 kwa mwaka, hatujui zinachafua mazingira kwa kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nigusie kidogo juu ya Mamlaka ya ukusanyaji wa Mapato katika nchi yetu, ambayo ni *TRA. TRA,* kuna malalamiko mengi makubwa ya kuwakamua sana watu au wafanyabiashara wadogo wadogo na hawa wa kati na malalamiko ya kuwaachia wafanyabiashara wakubwa, vijana wa mjini wanasema, *wakipeta,* yaani wanapata *exemptions* sana. Wafanyabiashara wadogo hawa utakuta mtu kaagiza kontena pengine la mali, wame-*share* watu 10 lakini mali ile itakaa bandarini miezi miwili. Kwa usumbufu wanaoupata au kwa kufanyiwa *up-lift* ya *value* ya mizigo ile kiasi kwamba wanashindwa kuigomboa. Badala ya kuwasaidia inakuwa tumezidi kuwakandamiza na kuwafanya wawe maskini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu, Serikali kupitia Wizara ya Fedha, chini ya Waziri wake Mheshimiwa Mkulo, itazame hili, wafanyabiashara hawa wadogo wadogo na wa ngazi za chini waweze kufanyiwa utaratibu mzuri wa mizigo yao ili waweze kukua. Utakuta wafanyabiashara hawa, mtu anafanya biashara miaka 10, 15 au 20, hana hata kibanda cha kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna malalamiko haya ya ulipishaji wa magari kwa kutumia *depreciation.* Magari yanathaminiwa *X–value price* ya gari jipya, halafu wanafanya *depreciation* sijui kwa kiwango gani, lakini habari ambazo ninazo ni kwamba gari lenye muda wa miaka 10 ambalo ni gari chakavu kabisa, linafanywa 35% ya bei mpya ya gari lile ambayo inakuwa ni thamani kubwa sana. Hapa tuone kwamba itakuwa bado tumewazidishia wananchi wetu umaskini badala ya kuwasaidia. Mtu gari la miaka 10, ni gari limechoka sana halafu linapewa *value* kubwa kiasi ambacho kwamba matumizi yake yeye atakayotumia ni muda mdogo na pia litakuwa linaharibu zaidi mazingira. Mchango wangu ni kwamba tuwawezeshe watu wetu waweze kuagiza magari mazuri ambayo angalau yametumika miaka mitano au sita, halafu kodi irekebishwe ili waweze kumudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusisitiza tu kwamba nchi hii ina rasilimali nyingi na rasilimali labda kubwa iliyopo ni watu, watu ni rasilimali kubwa sana, ndiyo rasilimali ya kwanza halafu ni ardhi. Tunavyo pia na vivutio kama dhahabu, madini, bahari, mito na maziwa, Serikali iweke mkazo ili hawa watu wetu wapangwe vizuri ili waweze kuvuna rasilimali hizi ili ziweze kufaidisha katika nchi yetu. Ikiwa watu wetu tutakuwa tunawaweka nyuma na tunawapendelea wageni basi siku zote tutakuwa tuko nyuma na rasilimali hizi zitavunwa ziondoke na tubakie maskini milele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mwongozo wa Mwenyekiti

**MWENYEKITI:** Mowngozo wa Mwenyekiti!

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kuhusu Kanuni ya 54(1)(a) na (g) wakati Mheshimiwa Mbunge wa Mwibara anazungumza...

**MWENYEKITI:** Hebu twende vizuri kidogo.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** *Okay!*

**MWENYEKITI:** Kifungu namba na hamsini na...

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Kanuni ya 54(1)(a) kwamba...

**MWENYEKITI:** Mmh mbona hakipo hicho?

**MBUNGE FULANI:** Kanuni ya 54 au 64?

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Namaanisha Kanuni ya 64(1). *Sorry* ambacho kinasema; "Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:- (a) hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli."

Mheshimiwa Lugola wakati anazungumza amesema kwamba Mheshimiwa Lema alikuwa Tarime kwa ajili ya kugombania maiti, amesema uongo tunaomba athibitishe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamaliza, kipengele (g).

**MWENYEKITI:** Mwongozo unatolewa kwa jambo moja tu.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** *Okay,* amefanya mambo mawili ya kuudhi.

**MWENYEKITI:** Sasa basi yatakuja kwa utaratibu mwingine maana kama ni mengi kiasi hicho maana yake shughuli iliyoko sasa kwenye *Order Paper*, kwanza kaa.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni (a) na (b) amevunja kwa wakati mmoja.

**MWENYEKITI:** Kwanza kaa!

Waheshimiwa Wabunge, kama kuna kitu ambacho ni rasilimali kubwa katika Bunge ni muda wake, sasa kwa kuwa tuna mambo hapa mahsusi ambayo yapo na hizi *politics* za vyama vingi na Mabunge ya vyama vingi lazima tuwe na *torelance*, vinginevyo tutatumia muda wa Bunge ku-*address* mambo ambayo wananchi hawana shida nayo.

Mimi kwa kutumia hiki kifungu ambacho umekiomba kwa sababu Mwongozo unaombwa kwa jambo moja na mahsusi na si mengi kiasi hicho, nina- *rule out* kwamba mimi nilimsikia vizuri Mheshimiwa Lema alisema yeye alikuwepo Nyamongo na kwamba alizuia mazishi yale, naomba Msemaji anayeendelea tuendelee. *(Makofi)*

Naomba nimuite sasa Mheshimiwa Stephen Masele.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti. Kwanza niwashukuru sana wananchi wote na wapiga kura wangu wa Jimbo la Shinyanga kwa kuniunga mkono wakati wote na kupinga maandamano yawe ya machana ama ya usiku na kujielekeza zaidi kufanya kazi ili kujilitea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili napenda kupongeza Bajeti hii kwa kuandaliwa kwa umakini mkubwa na kuzingatia hali halisi ya nchi yetu na hii imeonesha jinsi Serikali yetu ambavyo inaweza kusikiliza maoni ya wadau mbalimbali na ku-*adress* matatizo yaliyopo sasa, naiunga mkono kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposema Bajeti hii haiko halisia na fedha hakuna ni kupotosha umma. Hapa tuko kwenye Bunge la Taifa na wala siyo kikao cha harusi ambacho kinategemea marafiki waweze kuchanga fedha ili kufanikisha harusi. Lakini hapa tunajadili katika Bunge la Taifa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali, mapato ambayo yanapatikana kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge. Kwa hiyo, Bajeti hii ni halisia na tuko kwenye *serious business. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Shinyanga wamenituma kuwa Shinyanga na Kanda ya Ziwa tunakabiliwa na njaa kubwa sana. Sasa hivi wakazi wa Shinyanga wanashindia chakula mlo mmoja, naishukuru Serikali na nashukuru Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kusikia kilio changu na kuweza kuleta chakula cha msaada Shinyanga na sasa kimeanza kugawiwa kwa wananchi. Lakini chakula kile hakitoshi, na *ration* inayotolewa

kwa wananchi ni kidogo sana, wanapewa kilo kumi kwa kaya moja na sisi Wasukuma tunasifika kwa kula, kwenye suala la kula hatuna mzaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali iongeze *ration* ya chakula kwa kaya, badala ya kilo kumi iongeze mpaka kilo 20 ili kutoa nafasi kwa wenye familia kutafuta chakula cha kujikimu zaidi wakati ikiendelea kupambana na janga la njaa. Lakini lazima Serikali iangalie ni kwa nini mkoa wa Shinyanga hususan Wilaya ya Shinyanga Mjini, Kishapu na Shinyanga Vijijini zinakabiliwa na njaa kila mwaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Bunge la mwezi wa nne nilichangia hapa nilisema lazima Serikali iweke fedha nyingi kwenye kilimo cha umwagiliaji, si kwamba Shinyanga hatupati mvua, tunapata lakini ni mvua chache. Kama Wizara ya Kilimo itatenga fedha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji tukaweza kuvuna maji ya mito ambayo inatiririka na kupotea nina hakika tutaweza kufaulu kupambana na janga la njaa. Lakini nashukuru kwenye Bajeti ya kilimo imeongezewa fedha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na mimi naomba Serikali iweze kusimamia fedha hizi ziweze kufanya kazi iliyokusudiwa haswa kwenye miradi ya kilimo cha umwagiliaji. Pale Shinyanga nina miradi miwili ya kilimo, Mwamalili pamoja na Mwamashele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya maji tunashukuru mkoa wa Shinyanga tumepata maji kutoka Ziwa Victoria, lakini sasa hivi tuna tatizo, maji yale hayajaweza kuwafikia wananchi walio wengi, tunashukuru kwenye Bajeti, Serikali imeweze kuzingatia kuongeza fedha za usambazaji wa maji ili yaweze kuwafikia wananchi wengi.

Lakini maji ni huduma muhimu kwa wananchi, maji siyo anasa, wananchi wa Shinyanga wamenituma niiombe Serikali kwanza iipandishe hadhi Mamlaka ya Maji ya *Shinyanga (SHUWASA)* kwa kuwa inahudumia Wilaya mbili sasa, Wilaya ya Shinyanga Mjini pamoja na Wilaya ya Kishapu iweze kupata ruzuku ya Serikali na hatimaye iweze kusimamia huduma na *maintanance* za mitandao ya maji ambayo kwa sasa wananchi wanabebeshwa mzigo mkubwa wa kulipa bei kubwa ya maji. Wananchi wa Shinyanga wameniambia kabisa ikiwezekana panda hata juu ya meza uhakikishe bei ya maji inashuka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sehemu ya elimu kwa kweli inasikitisha kuona kwamba Mkoa wa Shinyanga umetengewa fedha kidogo sana kwenye elimu. Sote tunafahamu tuna shule chache kulinganisha na mikoa mingi, shule za sekondari ni chache, shule za msingi ni chache lakini mbaya kuliko yote Manispaa ya Shinyanga ikiwa ni Makao Makuu ya Mkoa hakuna *high school* hata moja na Halmashauri yetu imebebeshwa mzigo wa kuhakikisha inajenga shule lakini fedha zilizotengwa ni kidogo sana. Naomba Serikali kupitia Wizara ya Elimu ihakikishe kwamba inatenga fedha za dharula kujenga *high school* kwa sababu wananchi wengi wanahitimu kidato cha nne na hawana sehemu ya kwenda kusoma elimu ya juu ya sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika afya tuna mradi wa siku nyingi, sasa imepita miaka sita tangu Bunge la Tisa kujenga hospitali ya mkoa, lakini cha ajabu imetengwa

jumla ya shilingi milioni 68 kwa ajili ya kuanzisha ujenzi wa hospitali ya mkoa. Fedha hizi ni kidogo sana, hazitoshi hata kujenga zahanati ya kijiji. Naomba Serikali na Wizara ya Afya ihakikishe kwamba inatenga fedha za kutosha kuanzisha mradi wa kujenga hospitali ya mkoa ili iweze kuhudumia wakazi wengi wa mkoa wa Shinyanga. Kwa sasa wakazi wa Wilaya ya Shinyanga Mjini, wakazi wa Wilaya ya Kishapu na Shinyanga Vijijini wanatumia hospitali ya Shinyanga Mjini ya Wilaya ambayo inatumika kama ya mkoa ambayo haitoshi. Naishukuru Wizara ya Afya kwa kukubali ombi langu la kuifanya hospitali ya Kolandoto kuwa hospitali ya ubia na Serikali hilo ni suluhisho la muda tu lakini haiizui Serikali kujenga hospitali ya mkoa kwa ajili ya kuhudumia wakazi wa Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nakua nikiwa mdogo mwalimu wangu mmoja aliwahi kuniambia hadithi ya *the three sleeping giants*, sasa nilipokuwa baadaye nikauliza maana yake ilikuwa nini? Aliniambia *the three sleeping giants* akimaanisha ni Shinyanga, Mwanza na Tabora kwamba sisi ni majitu makubwa lakini tumelala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeamka, tunaomba Serikali iwekeze katika elimu katika mkoa wa Shinyanga, itusaidie katika afya, mambo mengine mtuachie wenyewe tutaweza kujikimu kutafuta fedha kujenga uchumi wetu. Lakini Mkoa wa Shinyanga umesahaulika kwenye afya, elimu na sisi tunachangia sehemu kubwa ya Pato la Taifa. Hii keki ambayo tunaichangia wote, haya mapato ambayo wote tunayachangia basi yagawanywe kwa uwiano na kuangalia kule kunakochangia zaidi na penyewe pananufaika. Sina mashaka na Bajeti hii kwa sababu nafahamu pamoja na kuwa naunga mkono Bajeti  na hata rafiki zangu wa Upinzani, rafiki yangu Mheshimiwa David Silinde najua pamoja na maneno mengi lakini anaiunga mkono Bajeti hii kimoyo kimoyo na ndiyo maana hata mimi natumia muda wangu kwenda kuwaona Mawaziri na kuwaomba kukamilisha miradi hii kama rafiki yangu Mheshimiwa David Silinde anafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali Bajeti hii imelenga vizuri kumsaidia Mtanzania wa kipato cha chini na haswa kwenye kukubali kununua mafuta *bulk procurement*, kwa kununua mafuta mengi hii itasaidia kuondoa tatizo la mfumuko wa bei wa bidhaa zetu  nyingi na hata kupunguza makali ya maisha ambayo yanawakabili Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya ardhi wengi wameizungumzia lakini nilikuwa naomba pia Serikali iweke mkazo katika upimaji wa ardhi. Itenge fedha kwa ajili ya kupima ardhi na wananchi waweze kunufaika na ardhi zao. Leo hii wananchi wengi wana ardhi lakini hawaweze kuzitumia kujipatia mikopo ili kuweza kujikimu kiuchumi. Lakini niipongeze Serikali pia kwa kukubali kuiweka kwenye mpango wa benki ya *TIB* ambayo kwangu mimi naamini ni ukombozi mkubwa wa kiuchumi kwa Taifa letu. Benki ya *TIB* katika mipango yake tunafahamu imejielekeza zaidi katika kilimo na mifugo pamoja na kuendeleza miundombinu. Nimefurahishwa kuona imetengewa shilingi bilioni 100 kila mwaka na naomba Wizara ya Fedha ihakikishe kwamba benki ya *TIB* inakuwa benki kubwa zaidi Tanzania na kuweza kuhudumia wajasiriamali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Watanzania na Wabunge wote hapa tunazungumza sana kuhusu uchumi na tunapigania wananchi waweze kujikomboa kiuchumi hasa kupitia ujasiriamali. Lakini ni muhimu sisi kama viongozi pia tuwaelimishe wananchi, leo hii Mtanzania akionekana anapata fedha anaitwa fisadi, mtu akionekana tajiri anaitwa fisadi, tuhukumu dhambi kwa jina lake, kwa kufanya hivyo tunalinyima Taifa mapato kwa sababu Watanzania wengi wanapopata fedha inabidi wajifiche na wanainyima Serikali mapato kwa kuhofia kuitwa majina ambayo hayafai. Tusioneane wivu wenyewe, Watanzania tukubali kujisifia wale wanaofanya vizuri kwenye uchumi na tuwape *support* ili waweze kushika uchumi wa nchi. Leo hii nchi yetu tunashukuru Serikali imepitisha Sheria ya *PPPA.*

Mheshimiwa mwenyekiti, Sheria hii itaisaidia Serikali kupitia na watu binafsi kushikilia uchumi wa nchi. Tunapozungumzia mifano kama ya China wenzetu wako katika *state capitalisim*, Serikali inashikilia na raia wake wanashikilia lakini sisi hapa raia akijitokeza Mtanzania kushikilia uchumi kwetu sisi inakuwa ni kosa. Nilimsikiliza kwa makini Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi alisema ni lazima tudhibiti tabia, mwenendo wa tabia zetu, tukifanya hivyo na tukajivunia Watanzania kushika uchumi wetu hakika uchumi wetu utakua. Lakini leo hii tunapigania uchumi ukue lakini wakati huo huo Mtanzania akipata uchumi mzuri tunaanza tena kumwita fisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sisi viongozi kama Wabunge na wengine tuanze sisi kwa mfano na tuwaambie wananchi kwamba Mtanzania kuwa tajiri siyo ufisadi na siyo kosa na tuwaunge mkono ndugu zetu Watanzania ambao wanajitokeza kwenye uwekezaji wa ndani na tuache kuwatukuza wawekezaji wa nje na kuwapuuza wawekezaji wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya shilingi imekuwa inateremka kila siku, naunga mkono mchangiaji mmoja amezungumza hapa asubuhi, ukienda nchi zingine ukiingia tu unatakiwa utumie pesa ya nchi ile, lakini Tanzania hapa tumehalalisha matumizi ya *dollar* na kwa kufanya hivyo tunapunguza *demand* ya shilingi. Naomba Wizara ya Fedha isimamie sheria ile, matumizi ya shilingi yawe ya lazima kwa mgeni yeyote anayeingia Tanzania, kwa kufanya hivyo tutaongeza *demand* ya shilingi na thamani ya shilingi yetu itaongezeka. Leo hii mtu analipa mpaka *bill* ya chakula kwa *dollar*, shilingi yetu tunaipeleka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Stephen Julius Masele kwa mchango mzuri na kutumia muda vizuri. Anayefuatia sasa nitamuita Mheshimiwa Pauline Gekul, atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratias Ntukamazima na kama muda utatutosha Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah ajiendae.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuweza kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Bajeti hii ya mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niweze kupongeza Waziri Kivuli wa Fedha wa Kambi ya Upinzani aliyeweza kuandaa Bajeti nzuri ambayo imeweza kubainisha vipaumbele mbalimbali na vyanzo mbalimbali vya mapato. Imani yangu ni kwamba Serikali imesikia na inaweza ikaiga kutoka huko kwa sababu ni vyanzo vizuri vinaweza vikawasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia Bajeti ya Serikali kwa miaka mitatu mfululizo tangu mwaka 2009/2010, 2010/2011 na 2011/2012. Nimejifunza kitu kimoja kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunatumia *equation* ya *deficit* katika kuandaa Bajeti zetu. Kuna *equation* kama tatu, ya *surplus*, *balance* na *deficit*. Ukiangalia tangu tumeanza kubajetia nchi hii hatujawahi kusogelea hata kipengele cha *balance* kwamba mapato ya ndani yanaendana walau hata na matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka utaona kwamba Bajeti yetu tunaendesha kwa mapungufu. Nitoe mfano mzuri, mwaka 2009/2010 mapato au makusanyo ya nadani yalikuwa shilingi trilioni tatu lakini matumizi yalikuwa shilingi trilioni sita ya kawaida. Mwaka 2010/2011 makusanyo yalikuwa shilingi trilioni nne wakati matumizi yalikuwa shilingi trilioni saba, lakini mwaka 2011/2012 tunategemea kukusanya mapato ya ndani shilingi trilioni sita wakati Matumizi ya Kawaida tunategemea kwenda kutumia shilingi trilioni nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti hii shilingi trilioni 13 ambazo tunategemea kuzitumia, shilingi trilioni nane ni Matumizi ya Kawaida. Hii inatufundisha nini? Kwamba nchi hii tuna rasilimali nyingi, tuna vyanzo vingi sana, tuna maliasili, madini, ardhi lakini tumeshindwa kubajetia kwa ujumla kwamba jinsi gani kile kidogo ambacho tunakikusanya tukitumie kwa utaratibu na kiweze kukidhi mahitaji ya kawaida tu tusiendelee kukopa. Watu wanasifia hii Bajeti kwa kiasi kikubwa kwamba ni Bajeti ambayo inaenda kugusa matatizo ya Watanzania, lakini tujiulize itakwenda kugusa vipi kama nusu nzima ya Bajeti tunategemea wahisani watuchangie halafu na Serikali pia ikope? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba kwa Tanzania inayoadhimisha miaka 50 ya Uhuru Deni la Taifa linapofikia shilingi trilioni 17 lazima Watanzania tupige mahesabu, kama tuna wataalamu wa uchumi watusaidie, nchi inadaiwa kwa miaka mitatu mfululizo kwa makusanyo ya shilingi trilioni sita kwa mwaka mapato ya ndani. Kidogo lazima tujiulize kwamba tunakoelekea ni wapi? Je, mwaka 2015 siyo tutakuwa tunadaiwa miaka mitano mbele? Hii inatufundisha kwamba Serikali iangalie katika matumizi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa *analysis* au uchambuzi wa Bajeti kwa ujumla wake, naomba nijikite katika suala la utawala bora. Wachangiaji wengi wameweza kuzungumza kwamba nchi hii tunahitaji amani, hatuhitaji kuona maandamano na kadhalika. Lakini mimi nijikite katika suala zima la utawala bora katika Vyuo Vikuu katika nchi hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi sana tumekuwa tukiona kwamba kuna matatizo, migomo Vyuo Vikuu hata siku moja huwezi kusikia kwamba imeisha. Utasikia kwamba leo Dar es Salaam, kesho *UDOM* na hivi tunavyoongea wanafunzi 400 wa *UDOM* wamefukuzwa au wamesimamishwa masomo, wamerudishwa majumbani wakapumzike kwa ajili ya migomo na hawajui ni lini Serikali inawarudisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naliongea kwa masikitiko makubwa wala siyo suala la vyama kwamba ni chama fulani kinachochea au ni watu fulani wanachochea migomo hii. Mara nyingi tunasikia tuhuma mbalimbali, vitengo vya Serikali vikituhumiana. Utasikia Bodi ya Mikopo inachelewesha fedha au Hazina hawapeleki fedha kwa wakati unaotakiwa. Hili linasikitisha kwa miaka 50 ya Uhuru tunaadhimisha watoto wetu waliopo Vyuo Vikuu wanaandamana kwa kukosa haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatenga Bajeti, tumeona kwamba kuchangia elimu ya juu tangu mwaka 2004 ilivyoanza tulianza na wanafunzi kama 16,000 jumla ya fedha za Kitanzania shilingi bilioni tisa zilitengwa kwa ajili ya kugharamia elimu ya juu. Lakini tukasonga mbele mpaka hivi tunavyoongea mwaka huu hii Bajeti tunayokwenda kupitisha Wizara ya Elimu nusu nzima ya Bajeti inakwenda kwenye mikopo ya wanafunzi, *almost 319 billion* zinakwenda Bodi ya Mikopo ili wanafunzi wakopeshwe. Lakini Serikali haijifunzi bado kwamba sekta hii ya elimu inakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulianzana wanafunzi 16,000 lakini sasa hivi tunavyozungumza wanafunzi 96,000 wanakopeshwa na Bodi ya Mikopo. Lakini sasa ukiangalia jinsi haki inavyotolewa katika Bodi ya Mikopo kwa wanafunzi, hizi fedha Hazina inachelewesha. Wanafunzi wakiingia mitaani tunaanza kunyoosheana vidole, kuna watu wanachochea migomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niishauri Serikali kwamba hakuna Mtanzania anayependa mtoto wake apambane na polisi, hakuna! Siyo wa Chama cha Mapinduzi wala CHADEMA, hakuna anayependa mtoto aliyefika Chuo Kikuu apambane na nguvu ya dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatia aibu kwani haiwezekani tukawa tunaongeza idadi ya walemavu nchini kwa sababu vijana wanadai haki zao, hii ni aibu. Wanavunjwa mikono na kuumia miguu kwa sababu wanadai haki zao. Suala la utawala bora tunapozungumza ndugu zangu tuangalie *TCU* wanafanya kazi? Bodi ya Mikopo wanafanya kazi? Hazina kwa nini wanachelewesha fedha za wanafunzi mpaka wagome?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naliongea kwa uchungu mkubwa na naomba Serikali iliangalie ili matatizo haya yanapotokea ya ucheleweshaji wa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu isiwe ni wanafunzi wanapambana na nguvu za dola inatia aibu. Serikali inatusikia waweze kuliona hili kwamba hatupendi na hatufurahii kuwaona wanafunzi wanapambana na polisi kwa ajili ya kudai haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala zima la uwezeshaji kiuchumi. Ukiangalia takwimu zinasema kwamba takribani wanafunzi 700,000 wanaoingia katika

soko la ajira ni 40,000 tu ndiyo wanaajiriwa. Lakini ukiangalia takwimu mbalimbali tunaambiwa kwamba idadi ya Watanzania wanapatao takribani milioni 43 ni milioni 31 wanapatikana vijijini, 73% ya hawa Watanzania wanapatikana vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hawa wananchi ambao wengi wao wanaishi katika mazingira magumu, miundombinu mibovu na hakuna umeme hawa ndiyo wengi wanaounda *population* ya nchi hii, ni wengi. Ukiangalia kwamba suala zima la uchumi Serikali imefanya *review* na imejaribu kupitia dira ya mwaka 2025 kuona jinsi gani umaskini unapungua, Serikali imeona kwamba umaskini vijijini haupungui kwa kiasi kikubwa kile ambacho walitegemea mwaka 2025 waweze kuwaambia Watanzania tumepunguza kiasi cha umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hayo kwa sababu gani? Uwezeshaji mkubwa unafanyika mijini, wananchi hawa walio wengi wanaokaa vijijini wengi wao ni mama lishe, wakulima, wafanyabiashara wadogo wadogo na kadhalika. Lakini angalia *contribution* yaani mchango wa Serikali katika kuwawezesha hao wananchi si kubwa vile ambavyo tunafikiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea takribani asasi za fedha kama 43 tu ndiyo zinatoa mikopo au ni asasi za Benki. Lakini ukiangalia akaunti ambazo zimefunguliwa katika Benki hizo ni akaunti kama milioni nne tu, hii inatupa picha ni kiasi gani Watanzania ni wachache ambao wana *access* huduma za Benki lakini huko vijijini huwezi kukuta hizo huduma. Mimi rai yangu kwa Serikali ni kwamba Serikali imeanzisha mifuko mbalimbali mfano Mfuko wa *SELF* kuwezesha wajasiriamali, huu mfuko uongezewe fedha ili vijana Wamachinga ambao wanahitaji kukopa wapate hizo pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna *VICOBA* huko akinamama ambao wanaendesha shughuli zao ndogo ndogo hawawezi kukopeshwa benki, vile *VICOBA* na *SACCOS* ziangaliwe ili akina mama wakope na vijana wapate kukopa pia ili kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala zima la *Tanzania Mortgage Finance Refinance Company* pia Benki ya Maendeleo ya Kilimo katika dirisha la *TIB.* Kupitia madirisha haya tukiboresha mikopo kwa ajili ya wakulima na wananchi wakilima kwa bidii umaskini utapungua. Lakini pia niseme kwamba hili dirisha linapatikana mijini tu, ukienda vijijini ukamuuliza mkulima wa kawaida *TIB* ni nini, hawafahamu. Serikali imelenga kweli kuondoa umaskini kwa wakulima na wajasiriamali wadogo wadogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme haya yote yanawezekana kama Serikali itaweza kukabiliana na matumizi yasiyokuwa ya lazima, kama Serikali itapunguza matumizi ambayo siyo ya lazima kwa sababu tunachoona sasa hivi katika Bajeti hii ni mbio ya mbuzi na farasi. Mbuzi lazima tutaona kwamba ana mwendo mdogo, ukipanda farasi ukavuka kamba farasi anatimua mbio. *TRA* wanakwenda mwendo wa mbuzi wanakusanya taratibu, Serikali wapo mbiom wanatumia kweli! Huo ndiyo ukweli na *TRA* hata wakijitahidi kukusanya kiasi gani kama Serikali mbio zake zitakuwa za farasi za

kutumia wakafungua mianya ya matumizi hatuwezi tukakuta matumizi *TRA* watakusanya, wananchi watakamatwa watalipa kodi bado hatuta-*balance* na bado tutaendesha Serikali kwa *deficit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme kwamba Watanzania wengi wana imani na sisi, tumebahatika tu kuingia humu ndani lakini wengine pia wangetaka kuingia humu ndani tuwatetee kwa haki. Tuongee ukweli, mikopo ipelekwe kwa wakulima, wananchi wajenge nyumba bora lakini pia vijana walio wengi ambao wako soko la ajira hawana ajira tuwawezeshe kupitia mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niseme kwamba Bajeti iangaliwe kwa upya na vizuri lakini pia vipaumbele hivi ambavyo tunavipendekeza vinagusa zaidi ya 73% Serikali isione haya kupekela fedha vijijini tutaondoa na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba nitunze muda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Pailine Gekul kwa mchango mzuri na kutumia muda vizuri. Sasa anayefuatia ni Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina na baadaye atafuatiwa na Munde Tambwe Abdallah na kama muda utaturuhusu Kheri A. Khamis.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie Bajeti hii. Lakini kwanza kwa niaba ya wananchi wa Ngara naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa Marais wanne tangu Uhuru, Marais wenye hekima, waungwana, wanaopenda maendeleo ya watu na wanaopenda amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesona seminari, nitaendelea kumuomba Mungu hata mara moja tusipate kichaa kama Idd Amin wa Uganda, kama Mobutu Seseseko wa Zaire, kama Bokasa wa *Central African Republic* na kama Abacha wa Nigeria. Naomba tuheshimu amani ambayo tumeletewa na Marais hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Kikwete kwa kurudisha utaratibu wa kuwa na mpango wa miaka mitano badala ya kuendelea na ile mipango mifupi ya zimamoto. Namshukuru sana.

Lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na timu yake kwa kutuletea bajeti nzuri, inayolenga kuinua hali za wananchi wa hali zote yaani wananchi wa hali ya chini pamoja na wafanyakazi. Naishukuru sana timu ya *Treasury* ambayo imetuletea bajeti nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchiwa Ngara ningependa nichangie maeneo kadhaa kwa njia ya kuishauri Serikali. Ya kwanza, tukitaka kufanikiwa katika kutekeleza mpango huu wa maendeleo wa miaka mitano pamoja na Bajeti hii

ambayo imeletwa kwetu, la kwanza ni lazima tuhakikishe kwamba tunakusanya mapato ya ndani mengi sana, na hiyo inawezekana kwa sababu tuna vyanzo vizuri sana. Nikianza na utalii kama ilivyozungumzwa kwenye kitabu, utalii pamoja na madini ni maeneo mawili ambayo yanaweza kutuletea fedha nyingi sana kama tutaweza kusimamia vizuri utalii pamoja na madini.

Kwa mfano, kwenye utalii nikitoa mfano wa hifadhi ya Ngorongoro pamoja na *TANAPA.* Hifadhi ya Ngorongoro wakati wowote hasa kiangazi kuna wanyama 25,000 wa aina mbalimbali na wakati wa mvua kuna wanyama 40,000 na watalii wanatoka dunia nzima kuja Ngorongoro kuangalia hao wanyama, na katika hao wanyama tunao *the big five* ambao watalii wanapenda kuwaona ambao ni simba, tembo, nyati, faru na chui. Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na Bajeti hii kwamba tuboreshe hoteli zetu na miundombinu mbalimbali katika mbuga za wanyama pamoja na Ngorongoro ili watalii waendelee kuja. *TANAPA* inasimamia mbuga za wanyama kama Serengeti na nyingine na watalii wengi wanakuja. Kwa hiyo, tunaweza tukapata fedha nyingi sana kutokana na mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunayo *tourist hunting* yaani uwindaji wa kitalii. Kwa muda mrefu hatujapata mapato makubwa sana kutokana na *tourist hunting,* nasikia huko nyuma malipo mengi yalikuwa yanafanywa nje ya nchi. Lakini napenda nimshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Ezekiel Maige ambaye kwa ujasiri ameachia vitalu viwe *open* kwa wote waweze kuomba vitalu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikwenda Zimbabwe na Mozambique, huko hakuna *foreign hunter* au mwindaji wa kitalii kutoka nje ambaye anaweza kuwinda Zimbabwe na Mozambique bila kuingia ubia na *Mozambican* au mwananchi wa Zimbabwe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ezekiel Maige ame-*introduce* hiyo *idea* kwamba ni lazima kuwepo na *joint venture* kati ya Watanzania na hawa wawindaji wa kitalii wanaotoka nje, nampongeza sana. Kwa hiyo, tukiingia kwenye *joint venture* tutaweza kupata mapato kutoka kwenye *tourist hunting. (Makofi)*

Eneo lingine ni madini, madini lazima tuyasimamie vizuri kwa sababu ndiyo tegemeo la wananchi wetu. Tutamkumbuka Mwalimu Nyerere alivyokuwa anachelea kuanza kuchimba madini akisema kwamba hatuna *geologist* wa kutosha ambao watazungumza lugha moja na wawekezaji. Lakini tukaanza kuyachimba ila nadhani ni eneo muhimu sana ambalo litatuletea fedha nyingi na namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha kwamba tulihuisha ile mikataba ambayo imekuwa tata na sasa hivi Serikali ijitahidi kwamba tunakuwa na mikataba mizuri ili tupate utajiri kutokana na madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRA* inaweza ikakusanya fedha nyingi zaidi kuliko inavyofanya sasa hivi, naomba *treasury* iisimamie vizuri *TRA*, watendaji wa *TRA* wawajibike vizuri, walipa kodi wakubwa yaani *big tax payers* watozwe kama ipasavyo, tukifanya hivyo *TRA* inaweza ikatuletea fedha nyingi sana kama watendaji watawajibika vizuri. Lakini pia Serikali za Mitaa ziongezewe uwezo wa kukusanya mapato, wanaweza kukusanya mapato mengi sana, lakini pia kuwepo na usimamizi wa hayo makusanyo

yatakayoletwa na Serikali za Mitaa kwa sababu nasikia huko kuna uvujaji mwingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *informal sector* yaani sekta isiyo rasmi *the sleeping giant* tukii-*tap* tunaweza tukaitoza kodi, sasa hivi hawatozwi kodi lakini nadhani mradi wa MKURABITA, mradi wa kurasimisha mali na biashara za wanyonge itatusaidia kupata fedha nyingi kutoka kwenye *informal sector*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi, tukishakusanya haya mapato naiomba Serikali isimamie vizuri matumizi ya Serikali. Tumeona kwenye Bajeti Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anazungumzia kwamba hati safi kwa hesabu zilizokaguliwa zimeanza kupungua sana. Sasa naiomba Serikali wale wanaohusika kama ni wabadhilifu wapewe adhabu inayostahili na hasa Maafisa Wahasibu yaani *Accounting Officer* ambao ni Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mashirika na Wakuu wa Idara zinazojitegemea waweze kuwajibishwa kama hawatapata hati safi.

Kuhusu mishahara na posho, mimi kama Katibu Mkuu Mstaafu wa Utumishi na mtaalamu ambaye amesomea masuala ya motisha siwezi kuacha kuzungumzia posho. Posho na mishahara ni vitu vinavyowekwa kwa kitaalamu na siyo mambo ya siasa. Kwanza mtumishi au mtu anapoajiriwa anaingia mkataba na mkataba huo unamueleza majukumu yake na haki zake na akitekeleza majukumu yake vizuri ni vizuri apewe mshahara wake unaostahili na posho zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtaalamu mmoja ambaye alianzisha kitu hicho anaitwa Profesa Herbert Simon, yeye alikuwa na nadharia ambayo imeendelea kutuongoza katika kupanga mishahara na posho, niitaje kwa Kiingereza na nitaitafsiri kwa Kiswahili, inasema; *Inducement contribution equilibrium* yaani uwiano kati ya mchango wa mtu katika taasisi yake pamoja na haki zake akishafanya kazi vizuri kwa sababu ana ujuzi ameuweka kwenye taasisi hiyo ni lazima umlipe mshahara mzuri na posho zinazostahili. Lakini ukitaka kuwa na mishahara mizuri pamoja na posho nzuri ni lazima ufanye kitu kinachoitwa *job evaluation. Job evaluation* maana yake nini? Ni uchambuzi wa kazi na kuzipa thamani kazi mbalimbali, ukishazipa thamani kazi mbalimbali basi unazipangia mishahara na posho zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila shaka Tume ya Bunge ya Utumishi ilifanya *job evaluation* kuhusu kazi za Mbunge. Je, Mbunge anafanya kazi gani? Zina uzito gani? Kuna unyeti gani wa kazi ya Mbunge? Baada ya kuona kwamba kazi ya Mbunge ni nyeti na ni muhimu sana kwa Taifa hili ndiyo maana wakatuwekea posho mbalimbali. Kwa hiyo, *sitting allowance* na yenyewe siyo kitu kibaya kwa sababu Mbunge ana makazi mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mimi nina makazi Ngara na hapa Dodoma na ninaingia gharama kubwa sana Ngara na hapa Dodoma na nimekuja na dereva wangu na ninaishi kwenye hoteli. Mshahara ni mdogo sana, usingetosha kama nisingekuwa napata posho ya *sitting* pamoja na posho ya kujikimu. Kwa hiyo, hakuna tatizo kuhusu posho, yote imewekwa kitaalamu kwa *job evaluation.* Kwa hiyo, nawaomba Wabunge

wenzangu wanaopiga kelele kuhusu posho wajue kwamba posho siyo siasa bali ni kitu kilichowekwa kitaalamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nizungumzie mambo ya uwezeshaji yaani *empowerment*. Kwa kweli wananchi wetu kama wenzangu walivyosema, wengi wanaishi chini ya ule mstari wa umaskini yaani *poverty line*.

Kwa hiyo, tunahitaji kuwawezesha wananchi wetu na tunaweza kufanya hivyo kwa kutumia vyombo vilivyopo, kwa kutumia kwa mfano ule mpango wa MKURABITA, mimi huko Ngara kwa kutumia fedha zangu hizo sijui za *sitting allowance*, sijui ni za nini nimemwajiri *consultant* na nimemwacha huko Ngara, anaeneza elimu ya ujasiriamali na amefanikiwa sana, wanajitokeza watu mia mbili, mia tatu kwenye kata mbalimbali wanataka awaweke kwenye vikundi vya *VICOBA* na *SACCOS* ili baadaye niwatafutie mtaji au nisaidiane na Serikali kuwatafutia mtaji. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningeomba Serikali i-*support* benki ya akinamama ambayo nimezungumza na Meneja Mkuu wa Benki ya Wanawake waweze kusaidia wanawake wa Ngara na wanawake wa sehemu mbalimbali. Lakini pia tuanzishe *microfinaces* (taasisi ndogo za kifedha) na mimi na nina mpango wa kuanzisha hicho kitaasisi cha fedha kusudi fedha kutoka *TIB* ziweze kupitia kwenye hicho kitaasisi cha *microfinance* kuweza kusaidia wananchi wa Ngara. Tuige mfano wa yule mtaalam Profesa Yunus Muhammad ambaye alileta mapinduzi sana kule Bangladesh kwa kutumia *Grameen Bank* ambako wanyonge wa Bangladesh sasa hivi wameinuka kimaisha kwa sababu ya hiyo *microfinance* aliyoanzisha Yunus Muhammad. Kwa hiyo, tukitumia *microfinances* zetu na sisi tutawainua watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ngara kwa kweli nilikuwa naangalia *strategic plan* ya Wilaya ya Ngara wakati *per capital income* ya Taifa ni laki sita na kuendelea, sisi ni 170,000, kwa hiyo, bado tupo chini sana ndiyo maana inabidi nijitahidi pamoja kushirikiana na Serikali kuhakikisha kwamba tunainua hali za wananchi wa Ngara.

Kuhusu kilimo, tukienda ukurasa wa 12 wa Bajeti hii, Mheshimiwa Mkulo, umezungumzia kwamba kuna mikoa ambayo ina mabonde mazuri sana kwa ajili ya kulima mpunga nayo ni Tabora, Mwanza, Shinyanga, Kigoma, Pwani, Mbeya, Kilimanjaro, Tanga na Morogoro ukausahau Kagera, na Kagera katika Wilaya ya Ngara ina mabonde mazuri sana kwa ajili ya kilimo cha mpunga na Karagwe ina mabonde mazuri sana, Kagera ina mabonde mazuri sana nasema hivyo kwa sababu baadaye sentensi inasema chini ya utaratibu huu wakulima wadogo wadogo watawezeshwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge muda wako umekwisha.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Muda wangu umekwisha? Mbona sijaenda mbali?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge kwa mchango mzuri.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** *Ooh! My goodness. (Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Anayefuatia sasa na ambaye naamini kwa muda uliopo pengine anaweza akawa msemaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Bajeti ya mwaka 2011/2012. Kwanza kabisa nianze kumpongeza Waziri pamoja na timu yake ya wataalam kwa kuandaa hotuba nzuri iliyogusa maisha ya Watanzania wengi, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea kuongea naomba niongee kitu kimoja ambacho naona kwangu mimi binafsi kimenishangaza sana. Wakati Wabunge wanaendelea kuchangia siku ya leo kuna Mbunge ametamka kwamba hotuba hii Mheshimiwa Waziri ame-*copy* na ku-*paste*. Naomba niseme Mheshimiwa Waziri haku-*copy* na ku-*paste*, Bajeti inajieleza lakini naomba niongee, Mheshimiwa Waziri tunamuamini, tunawaamini wataalam wake wana uwezo wa kufanya kazi kwa hiyo, Bajeti hii nzuri na imewagusa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi napinga kabisa kwamba Bajeti hii imekuwa *copied and pasted*, nashangaa mtu anapokaa na anasema maneno kama hayo mara aseme kwamba Serikali imefanya nini, Serikali hii imefanya mambo mengi sana tumejenga shule, tumeongeza vyuo vikuu, tumejenga zahanati na kadhalika. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Barabara za lami.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Tumejenga barabara za lami sasa hivi unatoka Dar es Salaam mpaka Nzega kwa lami kinabakia kipande kidogo tu cha kufika Tabora uwe na lami na wakandarasi wapo, naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashindwa kabisa kuwaelewa watu hawa sijui hawaoni, sijui wanafanya makusudi, mimi sielewi maana watu hawa wana akili timamu, wana macho, wana masikio na wanaona. Sasa unabaki unajiuliza mambo mengi tu mpaka unashindwa kuelewa, labda mimi niishauri Serikali tuwe na mpango mzuri baada ya miaka kumi au 20 tuandae kitu kinachoonesha tulipotoka, tulipo sasa na tunapokwenda, ili watu hawa wawe wanasoma hata historia maana hawaelewi kama mtu alikuwa anatoka Tabora mpaka Dar es Salaam kwa wiki moja, tunashangaa wanaposema kwamba Serikali hii haijafanya kitu chochote na hiyo pia itapunguza *propaganda* za uongo, watu wanakuwa wanasema uongo bila mpango, kwa hiyo, tukiandaa mpango huo utatusaidia sana kupunguza *propaganda* zinazoendelea za uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, nirudie tena kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa niaba ya wananchi wa Tabora kwa kuanza kutujengea barabara za lami, sisi wananchi wa Tabora tulikuwa na kilio kikubwa lakini sasa hivi tuna

wakandarasi wako sehemu tofauti tofauti, tuna wakandarasi Tabora - Nzega, Tabora - Itigi, Tabora - Ndono, Tabora - Sikonge, tuna imani na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, na ni kuhakikishie tu sisi mkoa wa Tabora majimbo yote ni ya CCM na yataendelea kuwa ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niipongeze Serikali kwa kutupatia pesa nyingi za miradi, tumejenga mabwawa, visima, zahanati, madarasa na kadhalika. Lakini sisi watu wa Tabora tuna maombi maalum katika Bajeti hii, kwenye mambo mazuri hapakosi changamoto, sisi watu wa Tabora soko letu limejengwa mwaka 1960, soko hili mpaka leo bado halijamalizika lilijengwa *shade* zake, lakini pia yalijengwa maduka ambayo mpaka leo hayajamalizika. Halmashauri ya Manispaa mmejitahidi kutoa pesa za ukarabati lakini sasa niiombe Serikali itupatie pesa ili tuweze kujenga soko la kisasa, kwa sababu sasa ile Tabora imekuwa Manispaa, zamani ilikuwa *town council*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Serikali pia ituangalie katika suala zima la hospitali, niliongelea suala la hospitali Mheshimiwa Waziri akanijibu vizuri lakini naomba niongezee tu kwamba ile ilikuwa ni ahadi ya Rais alisema Manispaa ya Tabora tuwe na Hospitali ya Wilaya na sisi kama Tabora tumeliona hilo, tumetenga shilingi milioni 100, tumetafuta kiwanja na tumeanza wenyewe kujenga *OPD*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kila siku kilio na mwenyewe, kwa hiyo, sisi watu wa Tabora tumeanza kujenga *OPD* tukitegemea Serikali itatuongezea pesa ili tupate hospitali ya wilaya tupunguze misongamano mikubwa iliyopo kwenye hospitali yetu ya mkoa ya Kitete, kwa sababu Wilaya ya Uyui haina hospitali ya Wilaya inaenda Kitete, Tabora Manispaa hatuna hospitali tunaenda Kitete, hatimaye msongamano unakuwa mkubwa na tunaweza tukawalaumu madaktari wetu kwamba hawatutibu ipasavyo lakini msongamano ni mkubwa sana. *(Makofi)*

Lakini pia niiombe Serikali kama itashindikana kutupa hela kwa mwaka huu basi wajaribu kutudhamini angalau *NSSF* na *PPF*, ili tuweze kupata soko na hospitali. Vilevile sisi Tabora hatuna ofisi ya Halmashauri ya Manispaa, ofisi zetu zipo kwenye jengo la Mahakama, mahakama hiyo ya toka enzi ya mkoloni. Kwa hiyo, tunakuomba Serikali itusikie tuweze kupata fedha za kujenga ofisi ya Manispaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende moja kwa moja kwenye Bajeti, nianze na *TRA*. *TRA* kuna kitu wao wenyewe wataalam wanaita *bands*, zile *bands* za *TRA* ni makadirio ya mapato ya *income tax* kwa mfanyabiashara, naongelea wafanyabiashara wa chini kuna makadirio ya shilingi 35,000, shilingi 95,000 na shilingi 291,000. Mimi nawaomba Wizara ya Fedha wapanue huo wigo sasa zile *bands* badala ya kutoka kwenye shilingi 35,000 kuingia kwenye shilingi 95,000 hapa katikati waweke kitu kwa sababu hawa wafanyabiashara wadogo, kwa mfano mtu akiwa analipa shilingi 95,000 ana mapato ya shilingi 7,000,000, akilipa shilingi 291,000 ana mapato ya shilingi milioni 14, naamini kabisa kwamba wafanyabiashara wadogo biashara zao hazikui kwa kiwango hicho. Kwa kusema hayo basi, naiomba Wizara iweke hizi *bands* katikati kwa mfano kutoka shilingi 95,000 iwekwe labda shilingi 120,000 watakadiria shilingi ngapi, waweke shilingi 180,000 watakadiria shilingi ngapi, waweke shilingi 250,000 watakadiria shilingi

ngapi, *otherwise* tutawaumiza wafanyabiashara wadogo maana ukimtoa kwenye shilingi 95,000 kwa mapato ya shilingi milioni saba, umlete kwenye shilingi 291,000 kwa mapato ya shilingi milioni 14, utakuwa umemuumiza sana naamini mapato yake hayatakuwa yamepanda kwa kiwango hicho labda kwa ndani ya mwaka mmoja au miaka miwili, naomba Serikali iliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niongezee Waheshimiwa wengi Wabunge wameongelea suala la *income tax* kulipa kabla ya kuanza biashara. Hili suala kwa kweli limekuwa na malalamiko mengi, lakini pia haliko sahihi, unamlipisha mtu kodi ya *income tax* wakati mtu huyu hajaanza kufanya biashara, naomba Wizara ya Fedha waliangalie hili kama itawezekana walirekebishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite moja kwa moja sasa kwenye upande wa mikopo. Kwa kweli tunaelewa bila kukopa maendeleo yatakuwa ni madogo kwenye kila sekta. Naomba niongelee wajasiriamali wa chini, kwenye kukopa urasimu na riba ni vitu ambavyo vimetawala sana, urasimu ni mkubwa sana kiasi kwamba wafanyabiashara wadogo wanashindwa kukabiliana na masharti yaliyopo kwenye mikopo. Kwa mfano, ukienda benki utaambiwa inatakiwa *cash flow*, hati ya nyumba au kadi ya gari, huyu mfanyabiashara mdogo hana uwezo wa kuvipata vitu vyote hivyo, hana mchanganuo sijui wa miaka mitatu wa hesabu zake za biashara anakata tamaa anaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi wanakuwa watu hawa wanakimbilia kwenye mashirika madogo madogo kwa mfano *PRIDE* au *FINCA* kuweza kwenda kukopa kujipatia angalau maendeleo. Ukienda *PRIDE* ni riba ni kubwa sana mtu akikopa shilingi 500,000 riba yake ni asilimia 28, mtu akikopa shilingi milioni 15 kuendelea riba yake ni asilimia 22, sasa asilimia 28 ukishaichukua yote hiyo kwa mwaka mimi nimepata faida shilingi ngapi? Nimelipia ada ya watoto wangu shilingi ngapi? Nimelipia pango langu la nyumba shilingi ngapi?

Naomba Wizara ikae na haya mashirika kama yanaomba vibali au leseni kwa ajili ya kufanya biashara ya kukopesha wafanyabiashara wadogo wadogo maana wanasema wenyewe wanakopesha wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati, wakae wakijua kabisa kwamba wafanyabiashara wadogo wadogo hawawezi kuwa na masharti ya hati ya nyumba, hawatakuwa nayo, hasa akinamama. Kwa mfano *PRIDE,* ukienda *PRIDE* mnaambiwa kwanza kuna kitu kinaitwa *make*, mjiweke watu 50 mnaofahamiana mjiunge ndiyo inaitwa *make*, lakini humo ndani kuna kitu kinaitwa *EG* ya watu watano mnaofahamiana kwamba mtu mmoja asipoleta hela *PRIDE* haina hasara, wenye hasara ni wale jamaa zake ambao sasa itabidi wamlipie yule mtu asipolipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu riba ni kubwa akina mama wengi na vijana wanashindwa ku-*afford* hiyo kitu matokeo yake tutakuwa tunabebewa makochi, mafriji na kuachika kwenye ndoa zetu, maana unapomwambia mume wako kwamba bwana kule *PRIDE* nimeambiwa nikitaka mkopo wa shilingi milioni 1.5 nipeleke hati ya nyumba atakwambia wewe mwendawazimu, shilingi milioni 1.5 ukaweke hati yangu ya nyumba huko? Mimi siwezi kukupa. Kwa hiyo, mimi nitajidhamini kwa vitu vyangu vya ndani

bila yeye kujua sasa siku nitakapokuja kunyang'anywa vile vitu ndiyo patakuwa hapatoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwaombe Wizara ya Fedha wakae na hawa watu wa mashirika madogo, waone hizi leseni zao masharti wanayowapa ni yapi na ni kweli shilingi milioni 1.5 mtu atoe hati ya nyumba? Ni kweli shilingi 500,000 mtu atoe kadi ya pikipiki au gari?

Mimi nadhani siyo sahihi, naamini Serikali yetu ni sikivu, imesikia na itafuatilia, maana bila kufuatilia kwa kweli tutabaki tunasema uchumi umepanda kwa asilimia saba, lakini uchumi kwa wajasiriamali wa chini watakuwa wanaona kama mnawaambia vitu ambavyo hawavielewi kabisa. Kama mtu anakopa shilingi 500,000 anachukua analipa asilimia 28 hawezi kupata faida anaona uchumi haujapanda yeye binafsi kwa sababu maisha yake yapo duni, ana maisha ya dhiki, kwa hiyo, unapomwambia uchumi umepanda kwa kweli anashindwa kukuelewa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ilifuatilie suala hili ili tuweze kupata uchumi mzuri kwa mtu mmoja mmoja wa chini naye aweze kupata keki hii ya Tanzania. Tumeboresha sana, ukienda ukurasa wa 13 mambo ya *VETA*, *SIDO* pamoja na vyuo vyote vya elimu, lakini lengo watoto wetu wasome, waajiriwe na wajiajiri wenyewe, sasa mtu ametoka zake *VETA* amesoma *IT* yake ameamua kufungua ofisi yake anaenda kwenye mkopo wa wafanyabiashara wa chini, anaambiwa lete hati ya nyumba anapata wapi? Anakutana na riba kubwa ndiyo ameanza biashara, tunashindwa kuwawezesha hawa watu, tujitahidi hizi riba zipungue tuweze kuwawezesha. Anaenda kuanzisha ufundi uashi, anasema ngoja nikakope ili nianze kwa sababu nimetoka kusoma, anakopeshwa vipi? Kwa hiyo, nawaomba sana Serikali walione hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala zima la *SACCOS* na *VICOBA.* Nashukuru sana Serikali kwa kuhamasisha *SACCOS* pamoja na *vicoba,* kwa kweli tumejiunga lakini pia tumewahamasisha akinamama na vijana wetu wajiunga na *SACCOS.*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Kengele ya kwanza, jamani ndogo, naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge ahsante sana kwa mchango mzuri na muda uliosalia hakika hauwezi kumtosha msemaji mwingine yeyote, kwa hivyo kwa leo huyu ndiye amekuwa msemaji wetu wa mwisho.

Waheshimiwa Wabunge, wakati wa mjadala wa jioni kumekuwa na maombi mengi ya Mwongozo, wengine Utaratibu na wengine Taarifa. Mambo haya matatu yanayoendesha mijadala hayatumiki vizuri na waombaji na hivyo ukikaa kwenye kiti hapa unashindwa, huyu anaomba Mwongozo au Utaratibu au anatoa Taarifa.

Sasa mimi ninawaomba sana tujaribu kupitia tuone vizuri kwa sababu ukiomba utaratibu maana yake unasema kuna Kanuni fulani imekiukwa kwa hiyo, unairejea na ile Kanuni, lakini ukiomba Mwongozo ni kwa jambo ambalo unadhani linahitaji sasa hapa maamuzi ya Spika, maana yake halionyeshi moja kwa moja kwamba kuna kitu fulani kimekiukwa kwa maana ya Kanuni. Lakini Taarifa inatolewa kwa yule anayesema na hasa kwa jambo ambalo amelisema bila ufahamu wa kutosha ama kwa kutokujua ukweli wake, sasa wewe unampa ukweli wake ili asiwe amesema uongo na akakiuka Kanuni ya 63, kwa maana hiyo unamsaidia. Sasa hapa Utaratibu ni kwamba mtu akipewa Taarifa anasema siitaki hata kama ina ukweli, sasa hii siyo tabia ya Kibunge, Bunge hili linakuwa *recorded* unaposahihishwa maana yake unawekwa vizuri ili *record* zikae vizuri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningeshauri pengine tutumie vizuri haya maeneo matatu maana ndiyo yanayoongoza mijadala yote tutakayoifanya katika kipindi hiki cha Bajeti. *(Makofi)*

Baada ya hii kuna mtu amedondosha *wallet* yake nyeusi.

**MBUNGE FULANI:** Ina hela?

**MWENYEKITI:** Ndiyo ina hela, kwa hiyo awaone Makatibu watampatia, amedondosha katika maeneo haya haya ya ukumbi.

Kesho wachangiaji wetu watakaoanza baada ya kipindi cha Maswali watakuwa ni pamoja na Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mheshimiwa Ali Kheir Khamis, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, na Mheshimiwa Stephen Ngonyani na wengine watafuatia.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno haya naomba niahirishe Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.32 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 17 Juni, 2011 saa tatu asubuhi)*